Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Pili - Tarehe 14 Aprili, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu kwa ajili ya orodha ya shughuli za leo, jana nilikaa Kikao cha Dharura na Menejimenti na tumekubaliana kutokana na lililotokea jana, kwenye Bajeti ya Mwaka 2010/2011 yawekwe makadirio ya kununua mtambo mwingine ili tuwe na mitambo miwili ya sauti wakati wote. Kwa sababu ingekuwa hivyo, lililotokea jana la kuungua kwa sehemu moja ya *control unit* lisingesababisha kwenda kufanya mipango ya dharura. Kwa hiyo, bahati nzuri ni wakati ambao tunafanya makadirio tumeamua hivyo. Katibu kwa shughuli za leo. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

**Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu – CDA**

**MHE. EPHRAIM NEHEMIA MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kujibu swali langu linalohusu Sheria ya Mwaka 1979 inayoutambua Mji wa Dodoma kama eneo maalum la uwekezaji, Serikali iliahidi kuihuisha na kuiboresha Sheria hiyo kabla ya ukomo wake:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa Sheria hiyo imefikia ukomo wake wa miaka thelathini?

(b) Je, ni sababu gani zilizoifanya Serikali ishindwe kutimiza ahadi yake hiyo yenye lengo la kuhakikisha ukuaji wa Makao Makuu ya Serikali Dodoma?

(c) Je, Serikali itatunga lini sheria mbadala ili kuboresha na kutimiza malengo ya sheria ya awali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mbunge, napenda kufanya masahihisho madogo ili kuweka kumbukumbu sawa.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayotambua Mji wa Dodoma kama eneo maalumu la uwekezaji ni ya mwaka 1989 na si mwaka 1979 kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza. Aidha, ukomo wa Sheria hiyo ulikuwa ni miaka 20 na wala siyo 30.

Baada ya kufanya masahihisho hayo, naomba kujibu swali la Mheshimwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua kuwa Sheria tajwa tayari imefikia ukomo wake wa miaka 20.

(b) Kama Serikali ilivyokiri katika kipengele (a) hapo juu, Sheria hii ilifikia ukomo wake tarehe 1 Novemba, 2009, ikiwa ni miezi mitano tu iliyopita. Aidha, ikumbukwe kuwa mchakato wa kutunga/kufanyia marekebisho katika Sheria si wa muda mfupi hususan ikizingatiwa kuwa Sheria husika ina muda mrefu tangu itungwe na haikuwa imetumika sana. Hivyo, kuna haja ya kupitia kwa makini malengo ya sheria wakati ilipoanzishwa na kulinganisha na hali halisi ya wakati huu ambapo kuna Sheria ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kujua ni maeneo gani yanatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na malengo ya wakati uliopo sasa. Hivyo basi, Serikali haijashindwa kutimiza ahadi yake ya kuhuisha na kuboresha Sheria tajwa yenye lengo la kufanikisha ukuaji wa Makao Makuu ya Serikali Dodoma na imo katika mchakato wa kufanya hivyo.

(c) Mchakato wa kupitia na kuiboresha Sheria hiyo ya zamani au kutungwa kwa Sheria mbadala utakapokamilika, Muswada wa Sheria hiyo utawasilishwa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuujadili na hatimaye kuipitisha iwapo watapendezewa.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo lazima nikiri kuwa, hayaleti matumaini kwangu mimi wala kwa Wananchi wa Dodoma Mjini kwamba; Serikali bado inatambua umuhimu ambao ulikusudiwa kuleta maendeleo hapa Dodoma na ambayo yalikusudiwa na ile Sheria ya awali.

Je, kutokana majibu haya ambayo yanakatisha tamaa ni kweli kwamba Serikali bado ina dhamira iliyokuwa nayo wakati inatunga Sheria hii ambayo ni kuleta maendeleo ya haraka Mjini Dodoma na kuutayarisha uwe Makao Makuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda

kumjibu Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, ili kuelewa vizuri maelezo niliyoyatoa kama nilivyosema pale awali lazima kuzingatia hali ya sasa ambapo pia tuna Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambacho pia kinahusisha Dodoma. Sheria ile kama itakavyokumbukwa, japokuwa imekuwepo kwa muda wa miaka ishirini, haikutumiwa vizuri na wawekezaji wengi, badala yake wamekuwa wakitumia Sheria ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Hivyo, tunadhani kwamba, pengine maudhui ya Sheria ile yanaweza yakaunganishwa kwenye Sheria ya Uwekezaji Tanzania, ambayo wawekezaji wengi pamoja na wale ambao wanataka kuwekeza Dodoma sasa wanaitumia zaidi kuliko ile ya zamani.

**SPIKA:** Niliwaona kwa maswali mafupi, Mheshimiwa Nyami na Mheshimiwa Lubeleje, kifupi sana tafadhali.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Sheria haipo na Serikali bado inaendelea kufanya kila kitu Dar es Salaam; je, hili siyo jibu kwamba wahusika katika Serikali hawana nia ya kuuendeleza Mji wa Dodoma kama ilivyokusudiwa na kwamba hilo ni kosa la makusudi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

Nirudie kusema kwamba, Sheria hii ilifikia ukumo wake mwezi wa kumi na moja mwaka jana na katika uhai wake ilitumika mara chache sana. Ikumbukwe kuna viwanda viwili tu ndivyo vilivyonufaika na Sheria hii; Kiwanda cha Vinywaji Baridi cha PEPSI Cola ambacho hakikukaa sana hapa na baadae kikaamia Mbeya; na Kiwanda cha Magodoro ambacho nacho hakikukaa sana hapa kikahamia Dar es Salaam.

Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, tuna Sheria ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambayo wawekezaji wengi pamoja na wale wanaotaka kuwekeza Dodoma, wanaona ni bora na inavutia zaidi na ni nzuri zaidi kuliko ile ambayo ilikuwa imetungwa kwa ajili ya Dodoma pekee.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nina swali dogo tu pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa mwaka jana wakati tunachambua bajeti tuliishauri Serikali kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Makao Makuu Dodoma ni kidogo sana inabidi ziongezwe; je, kwa Bajeti ya 2010/2011 Serikali imezingatia hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwa muda mrefu sasa Makao Makuu Dodoma imekuwa ikitengewa fedha kidogo na hii inajulikana ni hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, Makao Makuu Duniani kote hayajengwi na Serikali pekee, Sekta Binafsi ina nafasi kubwa sana katika ujenzi wa Makao Makuu. Ukienda Abuja, Brasilia, Islamabad na hata Canberra, Miji hii yote imejengwa kwa haraka zaidi kwa kutumia Sekta Binafsi; hivyo, tunatoa rai kwamba, Sekta Binafsi nayo isaidie katika kujenga Makao Makuu na fursa zipo nyingi tu hasa maeneo ya makazi.

Na.17

**Haki ya Mbunge Kupata Taarifa Kutoka Ofisi ya Serikali**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria inayohusu Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge inamuwezesha Mbunge kupata taarifa (*information*) kutoka Ofisi yoyote ya Serikali anapohitaji ili kumuwezesha katika kazi zake:-

(a) Je, kuna mipaka gani katika kutoa taarifa hizo?

(b) Je, kuna taarifa gani ambazo Mbunge hukataliwa anapozihitaji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, fungu la 10 la Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296, Toleo la Mwaka 2002 *(The Parliamentary Immunities, Power and Privileges Act (Cap. 296), R.E., 2002)* limeweka haki mahususi kwa ajili ya Mbunge kuomba na kupewa taarifa kutoka kwa Watumishi wa Umma kwa maneno yafuatayo:-

> *"Subject to this Act and to any statutory or other provisions regulating the disclosure of information by public officers, a member may, on request by himself, be furnished with information by the public officer concerned."*

> Tafsiri isiyo rasmi kwa Kiswahili ni hivi:-
> "Bila kuathiri masharti ya sheria hii na pia masharti yaliyowekwa na au Kanuni nyingine yoyote kwa ajili ya kudhibiti utoaji wa taarifa kwa watumishi wa umma, Mbunge aweza, kwa ombi lake mwenyewe, kupewa taarifa na Mtumishi wa Umma anayehusika."

Kwa tafsiri hiyo basi, maneno "*subject to*" (bila kuathiri) yaliyotumika kwenye fungu hilo, yana maana kwamba, haki hiyo mahusus ya Mbunge kuomba na kupewa taarifa kutoka kwa Watumishi wa Umma, imewekewa mipaka au masharti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimwa Damas Nakei, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mipaka au masharti yaliyowekwa na fungu la 10 la Sheria katika kutoa taarifa zinazoombwa na Mbunge ni yafuatayo:-

- Ombi la kupewa taarifa husika sharti liwe limetolewa na Mbunge mwenye na si na mtu mwingine, kwa niaba ya Mbunge huyo.

- Ombi husika ni sharti lizingatie na kufuata masharti yaliyowekwa na Sheria au Kanuni nyingine yoyote kwa ajili ya kudhibiti utoaji wa taarifa kwa Watumishi wa Umma.

(b) Taarifa ambazo Mbunge akiziomba anaweza asipewe ni zile ambazo hazizingatii na zinakiuka masharti yaliyowekwa na Sheria au Kanuni nyingine yoyote kwa ajili ya udhibiti wa utoaji wa taarifa husika ya Serikali.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Msingi wa swali hili ni pale ambapo Mbunge anapambana au anakutana na vikwazo au anapohitaji taarifa fulani katika kupewa hizo taarifa kwa kukosa ushirikiano kutoka kwa maofisa wanaohusika. Je, Serikali inaweza kusema nini juu ya watumishi au maofisa wanaozuia Mbunge kupata taarifa ambazo zinahusu wananchi wake au zinaweza kumuwezesha kushiriki katika masuala yanayohusu wananchi wake; Serikali inasema nini kuhusu watumishi au maofisa wa aina hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nakei kama ifuatavyo:-

Naomba kuchukua fursa hii, kuwaomba sana na kuwaagiza Watumishi wa Umma wasiwanyime Wabunge taarifa wanazohitaji, isipokuwa nao Wabunge wazingatie kwamba, wasiombe taarifa ambazo zinahusiana na taarifa za siri za Serikali ambazo kwa Kiingereza ni *Classified Matters* na pia wasiombe taarifa zinazohusu Usalama wa Taifa, yaani *National Security Matters,* taarifa zinazohusu Ulinzi na Usalama wa Taifa, yaani *Defence and Security of the United Republic* na pia wasiombe taarifa zinazohusu mwenendo wa kambi au vituo vya majeshi ya ulinzi na polisi kwa kuwa wakiomba taarifa hizo hawatapewa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nadhani Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba, Mbunge pamoja na Bunge majukumu yao makubwa ni matatu; utungaji wa sheria, usimamizi wa Serikali na uwakilishi wa wananchi; na katika majibu yake alipokuwa anajibu alikuwa anasema bila kuathiri masharti na Kanuni nyingine; bila kuathiri masharti na Kanuni nyingine, hayo masharti na Kanuni nyingine ndiyo hizo ambazo amezitaja kwenye jibu la swali la nyongeza la masuala ya usalama au kuna mengine ambayo hayajayataja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali la Mhehsimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Masharti ni pamoja na hayo ambayo niliyataja katika majibu ya nyongeza, lakini pia ikumbukwe kama kuna mahitaji makubwa na duniani kote pale ambapo kuna mahitaji makubwa ya wananchi ikiwa ni pamoja na Wabunge kupata taarifa Serikalini, kumekuwa na michakato ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sheria ambayo inatoa maelekezo kwa undani zaidi. Sheria hii inaitwa *Freedom of Information Act* kwa kawaida.

Katika nchi yetu, muda huu wote haujapata msukumo wowote kutoka kwa Jamii, Wabunge na hata Vyombo vya Habari. Kwa hiyo, ndiyo maana tumeendelea kutumia utaratibu huu ambao unatumika sasa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niseme hatutumii vizuri fursa tuliyopewa na Kanuni ya 81, ambayo inaruhusu Muswada Binafsi na Muswada wa Kamati. Mnapoyaona baadhi ya mambo yamepitwa na wakati, yajadilini na kwa njia hizo mbili kwa mujibu wa Kanuni ya 81, tunaweza kuleta mabadiliko. Nimekuwa nikisema Kamati nyingi zimejiweka katika hali ya kusubiri tu kupokea taarifa, halafu zinakuja hapa kwenye Ukumbi kulalamika kwamba sheria fulani imekaa vibaya. Ninakumbusha kuwa sisi ndiyo tunaotunga sheria.

Na. 18

**Kutosimamiwa Ipasavyo kwa Sheria ya Ardhi**

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na Miji wanashindwa kusimamia vizuri Sekta ya Ardhi hadi kusababisha Serikali kulaumiwa kwa kubomoa majengo yaliyojengwa kwa Sheria ya Ardhi?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kukemea Watendaji wote waliozembea katika masuala haya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zuleikha Haji, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umilikaji na uendelezaji wa ardhi mjini unaongozwa na sheria na taratibu mbalimbali zikiwemo Sheria ya Mipango Miji *(Urban Planning Act. No. 8)* ya Mwaka 2007, Kanuni ya Usimamizi wa Ujenzi Mjini *(The Local Government Regulations*) za Mwaka 2008, *The National Environmental Management Act* ya Mwaka 2004 na *Fire and Rescue Services Act No. 3* ya Mwaka 1985.

Kwa mujibu wa sheria na taratibu hizi, usimamizi wa uendelezaji miji ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo, kama kuna udhaifu wowote basi lawama hizo zinapaswa kuelekezwa kwa Serikali za Mitaa husika kwa kushindwa kutekeleza wajibu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu mbalimbali zilizobainishwa kusababisha usimamizi dhaifu kama uzembe, ukosefu wa maadili, rushwa na upungufu wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuingilia kati kila inapolazimu; kwa mfano, Serikali imewahi kuingilia kati na kuunda timu ili kufanya ukaguzi wa majengo ya maghorofa Jijini Dar es Salaam.

Baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, baadhi ya Watumishi wa Halmashauri za Wilaya na Miji wanashindwa kuisimamia vizuri Sekta ya Ardhi hadi kusababisha Serikali kulaumiwa kwa kubomoa majengo yaliyojengwa kinyume cha Sheria kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- Ukosefu wa maadili ya kitaaluma miongoni mwa Watumishi wa Halmashauri wanaopaswa kusimamia ujenzi ambapo wakati mwingine hutoa vibali vya ujenzi isivyo halali na hivyo kushindwa kusimamia uendelezaji.

- Ukosefu wa watumishi wa kutosha na wenye sifa zinazohitajika katika fani ya usimamizi wa ujenzi kwenye Halmashauri hivyo kukosekana ufuatiliaji unaohitajika wakati wa ujenzi.

- Ukosefu wa vitendea kazi hasa pikipiki/magari kutokana na Halmashauri kukosa uwezo wa kununua vifaa hivyo na hivyo kuwawia vigumu watumishi kufanya ufuatiliaji wa ujenzi katika maeneo yote mijini ikizingatiwa kuwa miji mingi imepanuka sana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua vizuri kuwa kuna haja ya kuwakemea watendaji wanaozembea katika usimamizi wa uendelezaji miji na kwamba, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali zikiwemo kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria watumishi wanaohusika. Aidha, kufuatia matokeo ya ukaguzi uliofanywa na timu ya kuchunguza maghorofa katika Jiji la Dar es Slaam, Serikali ilitoa maelekezo mbalimbali kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri, Miji, Manispaa na Majiji ili kurekebisha hali iliyokuwa imejitokeza. Maelekezo yalitolewa yalihusu mambo yafuatayo:-

- Kupitia na kufanyia marekebisho Muundo wa Idara za Ujenzi na kutengeneza majukumu kwa kila mtumishi katika Idara hizo ili kuondoa mkanganyiko katika shughuli za usimamizi wa uendelezaji.

- Kutunza orodha na taarifa za vibali vya ujenzi vinavyotolewa na kumbukumbu za usimamizi wa majengo yanayoendelea kujengwa.

- Kuanzisha taratibu za kufanya shughuli za kusimamia ujenzi kwa timu (*Task Force*). Hii inalenga kuondoa mianya ya rushwa katika usimamizi.

- Kuweka wazi taarifa za usimamizi wa majengo kwa kuziwasilisha katika Vikao vya Menejimenti na vya Halmashauri.

- Kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za usimamizi na ukaguzi wa majengo.

- Kufanya jitihada za kupata vitendea kazi vya usimamizi wa majengo kama vile pikipiki na magari kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi wa mara kwa mara.

- Halmashauri kuanzisha taratibu za ushirikiano na wadau wengine wanohusika na majengo.

- Halmashuri kuanzisha utaratibu wa kuwaelimisha waendelezaji juu ya Kanuni na Sheria za Ujenzi.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya ufanisi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado nina swali hapo. Yule ambaye amebomolewa nyumba yake ataelewa kwamba kuna matatizo mbalimbali, lakini mwenye kidonda mtampa dawa gani kwa sababu ndiye mwenye jengo, amekaribia kuhamia anakuja kuambiwa sivyo unabomolewa; je, mtampa ushauri gani au *counselling* gani mpaka awe na imani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kuchukua nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anachozungumzia hapa, anazungumzia kitu cha msingi sana. Watu wetu wanajijengea majengo ovyo ovyo, nimeeleza hapa na wakati mwingine vibali vinatolewa na Halmashauri. Ninataka niliambie Bunge lako kwamba, utaratibu tuliouweka sasa hivi ni kwamba, ikibainika kwamba kibali kimetolewa na Halmashauri wakaruhusu wakaenda kujenga nyumba katika eneo ambalo halikustahili kujengwa nyumba, ni lazima tutachukua hatua za kinidhamu kwa mtumishi aliyehusika na Halmashauri husika itakuwa *responsible* kwa tatizo lolote ambalo litakuwa limejitokeza pale.

Tutakwenda kuchunguza na kujua ni taratibu gani zilizotumika mpaka maamuzi yale yakafanyika. Katika hali ya kawaida, hatutegemei kwamba maamuzi yatakuwa yamefanyika kinyume na utaratibu niliouzungumzia hapa kama vikao halali vitakuwa vimekaa *which means* wakati mwingine ninachotaka kusema hapa ni kuwaomba pia na wananchi nao wasiingie katika kushawishi kwamba, wapate vibali vya kwenda kujenga

mahali halafu baadae yanatokea haya yanayotokea hapa. Nilithibitishie Bunge lako kwamba, tutachukua hatua na tutaendelea kusimamia kwa hali ya juu kuona hali hii haijitokezi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba tatizo moja la Idara ya Ardhi ni upungufu wa watumishi; na kwa kuwa tunafahamu maeneo mengi Maafisa Ardhi wamekaa muda mrefu wamejisahau; je, Serikali inasema nini juu ya kuongeza ikama na bajeti kwa ajili ya watumishi na kuwahamisha wale ambao wamekaa muda mrefu kwenye maeneo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai kama ifutavyo:-

La kwanza, linalozungumzia habari ya upungufu wa watumishi, halihusu wale wanaotoka katika Wizara ya Ardhi au wanaotoka katika Halmashauri walioko katika Kitengo cha Ardhi, inahusu pia na watumishi wengine. Utaratibu ulioko hapa sasa hivi ni kwamba, kila wakati tunashirikiana na Wizara ya Utumishi ili kuhakikisha kwamba, watumishi ambao wamepunguzwa katika Halmashuri zetu wanapata nafasi na wanaweza kwenda kufanya kazi katika maeneo ambayo yanaonekana yamepungukiwa na watumishi.

Hili la pili alilolizungumza Mheshimiwa Mgana Msindai la kwamba, watumishi wanakuwa wamekaa kwa muda mrefu katika eneo moja, mimi kwa niaba ya Serikali nakubaliana naye kwamba ni kweli kwamba, wakati mwingine ukimuweka mtumishi amekaa pale miaka kumi na tano, miaka ishirini, unaweza ukapata hili tatizo ambalo linazungumzwa hapa.

Kwa hiyo, tunakubaliana na ushauri wake na tutakwenda kuangalia vizuri jinsi ambavyo tutaweza tuka-*replace*, kwa kawaida utaratibu wetu wa kikazi hautaki sana mtumishi akae mahali kwa muda mrefu akazoeleka halafu akatusababishia matatizo haya. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa bado leo maswali mengi sana kwa Mheshimiwa Waiziri Mkuu, sasa la mwisho kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lile linaloulizwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini.

Na. 19

**Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara**

**MHE. OMARI S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 na 2009/2010 Bunge liliidhinisha shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara:-

(a) Je, Serikali imetumia vigezo gani kwa miaka miwili mfululizo kwa ajili ya ujenzi huo muhimu?

(b) Kwa utaratibu huo wa kutenga kiasi kidogo kila mwaka, je, itachukua miaka mingapi kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo?

(c) Je, Mradi huo utakapokamilika unatazamiwa kugharimu fedha kiasi gani na Serikali imeweka mikakati gani ili Mradi huo ukamilike?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mhehsimiwa Omari Shabani Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali hutenga fedha za miradi ya maendeleo kulingana na uwezo uliopo wa mapato na vipaumbele vya Serikali kwa mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010, Mkoa wa Mmanyara ulitengewa ukomo wa bajeti (*ceiling*) ya fedha za maendeleo za ndani na kati ya fedha hizo, Hospitali ya Mkoa wa Manyara ilitengewa fedha kama ifutavyo:-

| Mwaka | Bajeti ya Mkoa | Hospitali ya Mkoa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2008/2009 | 2,952,791,000 | 2,000,000,000 | 67 |
| 2009/2010 | 2,397,792,000 | 2,000,000,000 | 83 |

Takwimu hizo zinaonesha Hospitali ya Mkoa imepata kipaumbele cha kwanza katika ujenzi wa Hospitali ya Mkoa kwa kutengewa asilimia 67 ya bajeti ya maendeleo mwaka 2008/2009 na asilimia 83 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huu wa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa, Mkoa unatekeleza miradi mingine muhimu ambayo ni pamoja na ifuatayo:-

- Ujenzi wa Nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa;
- Ujenzi wa Nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbulu; na
- Ujenzi wa nyumba ya kupumzika ya Viongozi wa Kitaifa *(Rest House).*

Mheshimiwa Spika, hivyo, kimkoa vigezo muhimu vilivyotumika kutenga shilingi bilioni mbili za Mradi wa Hospitali ya Mkoa ni ukomo wa bajeti *(Ceiling)* ya Mkoa unaotolewa Kimataifa na vipaumbele vya Mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, makisio yaliyofanyika mwaka 2008 yanaonesha hospitali hiyo ikijengwa kwa awamu moja itagharimu shilingi bilioni 16 hadi itakapokamilika. Hata hivyo, kwa kiasi cha fedha kinachotengwa kwa sasa cha shilingi bilioni mbili kila mwaka, itachukua miaka minane kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo ya Mkoa endapo hakutakuwa na ongezeko la gharama. Aidha, kutokana na bei za vifaa vya ujenzi na gharama za huduma mbalimbali kupanda kila mwaka itachukua zaidi ya miaka minane kukamilika kwa hospitali hiyo endapo Serikali haitaongeza bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hiyo kutoka shilingi bilioni mbili zinazotengwa kwa kila mwaka.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (b), makisio ya bajeti ya mwaka 2008 yanaonesha kama hospitali hiyo ingejengwa kwa awamu, ingegharimu jumla ya shilingi bilioni 16 hadi itakapokamilika. Kwa kuwa hivi sasa mradi unaojengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kila mwaka gharama hizo zitaongezeka kadiri bei za vifaa na huduma nyingine zitakavyopanda; ili mradi huu ukamilike mapema, itabidi Serikali ya Mkoa iangalie tena upya vipaumbele vyake ili ione uwezekano wa kuongeza kiasi cha fedha zinazotengwa kwa ajili ya mradi huo kila mwaka kulingana na uwezo wa fedha utakaokuwepo.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili.

(i) Kama asilimia 83 ya Bajeti ya Maendeleo ya Mkoa inatumika kujenga Hospitali ya Mkoa, maana yake ni kwamba, hakuna tena uwezekano wa Mkoa kuendelea kuangalia vipaumbele kwa kuwa fedha zote zitakuwa zimekwisha; na kwa kuwa ili kuikamilisha Hospitali hiyo fedha zinazohitajika ni shilingi bilioni 16; na kwa kuwa sasa hivi Serikali itashindwa kupata bilioni 16; ninasema hivi kwa kuwa Serikali inao uwezo wa kutekeleza mradi wa kujenga hospitali ambayo itashughulikia maisha ya watu kwenye mpango maalum; je, Serikali inaweza kuweka Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara kwenye Mpango Maalum ili fedha hizo ziweze kupatikana? Ninajua kwamba, Serikali tunao uwezo mzuri wa kuchangisha na kutafuta wafadhili.

(ii) Kwa kuwa Mkoa wa Manyara ni Mkoa mpya na hospitali iliyopo sasa pale Babati Mjini inabeba majukumu ya Mkoa na nimesema hilo mara nyingi; na kwa kuwa zimeombwa fedha maalum kwa ajili ya kuiimarisha hospitali hiyo; je, Serikali katika kusubiri hospitali hii ya Mkoa sasa itafikiria hayo maombi maalum ili wananchi wasiendelee kuteseka? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, ni-*declare* kwamba, mimi nimekwenda katika Mkoa wa Manyara na nimeona hayo matatizo ambayo Mheshimiwa Omari Kwaangw' anayazungumzia na ninataka iingie katika *Hansard* akijua kwamba, ninatambua kwamba eneo ambalo linazungumzwa halikuwa na Hospitali ya Wilaya wala halikuwa na Hospitali ya Mkoa.

Vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu anatambua kwamba, hili eneo linalozungumzwa hapa ni eneo ambalo ni Mkoa mpya kwa hiyo, una matatizo yanayozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, nimetoa takwimu hapa na nikaonesha hela ambazo zinatengwa kwa ajili ya mkoa na asilimia kubwa kama anavyosema Mheshimiwa Kwaangw', imekuwa inapelekwa katika Hospitali hiyo ya Mkoa. Wanasema kupanga ni kuchagua, kama tunafika mahali tunaona kwamba Hospitali ya Mkoa ni kipaumbele kwa sababu ya afya ya watu wetu ni sahihi kabisa kupeleka kiasi hicho kikubwa ambacho kimepelekwa pale ili kuwaondolea wananchi hayo matatizo yanayozungumzwa pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lipo tatizo la msingi lililoko pale kwa maana ya kwamba ni mkoa mpya hauna hiyo huduma. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaliona ndiyo maana tumekuwa tunafanya hivyo mwaka hadi mwaka. Tumewaangalia wenzetu wa Singida wamefanya nini, wamekwenda na hela hizo kidogo kidogo na wakawa wanajenga kwa awamu; wamejenga *OPD*, wamekwenda wakajenga mahali ambapo watakaa akina mama na watoto na wakaenda kwa awamu mpaka wakafikia hatua hiyo. Tumezungumza na Mheshimiwa Kone akatuambia, tumekwenda Mbeya tukazungumza na Mheshimiwa Mwakipesile naye akatuambia jinsi walivyokwenda wakaweka *incinerator,* wakaweka maeneo mengine ambayo ni muhimu kwa kuanzia. Kwa hiyo, tunashauri kwamba, tukienda kwa awamu tutaondokana na hili tatizo ambalo limezungumzwa hapa.

Namba mbili, amezungumzia habari ya maombi maalumu na Serikali inaulizwa hapa habari ya maombi maalum. Serikali imesisitiza kwamba, hii bajeti ni *Cash Budget* maana yake huwezi kwenda nje ya bajeti kama ilivyopitishwa na Bunge, lakini hapo amezungumza habari ya wahisani ambao amewaita wafadhili; mimi nafahamu kwamba ni wahisani. Ninataka niahidi hapa kama Serikali tutashirikiana na Mkoa, tunao wataalam ambao wanaweza kutusaidia kuandika *write-up* ili tuweze kuondoka katika hili tatizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kwaangw' ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, tunakukaribisha na sote tutakuwa pamoja kushirikiana tuone kama tunaweza tukawapata watu wengine ambao wanaweza wakatusaidia tuondokane na tatizo hili.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ni zamu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Susan Lyimo, badala yake atauliza Mheshimiwa Said Amour Arfi. Naona tuendelee na utaratibu ule ule, likiwa swali la msingi ni la Mbunge Mwanamke basi kwa niaba yake anauliza Mbunge Mwanaume na vinginevyo. *(Kicheko)*

Na. 20

**Utaratibu wa Uchapishaji wa Vitabu wa Shule**

**MHE. SAID A. ARFI (K.n.y. MHE. SUSAN A. J. LYIMO)** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1992 Serikali kupitia Wizara ya Elimu ilitoa tamko kwamba itajitoa katika kuchapisha vitabu na pia mwaka 2004 Kamati ya Kuthibitisha Vifaa vya Elimu iliundwa ili kuwezesha uwepo wa vitabu vya aina mbalimbali lengo likiwa ni kutoa ushindani kwa wachapishaji na kusambaza vitabu shuleni ilimradi wapate vibali kutoka *Educational Materials Approval Committee (EMAC)* na mwaka 2005 Serikali ikapeleka madaraka ya kununua vitabu shuleni:-

Je, ni kwa nini Serikali imebadili utaratibu huo na utaratibu huu mpya uliotangazwa utaanza lini?

**NAIBU WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1991, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni, ilipitisha Sera ya Vitabu Vingi vya Kiada. Wizara ilitoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 1998 ambao ulianzisha Kamati ya Kutathmini Vifaa na Machapisho ya Elimu EMAC na Waraka huo ulifutwa na Waraka wa Elimu Na. 7 wa Mwaka 2005 ambao ulibadili Wajumbe wa EMAC.

Mheshimiwa Spika, lengo la Sera ya Vitabu Vingi vya Kiada lilikuwa ni kubadili mfumo wa utoaji na usambazaji wa vitabu ambapo usambazaji wa vitabu ungefanywa na wachapishaji binafsi badala ya Serikali ilimradi vitabu vitakavyochapishwa vipate ithibati ya EMAC.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Vitabu Vingi vya Kiada imekumbwa na changamoto kadhaa zikiwemo:-

- Kutokuwepo kwa ukomo wa vitabu vya kiada vinavyotumika shuleni na shule zilizo mbali na mji kutopata mahitaji ya vitabu vinavyohitajika.

- Suala la uchapishaji limekuwa la kibiashara zaidi badala ya kuzingatia taaluma.

- Kuwepo kwa aina nyingi za vitabu vya kiada ambavyo vilitofautiana Wilaya moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Serikali imeamua kubadili utaratibu huo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeunda Tume ya Wataalam ambayo miongoni mwa majukumu yake ni kupendekeza utaratibu wa kupata *Standard Texbook(s).* Tume hiyo inaendelea na kazi iliyopewa na pindi kazi hiyo itakapokamilika na kukubaliwa na Serikali ndipo utaratibu huo mpya utakapoanza kutumika.

**MHE. MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa maamuzi yanachukua muda mrefu kuchukuliwa hatua kama majibu yalivyo kwamba Serikali ilipitisha Sera ya Vitabu Mwaka 1991 na Waraka ukaja kutolewa mwaka 1998, miaka saba baadaye; na miaka saba tena baadaye imekuja kufutwa kwa Waraka mwingine Na. 7, kwa hiyo maamuzi yanachukua mrefu; je, kwa nini tunachukua muda mrefu katika kufikia maamuzi na ndiyo maana mmeunda Tume ya kuchunguza nayo itachukua miaka saba?

(ii) Nini athari inayowagusa watoto moja kwa moja kwa kuchelewa kutoa maamuzi kwa wakati muafaka?

**NAIBU WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, suala la vitabu vya kiada linagusa taaluma na mchakato mzima wa mtaala ukiwemo mihtasari. Hivyo ni vyema kupata ushauri wa kitaalam na hasa ukizingatia kwamba, vitabu vinagusa fedha na ni fedha nyingi; hivyo basi, inabidi kutumia busara na hekima zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nithibitishe kwamba, hivi sasa kwa kushirikiana na wachapishaji wa vitabu, Serikali yako Tukufu, imeshapitisha baadhi ya vitabu ambavyo vimeanza kutumika na tumeshirikiana na wachapishaji wenyewe, wameshaanza kuvisambaza vitabu hivyo kwa kupitia Mashariki na Magharibi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpatia Mheshimiwa Arfi namna ya kutawanya vitabu hivyo wakati zoezi lingine la kupata kitabu kimoja likiendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Kwa kifupi sana, Mheshimiwa George Simbachawene, halafu Kaimu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dkt. Slaa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa utaratibu unaosemwa hapa ni ule unaowezesha mfumo wa utoaji vitabu kwa shule za msingi, wengi tunafahamu hapa kwamba, kwa sekondari hatuelewi ni mfumo gani ambao unatumika kuwafikishia vitabu lakini pia imekuwa ni kama sisi viongozi wa kisiasa ndiyo hasa tunaotoa michango na kusaidia shule zetu za sekondari na mimi nimenunua vitabu vya shule zangu zote 12 za sekondari za Kibakwe; je, Serikali inasema kuna utaratibu gani na ni nani anayewajibika kupeleka vitabu kwenye Shule za Sekondari? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, mwenye wajibu wa kusambaza vitabu shuleni ni Serikali kwa kupitia Halmashauri zake. Serikali Kuu huingiza kwenye bajeti fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya maabara na kadhalika. Siku si nyingi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na TAMISEMI, tumesambaza vitabu nchi nzima vya masomo ya hisabati, baiolojia na kemia.

Niseme tu kusema kwamba, Maafisa Elimu wa Mikoa wanafahamu hilo kwa sababu tuliwaomba waje wavichukue vitabu hivyo Desemba na mwezi huu wa nne tayari tumepata ziada ya vitabu na vitabu hivyo tunavipata kwa kushirikiana au kwa kupata msaada kutoka nchi ya Marekani *USAID.* Kusambaza vitabu ni jukumu letu, Mheshimiwa Mbunge anaponunua ni mapenzi yake kwa jimbo lake. Tunawapongeza wote wanaofanya hivyo, tunawaomba waendeleze ari hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati yako ya Bunge ya *LAAC*, huwa inapita Wilaya zote na kati ya mambo inayokagua ni upatikanaji wa vitabu; na kwa kuwa Kamati yako imeona baadhi ya matatizo aliyoyasema Waziri hasa kwa kuwa mradi huu unatumia fedha nyingi na Waziri amesema kuna tatizo kwamba vitabu vinafanywa vya kibiashara; kwa miaka minne sasa taarifa inayopelekwa Wizarani ni kwamba kuna asilimia 40 kila mwaka inatumika kwa fedha za MMEM kununulia vitabu na kwamba uwiano wa kitabu kwa kitabu kwa mtoto ni moja kwa tatu lakini Kamati yako imeona kwamba taarifa hizo si kweli; na kwa kuwa Serikali imeunda Tume; je, iko tayari sasa kuchunguza kama kweli fedha zote zinazopelekwa tangu tumeanza MMES asilimia 40 na bado tunapeleka asilimia 40 fedha hizo hazitumiki vizuri; na je, tutapeleka asilimia 40 mpaka lini vitabu vitakapokuwa vimekamilika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali yako tukufu inayo taarifa kwamba, bado hatujaweza kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa watoto watatu. Taarifa hizi tunazipata kwenye ziara na hata pale tunapoagiza taarifa mbalimbali. Zipo baadhi ya shule ambazo zimefikia kiwango hiki lakini zilizo nyingi bado.

Mheshimiwa Spika, Tume iliyoundwa si kwa ajili ya kuchunguza ni kwa ajili ya kuangalia mwenendo mzima wa upatikanaji wa vitabu vya kiada wa shule za msingi. Naomba niseme jumla ya shilingi bilioni 143 zimeshatumika kwa ajili ya vitabu MMEM kwa maana ya elimu ya msingi na bilioni 19 zimeshatumika kwa ajili ya vitabu kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sisi sote kama Wabunge, kama Madiwani katika Halmashauri zetu, kuweza kuhoji matumizi ya fedha hizi na wengi wetu tumekuta vitabu hivi vikiwa vimenunuliwa lakini haviwafikii walengwa kwa hofu ya kuvipoteza.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa Walimu wote Wakuu na Wakuu wa Shule kuvitumia vitabu hivi ili kuwapatia wanafunzi waliopo kwenye shule zao haki yao ya msingi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Wazari. Sasa ni zamu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 21

**Ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji Kijiji cha Kirongwe**

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Rorya wanaipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kihistoria iliyoifanya katika kupambana na kudhibiti wezi, unyang'anyi wa mifugo uliokuwa unafanywa na majangili kutoka nchi jirani wakishirikiana na majangili wa ndani:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji katika Kijiji cha Kirongwe mpakani na Kenya?

(b) Je, Serikali iko tayari kutoa vyombo vya usafiri kwa ajili ya Maafisa Uhamiaji katika Kituo cha Uhamiaji kilichopo Wilaya ya Rorya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Philemon Mikol Sarungi, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimshukuru Mheshimiwa Sarungi, kwa ushirikiano mzuri lakini pia kwa jitihada zake za kufuatilia kwa umakini masuala yanayohusu Wanajimbo wake wa Rorya. Wizara inakusudia kuanza ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Kijiji cha Kirongwe kilichopo mpakani mwa Tanzania na Kenya (kandokando ya Ziwa Victoria). Ujenzi wa Kituo hicho tayari umewekwa katika mpango wa utekelezaji wa mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa sasa huduma zinatolewa kupitia Kituo cha Shirati kilichopo umbali wa kilometa 13 kutoka mpakani.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mpango wa utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 93 (Idara ya Uhamiaji), katika mwaka wa fedha 2009/2010, Kituo cha Uhamiaji kilichopo Wilaya ya Rorya kilipatiwa gari moja na pikipiki moja ili kuimarisha shughuli za doria na kukabiliana na uhamiaji haramu katika Wilaya hiyo.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa hali ya uhamiaji haramu Wilayani Rorya inafanana kabisa na Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa sababu inapakana na nchi jirani ya Rwanda; na kwa kuwa matatizo ya vyombo vya usafiri kwa watumishi wetu wa Uhamiaji yako katika kiwango cha juu kabisa Wilayani Biharamulo; je, Serikali iko tayari kuangalia uwezekano wa kutoa vyombo vya usafiri kama ilivyofanya kwa wenzetu walio mipakani na nchi jirani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba, tatizo la vyombo ama vitendea kazi katika maeneo mbalimbali kuhusu Wizara yangu, Waheshimiwa Wabunge mnalifahamu na Bunge lako Tukufu pia linafahamu.

Kitu tunachokifanya ni kwamba, haya matatizo tunayachukua awamu kwa awamu kutegemeana na tunavyopata uwezeshaji wa kifedha, lakini pia tunapokwenda nje ya bajeti. Kwa hiyo, hilo alilolisema Mheshimiwa Mukasa ni kwamba, tunalo katika mpango wetu na katika mtazamo wetu wa kuhakikisha kwamba tunaimarisha maeneo hususan yale ambayo yanapakana na nchi ambazo tumekuwa na matatizo nayo hasa katika maeneo ya kiusalama kwa usalama kwa muda mrefu sana. Ahsante.

Na. 22

**Watoto Wadogo kupelekwa Magereza ya Wakubwa**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema watoto wajengewe magereza yao au wawekwe sehemu maalum kwani wanapokuwa magerezani hukutana na wafungwa wenye tabia mbalimbali kama vile wezi, wabakaji, majambazi, ambapo huweza kuiga tabia hizo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba watoto watashindwa kujirekebisha kitabia kama watapelekwa kwenye magereza hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria zinazoratibu, kuongoza na kusimamia masuala ya mahabusu na wafungwa pamoja na Kanuni za Uendeshaji wa Jeshi la Magereza *(The Prisons Standing Orders)* ya mwaka 2003, kifungu namba 502, vifungu vidogo vya (ii) na (iii), wafungwa watoto wanapopelekwa magerezani wanatenganishwa na wafungwa wakubwa. Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Taasisi zote zenye mamlaka ya kukamata na kuhifadhi wafungwa na wahalifu zinatekeleza sheria hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaliona hili na kulitambua suala la (b); moja kati ya juhudi za magereza ni kurekebisha wafungwa wote kwa mujibu wa sheria niliyoitaja hapo juu katika kujibu swali (a).

Serikali huwapeleka watoto hao katika Gereza la Wami Morogoro na wale ambao hawajahukumiwa hutengwa na wafungwa wakubwa katika magereza walikoshikiliwa hadi hapo Mahakama itakapotoa uamuzi kuhusu hatima yao.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yake mazuri lakini nina swali la nyongeza. Waziri amejibu kuwa wanaohukumiwa hupelekwa Gereza la Wami Morogoro lakini ambao hawajapata hukumu (mahabusu)

huwa wanachanganywa na wakubwa ingawa hutengwa lakini wanatumia gereza moja na wanapopelekwa Mahakamani wote huwa wanatumia usafiri mmoja; je, kwa nini Serikali haiwajengei mahabusu yao na mahakama yao ili kuondosha tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hakika ninaelewa kwamba, suala analoliuliza linatoka moyoni. Yeye kama mzazi, ninajua kabisa ana uchungu na hao watoto wadogo, lakini nataka nimhakikishie kwamba, sheria iko bayana kwamba, kutenganisha kati ya watoto na watu wazima ni utaratibu ambao tumekuwa tunaufuata. Kuhusu suala alilolitaja kwamba katika maeneo ambayo hakuna gereza la watoto utenganishi huu unakuwepo lakini upande wa usafiri wanapokwenda mahakamani wanapelekwa kwa pamoja.

Hilo kwa kweli niseme nikiri kwamba lipo lakini watoto ambao wanafanya makosa kusema kweli idadi yao siyo kubwa kiasi hicho, ukitazama kwa picha iliyokuwa kubwa ya wafungwa wote ambao tuliokuwa nao, lakini tumelichukua hilo na tunalizingatia niseme tu hapa nimwambie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, bado tunakabiliwa na tatizo la uhaba wa vitendea kazi ikiwemo magari ya usafiri.

Hivi sasa tumeanza kupata hata magari ya kuweza kusafirisha wafungwa sisi wenyewe na mahabusu ambao wanakwenda mahakamani. Utaratibu huo tumeanza kuuweka, ambapo magereza wamekuwa na magari yao wenyewe na sasa tukisema kwamba tupanue wigo kuongeza na watoto, nisingependa kutoa ahadi hiyo lakini niseme ni jambo ambalo tumelizingatia.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Suala la ujambazi ambalo liko Bara hali kadhalika Zanzibar, wahalifu wako Bara na Zanzibar, pia watoto ambao wanashtakiwa Bara na kule Zanzibar wanashtakiwa; sasa kutokana na hali ilivyo na wakati huu tuliokuwa nao na ukizingatia Maofisa wengi wa Chuo cha Mafunzo kule Zanzibar wanapata mafunzo yao huku Bara; sasa ili kuoanisha basi mambo haya na kwenda katika Tanzania yenye amani Serikali haioni kwamba sasa umeshafika wakati suala hili la magereza liwe la Muungano kama ilivyo Wizara ya Mambo ya Ndani katika nchi yetu ya Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba, upande wa mafunzo tunakwenda pamoja, upande wa mashirikiano tunakwenda pamoja lakini hili si suala la Muungano. Niseme kwamba, tukijua taratibu zetu jinsi tunavyokwenda sidhani kama hapa itakuwa ni nafasi bora au sahihi kutaja au kutamka kwamba hili kweli sasa lichukuliwe hivyo.

Niseme kwamba ni pendekezo ambalo analiona Mheshimiwa Hafidh Ali na wengi wamelisikia na kwa hiyo tutatazama linakwendaje. Taratibu za mambo yanavyokwenda kimuungano ziko Kamati Maalum ambazo zinashughulikia masuala kama haya; nafikiri kule yanaweza yakazungumzwa vizuri.

Na. 23

**Askari Polisi Kulipwa Malimbikizo Mbalimbali**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo malimbikizo makubwa ya madeni mbalimbali kwa Askari Polisi kama vile posho, fedha za uhamisho na likizo:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho askari wetu wanadai katika malimbikizo hayo?

(b) Je, ni lini Serikali itawalipa Askari Polisi malimbikizo yao ili waondokane na kero hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya madeni ya Askari Polisi yanatokana na posho za safari za kikazi, uhamisho na likizo kutoka mwaka 2001 hadi Juni 2009 nazo ni takriban shilingi 9,227,707,000. Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali itawalipa askari malimbikizo ya madeni yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni tatu na milioni tano. Kwa sasa nyaraka za madeni hayo zimewasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo. Aidha, madeni yanayobaki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali anafanya zoezi la kuyathibitisha na Serikali italipa kwa jinsi uthibitisho utakavyokuwa unapatikana na jinsi bajeti itakavyokuwa ikiruhusu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba italipa shilingi bilioni 3.5 kwa mwaka wa fedha 2009/2010 huku ikielewa kwamba bado miezi michache kipindi hicho kumalizika; je, haioni kwamba ni busara ikatamka bayana kwamba kwa miezi michache hii iliyobaki, yaani April na Mei, ni lini hasa itawalipa madeni hawa askari?

(ii) Kwa kuwa, madeni ya askari yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku; je, Serikali sasa iko tayari katika bajeti ya mwaka 2010/2011 kuandaa mazingira ya kuwalipa madeni yote askari hawa ili dhana ya MKUKUTA iweze kutekelezeka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kwangu mimi ni furaha kutaja kwamba, Mheshimiwa Saanya na Mheshimiwa Masoud ni Wajumbe katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama, ambayo inashughulikia masuala haya na niseme kwamba ni masuala ambayo wamekuwa wakiyafuatilia kwa ukaribu sana. Yeye anafahamu kabisa kwamba, nia ya Serikali na nia ya Wizara yangu ni kuhakikisha kwamba tatizo hili tunaondokana nalo. Sasa kuhusu ni lini; ni kwamba, hapa nivyotamka Mheshimiwa Masoud, nimelitamkia Bunge na nimelitamkia Taifa kwamba katika kipindi cha mwaka huu wa fedha tulionao hizi pesa zitalipwa. Ningemwomba asiwe na shaka, kwa sababu siwezi nikasema kwamba itakuwa kesho au keshokutwa. Hizi nyaraka zipo Wizara ya Fedha na wao wana utaratibu wao na tunasubiri waweze kutuletea hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, ninadhani haitakuwa busara kwangu mimi kutaja kwamba ni lini zitalipwa, nafikiri labda wenzetu wa Wizara ya Fedha, wao wanajua taratibu zao, lakini tumepata hakika kwamba watatulipa hizo fedha ili tuweze kuwapa hawa askari wetu ambao wanafanya kazi nzuri sana katika ulinzi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu haya madai na madeni ya Polisi. Mimi niseme kwamba, suala tunaloshughulika nalo hapa kwa sasa na ambalo ninalijibu ni sehemu ndogo tu ya deni kubwa kwa sababu hili ni deni la Polisi, lakini kuna deni la Askari Magereza, kuna Uhamiaji na pia wapo Wazabuni. Kwa hiyo, wewe mwenyewe unalijua deni hili, Rais ameshalitamka, Waziri Mkuu ameshalitamka na Wizara ya Fedha wanalishughulikia. Kitu hiki kwa kweli kimekuwepo, hakipendezi na tumesema kwamba askari wetu ni lazima walipwe madai yao kwani ni haki yao. Kwa hiyo, ni kitu ambacho tunakifanyia kazi na ni matumaini yetu kwamba, katika mwaka ujao wa fedha, hili suala tutaweza kuachana nalo, yaani tutakuwa tumesema kwamba tumelipa madeni haya ya askari wetu ambao wanatufanyia kazi nzuri katika Taifa letu.

Na. 24

**Kujenga Barabara Za Juu *(Fly Over)* Jijini Dar-es-Salaam**

**MHE. MOHAMMED A. CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa Jiji la Dar-es-Salaam limezidiwa na msongamano wa magari kutokana na ufinyu wa barabara zake:-

Je, Serikali iko tayari kuzishawishi Kampuni au Mashirika binafsi ya nje na ndani kujenga barabara za juu *(Fly Overs)* kama zilivyo nchi nyingine duniani ili kuondokana na tatizo hilo sugu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuyashawishi makampuni na mashirika binafsi ya nje na ya ndani ili kushiriki katika ujenzi wa barabara za juu ama *fly overs.* Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)*, imekamilisha Mpango wa Barabara za Jiji la Dar-es-Salaam, ambao umeainisha maeneo yote ambayo yanahitaji kujengwa barabara za juu. Maeneo hayo ni pamoja na TAZARA, Ubungo, Magomeni, Jangwani eneo la Fire, KAMATA na makutano ya barabara ya Nyerere na Kawawa pale Chang'ombe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, Serikali imekubaliana na Serikali ya Japan, kujenga barabara za juu katika makutano ya TAZARA na Ubungo. Upembuzi yakinifu na usanifu, unatarajiwa kuanza Agosti mwaka 2010. Ujenzi rasmi utaanza baada ya usanifu kukamilika na kulipa fidia kwa mali zote zitakazobainika kuathiriwa na ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano hayo, Serikali ya Japan itagharimia usanifu na ujenzi na Serikali ya Tanzania itagharimia fidia ya mali na uhamishaji wa miundombinu ya huduma za jamii kama vile umeme, maji na kadhalika.

**MHE. MOHAMMED A. CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yenye kutia matumaini, nilikuwa nataka kujua katika kipindi hiki cha mpito mpaka kufikia wakati huo wa ujenzi, Serikali ina mpango gani hasa ukizingatia kwamba kuna mpango uliotangazwa kwamba kutakuwa na mabasi yaendayo kwa kasi ambayo yatachukua abiria kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari njiani?

Mheshimiwa Spika, la pili, mbali ya barabara hizi kuu ambazo zinaingia na kutoka mjini kuna barabara za katikati ya mji sasa hivi zina msongamano zaidi ambao pia unasababisha usumbufu mkubwa, ukizingatia kwamba miundombinu iliyokuwepo ni ya mwaka 47 na magari yaliyopo sasa hivi karne ya 21 ni zmara 10 zaidi; je, Serikali ina mpango gani wa kuratibu mipango hii ili kuwe na wepesi wa huduma za kiuchumi kwa kila siku?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chomboh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mpito, Serikali itaendelea kudhibiti miundombinu ya usafiri katika Jiji la Dar-es-Salaam ili kupunguza msongamano na kupunguza adha ya usafiri katika Jiji. Mradi huu wa mabasi ya kwenda kasi, unaratibiwa na Mamlaka ya *DRT*, ambayo sasa hivi imefikia katika hatua za kuweza kuanza ujenzi na kuweza kumpata muwekezaji ambaye atanunua mabasi hayo. Kwa hiyo, Mamlaka hiyo inaendelea na mpango huu, najua imechukua muda mwingi kushinda vile ambavyo tungependa lakini kwa bahati mbaya taratibu zimekuwa ngumu na ndiyo zimelazimisha mpaka hivi sasa bado mabasi hayo hayajaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Chomboh ni kuhusu barabara katikati ya Jiji; ni kweli tunatambua kwamba, barabara hizi ni finyu kwa maana ya

wembamba, lakini pia kwa maana ya idadi ya barabara katika Jiji la Dar-es-Salaam. Kwa hiyo, Serikali katika kipindi hiki inaendelea kujitahidi kuboresha miundombinu ya barabara katika Jiji kwa kuongeza barabara, lakini pia kwa kupanua barabara. Mpango wa sasa hivi ambao tutaanza nao ni Barabara ya Ali Hassan Mwinyi maungano na Bagamoyo. Ndani ya mwaka huu wa kalenda wa 2010, tutaanza kuipanua barabara hiyo na kuwa barabara mbili kwa kila upande. Hili litafanyika kwa ufadhili wa Serikali ya Japan na pia itatusaidia na barabara nyingine ambazo ziko katikati ingawa ziko kwenye barabara mbili, walau ziwe pana kidogo kuweza kupishana kiurahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka juzi tumeanza Mradi Maalumu wa kuongeza barabara nyingine 10 ndani ya Jiji la Dar-es-Salaam, ambazo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kwa mfano, kuna Barabara ya Ubungo Bus Terminal – Kigogo – Kawawa Roundabout, ambayo sasa hivi imefikia ukamilishaji wa 57% pamoja na nyingine. Zipo hizi 10 na nitampatia Mheshimiwa Mbunge, katika kuzijenga kwake sasa tutaongeza idadi ya barabara katika Jiji la Dar-es-Salaam na kuondosha msongamano ambao umekuwepo kwa muda mrefu.

Na. 25

**Ahadi ya Kujenga Barabara ya Dodoma – Babati kwa Lami**

**MHE. ZABEIN M. MHITA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Serikali iliahidi kutenga shilingi bilioni 45 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Babati, kwa kiwango cha lami, lakini utekelezaji wake bado haujaanza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

(b) Je, Serikali inawaambia nini Wananchi wa Kondoa kuhusu ahadi hiyo ambayo pia ilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza kujenga Barabara ya Dodoma - Babati katika mwaka huu wa fedha 2009/2010. Utekelezaji wa ujenzi katika barabara hii umegawanywa katika sehemu nne kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ni ile ya Dodoma – Mayamaya, yenye urefu wa kilometa 43. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu hii ni Kampuni ya *SINO Hydro* ya China, kwa gharama ya shilingi bilioni 40.6; muda wa ujenzi

umekadiriwa kuwa ni miezi 27. Kwa sasa Mkandarasi yuko katika maandalizi ya kuanza kazi.

Sehemu ya pili ni Mayamaya – Bonga, yenye urefu wa kilometa 204; eneo hili bado halijapatiwa pesa. Mazungumzo kati ya Serikali yetu na Serikali ya Japan kwa ajili ya kusaidia ujenzi yanaendelea vizuri hivi sasa.

Sehemu ya tatu ni Daraja la Mto Kolo, lenye urefu wa mita 60. Zabuni za ujenzi wa daraja hili ziko katika hatua ya uchambuzi ili kumpata Mkandarasi.

Sehemu ya nne na ya mwisho ni Babati – Bonga, yenye urefu wa kilometa 16. Zabuni ya ujenzi wa kilometa 16 Babati – Bonga pamoja na kilometa tatu za mchepuo kuingia Kondoa Mjini kutoka Bicha, ziko kwenye hatua ya uchambuzi ili kupata mkandarasi.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri ya swali langu, lakini naomba ufafanuzi kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jibu la kuwa barabara ya kutoka Dodoma – Babati itajengwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 kidogo linanipa wasiwasi kwa sababu sasa huu ni mwezi wa 10 tangu mwaka huu wa fedha 2009/2010 uanze na bado miezi miwili tu mwaka huu wa fedha uishe; je, Mheshimiwa Waziri, atawahakikishia Wananchi wa Kondoa kwamba barabara hii itaanza kujengwa kabla ya mwaka huu wa fedha 2009/2010 kuisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Daraja la Mto wa Kolo, ambalo lilivunjika tangu mwaka 1997 wakati wa mvua za *El-Nino*; lakini katika jibu tunaambiwa kwamba, sasa zabuni ipo katika hatua ya uchambuzi ili kumpata mkandarasi. Je, hatua hii ni baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu au upembuzi yakinifu na usanifu utafanywa tena baadaye? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dada yangu Zabein Mhita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba, barabara hii imegawanywa katika mafungu manne. Fungu la kwanza la Barabara ya Dodoma – Mayamaya, kilometa 43, kwa maana ya kuanza ujenzi, mkandarasi ameshapatikana. Taratibu zote za usanifu, upembuzi yakinifu, kumpata mkandarasi na kumpata msimamiaji wa mkandarasi, zote zimekamilika na mkandarasi sasa hivi yuko katika hatua za ujenzi. Mkandarasi huyu sasa hivi analeta mitambo kwenye barabara, anaanza kusafisha eneo, kwa maana hiyo ni kwamba, hivi karibuni ataanza ujenzi. Mimi kama Waziri mwenye dhamana ni mategemeo yangu kwamba, *SINO Hydro* ni kampuni

ambayo tumefanya nayo kazi kwa muda mrefu; itawajibika vizuri na kwamba wananchi wataiona barabara hii ikianza kujengwa ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la Daraja la Mto wa Kolo; tunapompata mkandarasi maana yake upembuzi na usanifu vimekamilika. Hatumtafuti mkandarasi kabla usanifu haujafanywa, kwa hiyo, sasa hivi tunamtafuta mkandarasi kwa sababu taratibu hizo zimekamilika na kwa maana hiyo mara tutakapompata mkandarasi, mategemeo yangu ni kwamba, kwa vile sasa hivi uchambuzi ndiyo unafanywa, wakandarasi wameshawasilisha zabuni zao, mkandarasi pia kwa ajili ya Daraja la Kolo tutampata ndani ya mwaka huu wa fedha.

Na. 26

**Mipango ya Kuingiza Nchini Zana za Kilimo**

**MHE. DK. LUKA J. SIYAME** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishaweka mipango ya kuingiza nchini zana za kilimo yakiwemo matrekta makubwa na madogo *(Power Tillers)*, ambayo yangekopeshwa kwa wakulima kwa masharti nafuu na kuwekewa ruzuku ya asilimia 80:-

(a) Je, mipango hiyo imefikia wapi?

(b) Je, utaratibu wa ukopeshaji wa zana hizo utakuwaje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Lucas Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mipango ya Serikali ya kuingiza zana za kilimo yakiwemo matrekta makubwa na matrekta madogo, mwaka 2009/2010 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri za Wilaya kununua matrekta madogo 1,628 na matrekta makubwa 55 kupitia Mpango wa Wilaya wa Kuendeleza Kilimo, yaani *DADPs*. Matrekta hayo yatakopeshwa kwa wakulima kwa utaratibu wa uchangiaji wa asilimia 20 ya gharama za kuyaingiza matrekta hayo nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zinapaswa kuandaa utaratibu wa kuvitambua vikundi vya wakulima ambavyo vimeibua miradi ya kilimo na hatimaye kujiwekea utaratibu wa namna watakavyovikopesha vikundi husika zana wanazokusidia kukopa. Kwa mfano, Wilaya ya Mbozi kwa sasa inakamilisha ununuzi wa matrekta madogo ya mkono 13, yenye thamani ya shilingi 75,197,200 wakati huo huo wakijiandaa na taratibu walizojiwekea katika kuwakopesha wakulima wao matrekta hayo yatakaponunuliwa.

**MHE. DK. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majibu yaliyotolewa kwa sehemu (a) ya swali langu la msingi ni marejeo ama nukuu ya Ibara ya 135, iliyoko ukurasa wa 89 wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya Mwaka 2009/2010; je, hivi sasa Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza uagizaji huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Siyame kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii ni nukuu ya bajeti yetu ya Ibara ya 135, ukurasa wa 89, kama alivyosema na kama ilivyo kawaida kwamba, tunatekeleza bajeti ambayo imepitishwa na Bunge. Kuhusu kwamba tumefikia wapi, nipende kusema kwamba, fedha hizi zinapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, kila Halmashauri imefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa hatua hizi. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Siyame, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, tuuulize kwenye Halmashauri zetu kwamba taratibu za uagizaji wa matrekta haya zimefikia wapi.

Na. 27

**Ahadi ya Kulipa Madeni ya Pamba ya Wananchi wa Mwibara**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wengi wa Jimbo la Mwibara hawajalipwa madeni ya pamba waliyouza kwa *Mara Cooperative Union (MCU)* miaka mingi iliyopita:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kulipa madeni hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali Mheshimiwa Charles Maguguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko makini katika kutekeleza ahadi zake inazozitoa mara kwa mara na hivyo ndivyo ilivyofanya kwa ahadi ya kuwalipa wakulima waliokuwa wanaidai *Mara Cooperative Union* kwa kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizohakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka 2004, *Mara Cooperative Union* ilikuwa inadaiwa na wakulima wa pamba Mkoani Mara shilingi 229,789,629.

Katika hesabu hii, shilingi 43,057,836.65 zilikuwa zinadaiwa na wakulima 767 wa Jimbo la Mwibara la Mheshimiwa Mbunge. Wakulima hao walilipwa Mwezi Mei,

mwaka 2009 kupitia vyama vyao vya ushirika vya msingi saba vya Jimbo la Mwibara, ambavyo ni Nyarugoma, Kenkobyo, Iramba, Nyamitwebeli, Chamgari, Kasahunga na Kibara.

Mheshimiwa Spika, wakulima waliolipwa mpaka mwezi Mei, 2009 ni wale waliokuwa kwenye orodha zilizowasilishwa na kuhakikiwa na Serikali.

Wakulima ambao awali orodha zao zilihakikiwa na kugundulika kuwa zilikuwa na makosa, walikuwemo wa Chama cha Kabarongo kilichopo pia katika Jimbo la Mwibara na sasa wamepelekewa malipo yao na ulipwaji utafanyika mwezi huu wa Aprili, 2010. Jumla ya wakulima hao ni 231, ambao watalipwa jumla ya shilingi 8,571,425.

Na. 28

**Kuboresha Mawasiliano ya Simu za Kiganjani - Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa mtandao wa mawasiliano ya simu za kiganjani umeenea karibu maeneo yote ya Jimbo la Kahama hadi mwaka 2009 ingawa katika baadhi ya maeneo usikivu wa simu bado si mzuri:-

(a) Je, ni lini Kampuni ya *ZAIN* ambayo ndiyo imeeneza mtandao wake katika Jimbo la Kahama itaimarisha usikivu wa mtandao wake?

(b) Je, kwa nini Makampuni ya *TIGO*, *Vodacom* na *Zantel* hayaigi mfano wa *Zain* wa kueneza mitandao yao katika maeneo haya licha ya kukidhi vigezo vyote vinavyohitajika?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kulikuwa na usikivu hafifu wa mtandao wa mawasiliano wa Kampuni ya *ZAIN* katika Jimbo la Kahama, kutokana na kuzidiwa kwa mitambo ya mawasiliano ya Kampuni hiyo.

Matatizo ya kutokuwepo usikivu mzuri katika maeneo ya Jimbo la Kahama, yalitokana na marekebisho yaliyokuwa yakifanywa na Kampuni ya *ZAIN* katika Kanda ya Ziwa ya kubadilisha mitambo ya zamani ya aina ya *Alkatel* na kuwekwa mingine mipya ya aina ya *Huawei.*

Hivyo, tayari *Zain* imeshaongeza nguvu kwa kufunga mitambo mipya ambayo ina uwezo mkubwa na hivyo kuweza kuwahudumia wateja wake vizuri zaidi. Ninaamini kwamba, hivi sasa usikivu katika maeneo mengi ya Kahama umerejea katika hali nzuri kutokana na uboreshaji huo kufanyika.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya *Vodacom* inatambua umuhimu wa kujenga minara ya mawasiliano ya simu za mikononi na tayari imejenga minara katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kahama, usikivu wa mtandao ni mzuri.

Aidha, *Vodacom* inaendelea na juhudi ili kuhakikisha kuwa, tathmini ya kibiashara inafanyika ili kujenga minara saba ya mawasiliano katika maeneo mengine ya Jimbo hilo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Zantel* imeyaweka maeneo ya Jimbo la Kahama kwenye mipango yake ili kuyafanyia tathmini ya kibiashara kwa mwaka 2010/2011. Kampuni ya Simu ya *TIGO,* inao mtambo wake wa mawasiliano katika eneo la Kahama. Hata hivyo, Kampuni hiyo imeahidi kuyatembelea maeneo ya Jimbo la Kahama kuona uwezekano wa kuimarisha mawasiliano kwenye eneo hilo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa pamoja na *Zain* kufunga mitambo mipya, bora na yenye nguvu zaidi, bado baadhi ya maeneo haya ya Kata za Chona, Chambo, Uyogo, Idahina na Igwamanoni, yana matatizo ya usikivu; bado wananchi inawalazimu kupanda juu ya mti au juu ya milima ili kuweza kupata mawasiliano. Je, Waziri yupo tayari kuwabana zaidi *Zain* kuelekeza nguvu ya maboresho yao katika maeneo niliyoyataja ili kuondosha kabisa kero hii?

(ii) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kahama ina Majimbo mawili; Jimbo la Msalala kwa Mheshimiwa Maige na Jimbo la Kahama na yote yana matatizo kama niliyoyaainisha. Je, Waziri atakuwa tayari baada ya Kikao hiki cha Bunge kufuatana na mimi kwenda Kahama kutembelea maeneo niliyoyataja na mengine ili kuthibitisha aliyoyasema katika jibu lake kwa swali langu la msingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba, bado kuna maeneo machache ambayo usikivu siyo mzuri. Ukiacha hayo aliyoyasema, yapo maeneo ya Ulowa, Usetu na Nyamilangano, pia Mawasiliano hayajawa mazuri na tutaendelea kuwabana *Zain* ili waweze kutoa huduma nzuri zaidi katika maeneo hayo. Kama ni mitambo iliyo na matatizo, basi ibadilishwe ili iwekwe mitambo ambayo huduma zake zitakuwa zinaboreka.

Mheshimiwa Spika, pili, nakubaliana naye kwamba, kama nia ni kwenda kuona haya tunayoyazungumza, basi tutaona uwezekano wa kwenda, kama sitaweza mimi, Mheshimiwa Waziri yuko pamoja nami au Watendaji tulionao; lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ujumbe kutoka Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, utakuwa tayari kuwa nae katika maeneo hayo ili kuona hali halisi ya mawasiliano.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la mawasiliano Kahama linafanana na Bukombe; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri au Serikali kwa ujumla wamekuwa wakionesha jitihada kubwa sana za kutusaidia mawasiliano katika Wilaya ya Bukombe hususan katika maeneo ya Rugunga, Nyasato na maeneo mengine ambayo hayana kabisa mitandao lakini makampuni ya mawasiliano hayajaonesha juhudi yoyote ya kuwasaidia wananchi wale ambao mpaka leo hawana mawasiliano yoyote; je, Serikali inasema nini kuhusiana na makampuni haya?

Serikali inaweza ikayaomba Makampuni yafanye kazi na baadaye yakaamua kuacha kuikaidi Serikali; ni nani mwenye uwezo kati ya Kampuni na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Luhahula, Mbunge wa Bukombe, kama ifutavyo:-

Najua kuna maeneo ambayo ameyasema ambayo mawasiliano hayajafika; lakini nina hakika Mheshimiwa Luhahula atakubaliana na mimi kwamba, juhudi kubwa zimefanywa na makampuni yetu ya simu za mikononi kufikisha mawasiliano katika maeneo mengi.

Hayo maeneo aliyoyasema Mheshimiwa ni machache tu na kwa hakika na wao hamu yao ni kufanya biashara kufika maeneo mengi ambako wanaweza ku-*realise profit*. Zaidi tu ni kuendelea kuwakumbusha kama tulivyokuwa tunawakumbusha na tayari suala la Mheshimiwa Luhahula nilishaliandikia nina hakika Mheshimiwa Luhahula atapata jibu muda sio mrefu sana.

Kuhusu nani ni mkubwa baina ya makampuni na Wizara niseme tu Mheshimiwa hapa si suala la ukubwa tulikubaliana sisi wenyewe hapa kwamba, masuala ya kibiashara sasa tuyaache sekta binafsi ifanye shughuli zake. Wizara kazi yetu kubwa ni kuweka sera na kusisitiza sera zile zitekelezwe kwa mujibu wa tulivyozipanga. Tukubaliane basi na Mheshimiwa Luhahula kwamba, wakati sisi tulioko kwenye Wizara tunawabana makampuni basi na ninyi mkiwa mko tayari Mheshimiwa Luhahula, mtusaidie kwa upande mwingine kwa sababu sisi tuki-*push* na ninyi mki-*push* labda mambo yatakwenda kwa wepesi zaidi. Pia tukumbuke kwamba mmoja akiwekewa mawasiliano ambayo hayakuwa kwenye *business plan* na *corporate plan* ya kampuni ni kwamba mwingine anakosa yale mawasiliano. Ndiyo maana wengine wanafikiwa mapema wengine wanachelewa kidogo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa swali la msingi linafanana na swali ninalotaka kuuliza na kwa kuwa Kahama ni jirani na Bukene na sehemu ninazotaka kuzizungumza ziko karibu sana na Kahama katika Jimbo la Bukene, ambazo hazina mawasiliano ya simu na nimeshaziandikia, nimeambiwa watatusaidia lakini bado, naomba kuulizia tu ili wananchi wa Bukene na wenyewe wajue lini watapata mawasiliano ya simu katika sehemu ya Nabala, Kata ya Kahama ya Halanga na Semembela na Mbutu, Kata Mambali.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba kuna maeneo anayoyazungumza hayana mawasiliano na yeye alituandikia na sisi tukawaandikia makampuni husika, kazi iliyobaki kwetu sisi ni kusisitiza upande wake na upande wangu kuwasukuma wenye makampuni waone umuhimu wa kupeleka mawasiliano katika Kata ambazo kwangu ni ngumu kuzikumbuka zote ambazo amezitaja. Lakini akiondoka hapo akumbuke kunipa tena ile barua yake ili niweze kusukuma kwa upande wangu vile vile ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa Clemence Lyamba umehangaika sana, nadhani nikupe nafasi ingawa zimepita dakika mbili sasa. *(Kicheko)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuwa hali ya mtandao wa mawasiliano ya simu iliyotamkwa katika Jimbo la Kahama, Bukombe na Bukene zinafanana kabisa na hali inayohusu Jimbo la Mikumi. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwa msisitizo maalum kushawishi kampuni hasa VODACOM na ZAIN kupeleka mawasiliano katika Kata tatu katika Jimbo la Mikumi zilizosalia zilizo pembezoni na katika miinuko mikubwa za Vidunda, Uleling'ombe na Malolo ili ziweze kunufaika na biashara katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwahakikishie wananchi wa Mikumi kwamba Mheshimiwa Lyamba anafuatilia kwa karibu masuala ya mawasiliano. Ni hivi karibuni tu nikiwa katika shughuli zangu za Jimboni kwangu alinileteа *message* kunikumbushia, nami nikawakumbushia wenzangu wanaohusika katika masuala ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie wananchi wote kwamba Wabunge wenu wanafanya juhudi kupata mawasiliano katika maeneo yenu. Tatizo hapa ni kwamba, inawezekana wenzetu wanapopata mipangilio yao fedha zikawa labda ni ukosefu kidogo kwa sababu wana *roll* sehemu nyingi sana na Tanzania ni kubwa sana hatuwezi kuijenga kwa mawasiliano kwa muda mfupi.

Lakini tukiri sote kwamba hali tuliyonayo sasa na tulivyokuwa ni hatua kubwa tuliyopiga, nikubaliane naye kwamba maeneo ya Vitunda, Ulilingʼombe na Malolo tutaendelea kuyawekea msukumo kwa makampuni ya simu ili waone umuhimu wake, najua jiografia za kule ni ngumu na najua kwamba vijiji viko mbalimbali sana lakini tutaendelea kuwaambia wenzetu wenye makampuni waone umuhimu wa mawasiliano

kwa sababu mawasiliano sasa si anasa isipokuwa ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Na. 29

**Hitaji la Mtandao wa Simu za Mkononi Tarafa za Sepuka na Ihanja**

**MHE. YONO S. KEVELA (K.n.y MHE. MOHAMED H. MISSANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa vijiji vya Maswesa, Ighobwe, Msosa, Lyumbu, Mngungira na Ufana katika Tarafa ya Sepuka pamoja na vijiji vya Iglasoni, Kinyampembee, Nkhoiree na Mpetu katika Tarafa ya Ihanja wamekuwa wakisubiri kupatiwa mtandao wa simu za mkononi bila mafanikio.

Je, ni lini hasa wananchi wa vijiji hivyo watapatiwa mtandao wa simu za mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Misanga, Mbunge wa Singida Kusini kama ifuatavyo:-

Katika kuhakikisha kuwa maeneo mengi yanapata mawasiliano ya simu za viganjani, Kampuni ya Simu ya VODACOM tayari imejenga mnara katika Tarafa ya Sepuka ili kuwezesha mawasiliano kwenye vijiji vingi vya Tarafa hiyo vikiwemo Msanja, Nsonga, Ndaiheya, Elisiya, Mwamiru, Maswesa, Ighobwe, Msosa, Lyumbu, Mngungira na Ufana. Aidha, kampuni hiyo, imeyajumuisha maeneo yaliyoko katika Tarafa ya Ihanja kwenye orodha ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa tathmini ya biashara kwa mwaka huu wa 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake kampuni ya simu ya ZANTEL inaendelea na mchakato wa kupanua mtandao wake. Sanjari na hilo, katika mpango wake wa tathmini ya kibiashara wa mwaka 2010, kampuni hiyo itavihusisha vijiji vya Ighobwe, Msosa, Lyumbu, Mngungira na Ufana vilivyoko katika Tarafa ya Sepuka na vijiji vya Iglasoni, Kinyampembee, Nkhoiree na Mpetu vilivyoko kwenye Tarafa ya Ihanja.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya ZAIN imejenga mnara wa simu katika Kata ya Sepuka ambao mpaka sasa unafanya kazi na unahudumia vijiji vinavyozunguka Kata hiyo. Aidha, Kampuni ya Simu ya ZAIN imefanya tathmini ya kibiashara katika Tarafa ya Ihanja na kubaini kuwepo kwa uwezekano wa kuboresha mawasiliano kwa kujenga mnara.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya TIGO inaendelea na mpango wake wa kupanua huduma za mawasiliano hususan katika maeneo ya vijijini. Sanjari na hilo, TIGO imeahidi kufanya tathimini ya kibiashara maeneo ya Jimbo la Singida Kusini ili kuwezesha mawasiliano.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyonikumbuka mawasiliano kwenye Tarafa za Imalinyi, Wang'ombe na Mdandu lakini pamoja na hizi pongezi namwomba anisaidie kama kuna uwezekano kuongeza minara zaidi kwenye Tarafa hizi za Imalinyi, Wang'ombe na Mdandu hasa VODACOM na TIGO kwa sababu ZAIN imeshafika kwenye maeneo yangu. lakini naomba anisaidie kuniongezea minara mingine ya VODACOM na TIGO kwenye maeneo niliyozungumza.

**SPIKA**: Sasa huu ni ujanja wa kuuliza swali la nyongeza, la mwenzio swali msingi halafu unadandia unaweka yako, sasa basi nitaangalia siku za usoni ujanja huu. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sisi Wizara tunashukuru kuona kwamba maeneo mengi ya Waheshimiwa Wabunge yamefikiwa na maeneo hasa ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tu ilikuwa tunafuatilia kwa karibu sana. Nimhakikishie tu kwamba tutawaandikia tena VODACOM na ZAIN kuwakumbushia kwa sababu na wao tuliwaandikia wakati tunafanya shughuli hizi kwa pamoja ili maeneo aliyoyataja ya Imalinyi, Wang'ombe waweze na wao kufika kwa sababu wananchi wana utashi wao sio lazima wafuate ZAIN au ZANTEL kama wana VODACOM na nyingine waweze kutumia. Kwa hiyo tunamhakikishia kwamba tutawaandikia hawa wenye makampuni waone wanafika maeneo hayo.

**SPIKA:** Ili kumtendea haki Mheshimiwa Misanga, naomba nimruhusu Mheshimiwa Diana Chilolo Viti maalum Singida nadhani yeye atauliza nyongeza inayohusu maeneo haya.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amefanya juhudi kubwa sana angalau kujenga huo mnara mmoja katika Tarafa ya Ihanja lakini mnara huo hautoshelezi maeneo yote haya yaliyotajwa na Mheshimiwa Missanga. Je, atakuwa tayari kujenga mnara na katika Tarafa ya Sepuka ili Kata nyingi ambazo zimeainishwa na Mheshimiwa Missanga ziweze kupata mawasiliano pamoja na kutokujenga mnara katika Tarafa ya Nkonko, Jimbo la Mheshimiwa Chiligati ambako nako wananchi wanamsumbua vivyo hivyo kupata mawasiliano ya simu za mikononi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeelezea vizuri tu kwamba tayari tumejenga mnara na wako wenye nia ya kujenga Sepuka ili vijiji vilivyoko maeneo hayo vifaidike na mawasiliano ya simu. Namhakikishia Mheshimiwa Chilolo kwa niaba ya Mheshimiwa Missanga kwamba tutajitahidi kadri tunavyoweza kuona tunawasukuma

maana yake jamani lazima mjue kwamba sisi Wizara hatujengi minara isipokuwa tunawasukuma wenzetu wa Mawasiliano waone umuhimu wa kufika katika maeneo yenu kutatua matatizo ya mawasiliano kwa kujenga minara au kwa kuwafikishia mawasiliano kwa njia yoyote ile. Kwa hivyo, maeneo aliyoyazungumza ya Nkoko nayo pia tutayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba Jimbo la Mheshimiwa Chiligati ambaye hawezi kujisemea hapa nililitembelea na nilifika mpaka maeneo ambapo wanachimba dhahabu kule Lodoni na hivi sasa nikiri kwamba wananchi wa Lodoni sasa wanafaidika na mawasiliano. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Chiligati kwa juhudi zako hizo ingawaje Mawaziri hawawezi kusema hapa, lakini tuko kuwasemea ninyi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwishapita. Tunayo matangazo machache, wageni, 13 wa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolwa, wageni hao ni Makatibu Kata wa CCM kutoka Wilaya ya Kilolo wakiongozwa na ndugu Zakaria Mwansasu, ningeomba wasimame Waheshimiwa Wabunge wawatambue. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambao ni makada wa CCM kutoka kata ya Mwakilyambiti, Jimbo la Kwimba ambao ni ndugu Jairos Kajala na ndugu John Chenya, naomba wasimame. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali *PAC* anaomba wajumbe wote wa Kamati ya *PAC* mkutane leo saa saba mchana katika ukumbi namba 231, jengo la utawala.

Tangazo kutoka kwa Katibu wetu wa Bunge ni kwamba, katika mpango wa maendeleo wa Bunge wa miaka mitano ofisi imefanya utaratibu ili kuboresha huduma tunazozitoa kwa Wabunge na wafanyakazi. Kwa maana hiyo iliteuliwa kampuni ya wataalam waelekezi na wapo kwenye viwanja vya Bunge na watapitapita kupata maoni na mawazo kutoka kwa wadau wote muhimu zaidi wakiwa ni Wabunge wenyewe kuhusu huduma mbalimbali kantini, usafiri na *Hansard*. Kwa hiyo, tunakuombeni Waheshimiwa mtoe ushirikiano wa kawaida ili waweze kuyaweka kwenye taarifa mambo mahsusi ili tuzidi kuboresha huduma za Bunge letu. Kwa hiyo, wana vitambulisho, watakuwa wanatamani kuongea nanyi lakini lengo ni kuboresha huduma kwa hiyo ni vizuri muweze kuwasikiliza.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo, sasa namwita Katibu kwa shughuli inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa sheria ya Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2010

***[The Persons with Disabilities Bill, 2010]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge jana tulipoahirisha Bunge niliwatamkia kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge wawili bado wataongea kwenye Muswada huu unaohusu walemavu. Wao ni Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Said Amour Arfi. Leo nimepata ombi la Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nimelikubali. Kwa hiyo, kwa mtiririko huo huo tutaanza na Mheshimiwa Lediana atafuata Mheshimiwa Said Arfi halafu Mwanasheria Mkuu. Sasa namwita Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nami nianze kwa kupongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu muhimu. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii muhimu na pia kama wenzangu walivyosema jana naomba sheria hii ikipitishwa basi kanuni zitengenezwe mapema. La sivyo tutaishia kuwa na sheria ambayo haina kanuni.

Mheshimiwa Spika, hii imetuonyesha tulipitisha hapa sheria ya masuala ya UKIMWI mapema sana lakini mpaka leo tunavyozungumza sheria hii haijaanza kufanya kazi kwa sababu hakuna kanuni. Sasa hiyo ndiyo hofu ya wengi nikiwemo na mimi. Kwa hiyo, naomba kanuni zitengenezwe haraka ili sheria ianze kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuweka usawa, kwa kweli watu wenye ulemavu hawajawahi kubaguliwa na Serikali hii, wamepata elimu na napenda nimpongeze Mtanzania mwanamke wa kwanza anayeongoza Chama cha Watu Wasiona Afrika Mashariki yenye makao makuu yake Nairobi. (*Makofi*)

Ni mwanamke wa Kitanzania asiyeona, msomi na wapo wengi wa namna hiyo na napenda Serikali itambue michango mikubwa wanayoitoa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu tunaomba pia shule za watu wenye ulemavu pamoja na walimu waangaliwe, wale walimu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana, tuangalie kuwapa motisha ya namna yake. Wale watoto wa kawaida tu ni kazi kuwafundisha, lakini walimu hawa wamekuwa wanafanya kazi ngumu kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na elimu pia naomba Miswada au Sheria mbalimbali zitafsiriwe kwenye lugha au kwa kutumia alama kwa mfano, wale wasiona waweze pia kusoma, hii ni pamoja na machapisho mbalimbali, ili waweze kufuatilia kila kitu kinachoendelea. Kwa namna hiyo tutahakikisha kwamba elimu imemfikia kila

mmoja wetu, wenzetu walizungumzia vitu mbalimbali lakini inawezekana tunakwenda hata madukani hatuoni saa kwa watu wasiona sasa yawepo na maduka maalum ambayo yanakuwa na vifaa vya watu ambao wana ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na alama napongeza sana ndugu tuliyezungumza jana aliyejiandaa kutoa elimu ya alama ambazo ameziweka kama alama tano, nampongeza kwa kazi nzuri aliyofanya. Lakini alama hizi zikiwa ni pamoja na alama za barabara kama madereva hawatapewa elimu ya kutosha hizi alama hazitaweza kutumika. Katika nchi za wenzetu, mahali ambapo kuna taa za kuongoza magari kuna pia kengele kwa watu wasioona, akisikia ile kengele inagonga anajua sasa inaruhusu watu wapiti, wale wanaoona wanapita na yeye anajua kwamba sasa ni wakati wake wa kupita. Lakini sisi madereva hawajali, angalia Dar es Salaam, taa zinawaka za magari kusimama lakini dereva anaangali huku hakuna gari anapita. Kwa hiyo, ni mpaka pale tutakapokazia sheria madereva watambue kwamba, wanatakiwa wafuate alama za barabarani na sheria zetu zifanye kazi, kama dereva hafuati alama za barabarani achukuliwe hatua, watu wenye ulemavu hawataweza kutumia barabara zetu.  Kwa hiyo, hilo nalo litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo mbalimbali masuala ya majengo tumeshazungumza, bahati mbaya majengo mengi yalijengwa zamani hayakuweka sehemu ambazo watu wasioona wanaweza kutumia ikiwa pamoja na vyoo vyetu. Vyoo vingine ni vidogo, kama kuna mtu mwenye ulemavu anayetumia baiskeli ya miguu mitatu ataingizaje baiskeli yake wakati chumba ni kidogo? Kwa hiyo kuna haja ya kurudi kuboresha majengo yaliyojengwa zamani na ambayo yapo kama yanaweza kufanyiwa ukarabati wa kuweza kuhakikisha kwamba mmoja wetu anapata nafasi. Lakini hii ni pamoja  pia na watoto wetu walioko mashuleni, sina uhakika na vyoo vilivyoko kwenye shule za msingi, kwenye shule za sekondari, kama vimewekwa kuweza kuwezesha watu wenye ulemavu kuweza kutumia sehemu hizi.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira, ninapongeza Muswada kwa kuweza kuona hili na napenda kusisitiza kama tulivyosema kwamba kupata uzoefu sio rahisi, wengi wanatoka vyuoni hawana uzoefu, asilimia tatu ya ajira katika sehemu za kazi kama ni watu 50, basi na wao wazingatiwe ili kuhakikisha kwamba wanapata nafasi.

Mheshimiwa Spika, napenda nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kuonyesha mfano kwa kutenga nafasi za watu wenye ulemavu na hili wote ni mashahidi tumeona mchango wao mkubwa watu wenye ulemavu waliomo Bungeni, wametoa mchango mkubwa sana.  Nakipongeza Chama cha Mapinduzi kuonyesha kwamba ni kinara wa kujali haki za binadamu na iwe ni mfano pia kwa vyama vingine kuweza kuangalia suala la watu wenye ulemavu. Lakini Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuishia hapo kwamba Chama kimetenga nafasi aliongeza kuteua pia katika nafasi zake alizonazo, kuongeza nafasi kwa watu wenye ulemavu, tunatakiwa tumpongeze na huu ni mfano wa kuigwa na nina uhakika watu wenye ulemavu wamepongeza Chama cha Mapinduzi kikiongozwa na Mwenyekiti ambaye ndiyo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sina fadhila, nitakuwa sikuwatendea haki wanawake wa Mkoa wa Iringa kama sitatumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kumtambua mama mwenye ulemavu katika Wilaya ya Makete ambaye ni mlezi wa watoto yatima kwa kutoa mchango wa gari, bajaji pamoja na mchango wa biashara. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Iringa na wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa ujumla kwa kutambua matatizo yanayowapata watu wenye ulemavu na napenda niseme hivi nimekwenda Makete nimemkuta yule mama amejifunza gari anaendesha mwenyewe wala haendeshwi na mtu.

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha kwamba watu wenye ulemavu wakiwezeshwa wanaweza na wote tumewaona na nasema haya kwa sababu nimesoma shule ya sekondari ambayo tulikuwa tunasoma na watu wenye ulemavu na leo namtambua mwalimu wangu Mheshimiwa Gaudensia Kabaka. Kwa hiyo, kusomesha watoto wenye ulemavu na walikuwa wanasoma shule za vipaji na ndiyo hao walioweza hata leo nikizungumza, kuna mwanamke Mtanzania wa kwanza ambaye anashika Afrika Mashariki, amesoma kwenye shule ya vipaji shule ya sekondari ya wasichana Tabora Girls. Kwa hiyo, hayo ni matunda na matunda ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la Muswada huu umesema kwamba *social support*, hawa wenye ulemavu wahudumiwe na ndugu, rafiki ni kweli hilo ni sahihi, lakini Serikali iendelee kuwahudumia kwa sababu wengine wana mzigo mkubwa sana. Tumeshuhudia kwenye *TV* tunamuona mama ana watoto wenye ulemavu watano, wanne yeye pekee, hivi akiachiwa na ndugu wamsaidie wataweza? Kwa hiyo, nashukuru huu utaratibu wa sheria hii utakuwa unaangalia masuala ya watu wenye ulemavu mpaka kwenye ngazi za chini, ngazi za Halmashauri, ngazi za vijiji na watu hawa waweze kutambuliwa na ningeshauri kwamba basi itengwe asilimia fulani kwa watu ambao wana matatizo ya aina hii, mtu labda ana watu wenye ulemavu akizidi mmoja na kama hali ya kiuchumi sio nzuri Serikali ichukue jukumu hili. Tumeona mzigo huu kwa watu wanaotunza watu wenye ulemavu, wengine ni akinamama wameelemewa na mzigo, kwa hiyo Serikali pia iliangalie suala hili kwa makini kabisa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la UKIMWI, watu wenye ulemavu na wenyewe wanakumbwa na tatizo hili na wengine kama tunavyojua hawaoni na wengine kama tulivyosema hawawezi hata kujihudumia. Nashauri kwamba, wapewe elimu ya kutosha ili waweze kujikinga na narudia hiyo hiyo kwamba elimu hiyo pia itolewe kwa wasioona, yaani waipate kupitia maandishi yale wanayoweza kusoma wao ili elimu hiyo iweze kumfikia kila mtu. Tukisema kila mwananchi afikiwe na elimu hii basi na mlemavu imfikie elimu hiyo, tukizungumza habari ya elimu kwanza tuzungumze pia na wao wapate elimu wasome, wajielimishe kwa machapisho ambayo yana lugha ambazo wanazielewa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tunatakiwa tulitilie umuhimu ni vifaa, wengi wamezungumza vifaa vyao ni vya ghali sana zikiwemo fimbo nyeupe na vifaa vingine vya viungo, tungeweza labda tukaviingiza pia kwenye mifuko ya huduma za afya yaani *CIHF* tuweke kwenye matibabu, wanapopewa matibabu yale basi na vyenyewe

viingizwe kwa sababu kama tulivyoona gharama ni kubwa sana, hivi mwanakijiji anaweza kulipia 300,000/=? Wengine tunawaona hawana hata baiskeli. Kwa nini tusiweke utaratibu kwamba, Halmashauri ikaongezewa fedha na ikatenga kiasi fulani kila mwaka kwa ajili ya kununua vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu ambao hawana uwezo wa kuvinunua wao wenyewe na wale wakaweza kupata vifaa hivyo, tunawaona wengi wako vijijini na tunawaona watu mbalimbali wakiwemo Wabunge wananunua zile baiskeli lakini hazijaweza kumfikia kila mtu, nawapongeza sana wale wote wakiwemo Wabunge ambao wameweza kufanya kazi hiyo lakini hazijamfikia kila mtu.

Serikali pia kwenye Halmashauri tutenge fungu, najua kwamba tukiweka hivyo kila kijiji kitatambua watu wenye ulemavu ambao hawana vifaa na ambao hawana uwezo waweze pia kupewa vifaa hivyo. Hapo tutakuwa tumeweza kuwasaidia na kupunguza tatizo kubwa linalowakabili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wanaosoma shule. Kwa watoto wengine elimu imekuwa ni ngumu kuweza kuimudu, wazazi wengine wana watoto wawili au watatu wanaosoma shule labda za sekondari na wengine vyuo vikuu wanaambiwa wachangie ile asilimia, inakuwa ni kazi kubwa kumudu. Naomba hili pia liweze kuangaliwa kama kuna uwezekano ile asilimia wanayoambiwa wachangie wale watoto wakiwemo watoto wenye ulemavu iweze kuondolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nirudie kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuweza kuleta Muswada huu muhimu na tungefurahi Bunge hili likiishapitisha na Sheria hii iwe imetunga Kanuni ili ianze kufanya kazi. Narudia kusema kwamba hii ni pamoja na Sheria ya UKIMWI, tutafurahi sana kama Sheria ya UKIMWI tukimaliza Bunge hili ikiwa na Kanuni pamoja na hii Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga tena mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o, Mbunge wa Viti Maalum Iringa na sasa anafuata Mheshimiwa Said Amour Arfi na wakati huo huo ajiandae mchangiaji wa mwisho ambaye atakuwa ni Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi nami ili niweze kuchangia Muswada huu ambao ni Muswada muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya ndugu zetu walemavu.

Mheshimiwa Spika, nitangulie pia kwa kuunga mkono hoja hii na kwamba imekuja kwa wakati muafaka, lakini ni dhahiri kabisa kwamba Serikali imekuwa ikijali maslahi na maendeleo ya walemavu kwa kipindi kirefu na ndiyo maana katika kifungu cha 63 cha Muswada huu kinafuta Sheria zilizokuwepo huko nyuma za mwaka 1982 na Sheria namba 2 na 3 iliyokuwa inahusu mafunzo na ajira.

Ni jambo jema kwa Muswada huu ambao umeletwa mbele yetu na hatimaye naamini kwamba Bunge hili litaupitisha na kuwa Sheria imebeba pia maudhui yaliyokuwepo katika Sheria zilizofutwa na Muswada huu. Lakini nilikuwa napenda kutahadharisha kwamba Sheria yoyote haiwezi kuwa Sheria nzuri kama haiwezi kusimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hofu niliyonayo ni juu ya usimamizi wa Sheria ambazo tumezitunga kwamba, je, zinaleta tija na makusudio ambayo yalikuwa yamedhamiriwa kwa kuanzishwa kwa Sheria hiyo? Kwa maana kwamba kumekuwepo na Sheria toka mwaka 1982, lakini sina uhakika ni kwa kiasi gani Sheria hizo ziliweza kuwanufaisha walemavu. Lakini naamini kwamba tutajisahihisha katika upungufu wowote uliokuwepo huko nyuma ili maudhui yaliyomo katika Muswada huu yaweze kuwanufaisha ndugu zetu walemavu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niungane na maneno mazuri sana ambayo Waheshimiwa Zulekha Yunus na Margreth Mkanga jana walisema kuhusu muundo wa Baraza la Walemavu.

Mheshimiwa Zulekha Yunus alitoa methali kwa lugha ya Kiingereza akasema: “Nothing *about us without us*“ na Mheshimiwa Mkanga pia aliweka mkazo kwa kusema “Huwezi kujua maumivu ya kiatu usichokivaa.”

Mheshimiwa Spika, makusudio ya Waheshimiwa hawa ni kuonyesha ni namna gani kwamba muundo wa *council* hii haujakidhi matakwa ya kuwakilisha kundi hili la walemavu pamoja na kwamba hawana mashaka na hawa watakaoingia kwamba watazungumzia masuala yanayowagusa walemavu, lakini kama wangeshiriki wenyewe na likawa la kwao basi lingeweza kuleta tija zaidi. Niungane nao kwamba iko haja ya kuangalia muundo wa hili baraza na hata utakaporejea katika majedwali ambayo yanaunda mabaraza katika ngazi ya Mtaa, Kijiji, Wilaya na Mkoa yanapishana. Uwakilishi ni mkubwa katika ngazi za vijiji, mtaa na Mkoa katika majedwali namba 3, 4 na 5 ambayo yanahusu Mkoa, kijiji na mtaa, yana Wajumbe watatu watatu.

Mheshimiwa Spika, unapokuja kwenye jedwali namba 2 ambalo linahusu Wilaya, lina Wajumbe wawili, unapokuja kwenye Taifa ni mjumbe mmoja kutoka kwenye *apex*. Hapo utaona uwakilishi unakuwa mkubwa zaidi katika ngazi za chini na unakwenda unapungua na sijui ni kwa sababu gani kama Mkoa wanaingia Wajumbe watatu lakini Wilaya wanakuwa Wajumbe wawili, sijui ni upungufu tu wa kawaida ya kiuandishi au ndiyo dhamira ilivyo ya kupunguza Wajumbe katika ngazi ya Wilaya. Nafikiri ipo haja ya kulitafakari hili na kuangalia ni namna gani walemavu wenyewe wanashiriki katika hili na kulifanya ni la kwao.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii nikifahamu fika kabisa kwamba Mamlaka ya uteuzi wa Mwenyekiti wa Baraza hili yako juu ya Mheshimiwa Rais. Nitangulize kwa kumwomba Mheshimiwa Rais kupitia Bunge hili kwamba wakati atakapofanya uteuzi basi Mwenyekiti wa Baraza hili atokane na wao wenyewe walemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilikuwa naomba lijaribu kuangaliwa ni lile ambalo linatoa kifungu cha 8 na 9 yaani sehemu ya 3 ya muundo na majukumu ya *Council*, inanipa hofu sana pale ambapo Sekretarieti itakuwa inapokea maelekezo kutoka kwa Waziri na kutoka kwa *Council*. Hapa linanipa hofu sana kwamba inawezekana kukawa na ufanisi mdogo katika mtiririko huo wa kumpa Mamlaka Waziri kufanya kazi moja kwa moja na Sekretarieti.

Nadhani ingekuwa ni busara Waziri akashauriana na akatoa maelekezo kwenye *council* na *council* ndiyo ikaisimamia *secretariat* badala ya Waziri kuisimamia *secretariat* moja kwa moja au kutoa maelekezo kwenye *secretariat*.

Mheshimiwa Spika, pia katika sehemu ya 7, kifungu cha 26 (1), (2) na (3) vimezungumzia haki ya walemavu ya kupata matibabu. Hili kidogo linanipa hofu kwa sababu walemavu kwa mujibu wa Muswada huu wa Sheria wasibaguliwe na wana haki ya kupata huduma hizo za afya kama walivyo Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama tunaweza kuwatendea haki walemavu hawa ni kwa kuweka huduma hizi kuwa ni za lazima kwao kama Sheria inavyotamka, lakini ziwe zinatolewa bure. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewasaidia. Mfano mzuri jana Mheshimiwa Mkanga alikuwa anazungumzia juu ya vifaa vinavyowasaidia wenye matatizo ya ulemavu wa viungo kwamba vinagharimu pesa nyingi na idadi kubwa ya Watanzania na waathirika wako vijijini na uwezo wao ni mdogo. Kwa hiyo, Serikali ibebe jukumu hili la kuwasaidia hawa walemavu kwa kadri mahitaji yao yatakavyokuwa yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, pia nigusie ukurasa wa 53 wa Muswada ambao unazungumzia madhumuni na sababu ya kuletwa kwa Muswada huu. Inasikitisha kwamba katika ukurasa wa 53 (10) kwa mujibu wa Muswada imeandikwa kwamba inahusu vipindi vya *television*, huduma za simu, Posta na Forodha kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Sehemu hii inazitaka *television* kuwa na mfumo wa lugha na tafsiri ya vipindi vya *television*. Aidha, watoa huduma wa simu pia wanatakiwa kuwa na muundo wa vifaa rahisi kwa ajili ya walemavu. Sehemu hii vile vile inapendekeza kufutiwa kodi na gharama za kusafirisha vifurushi.

Lakini ukija kwenye Muswada wenyewe sehemu ya 10 haizungumzii maudhui hayo lakini maudhui yanayozungumziwa hapo yako katika sehemu ya 9 na dosari hii bahati nzuri Kamati iliyopitia Muswada huu imeeleza hapa kwamba ni vizuri wakawa wanahakiki ili kuturahisishia kuweza kufuatilia. Lakini unapokuja katika kifungu hicho cha 9 hukuti kipengele chochote kinachogusia misamaha ya kodi. Kwa hiyo, napenda nipate maelezo kwamba hii misamaha ya kodi watakayopewa walemavu inahusu vifaa gani? Mathalani je, mlemavu anapohitaji chombo cha usafiri kama bajaji je, atapewa msamaha wa kodi na Serikali ili bajaji iwe rahisi na walemavu wengi waweze kumiliki vyombo vya usafiri? Kwa hiyo, vyombo ambavyo vinakusudiwa kuwasaidia walemavu ama viainishwe katika Kanuni na katika utaratibu wowote ule ili viweze kufahamika na

visiweze kutuletea matatizo kwa sababu kazi mojawapo ya *council* ni pamoja na kusaidia kurahisisha kupata hiyo misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa yanahusu Muswada huu. Lakini kuna baadhi ya ulemavu unasababishwa tu na kukosa huduma katika wakati muafaka, vimekuwepo vituo vya kulelea na kuwatunza walemavu mfano mzuri ni kituo cha Mlali hapa Kongwa. Nilibahatika kwenda kutembelea kituo hicho, nilimpeleka Mlemavu mmoja kutoka Jimboni kwangu na nikavutiwa sana na kazi nzuri wanayofanya katika kituo kile. Ni kituo ambacho wanastahili kupongezwa, ni kituo ambacho kina vifaa vinavyotosheleza, ni kituo kizuri ambacho kinawahudumia Watanzania wengi kutoka Mikoa mbalimbali. Lakini kinachosikitisha ni kwamba katika kituo hicho hakuna hata mchango wa senti tano kutoka kwenye Serikali yetu, iliniumiza sana baada ya kufika katika kituo hicho na kuangalia vifaa walivyonavyo, huduma wanazozitoa kwa gharama nafuu kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini hata msaada wa kupewa daktari bingwa tu kwa ajili ya kuwahudumia wale watoto bado tunaona uzito kuwasaidia. Pale inapotokea Taasisi za dini zikajitolea kufanya shughuli nzito na ngumu kama ile wanayofanya Kanisa Katoliki pale Mlali inapaswa Serikali isaidie, kama tunaweza kusaidia na kutoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji wanaokuja kuchimba Madini na kadhalika na vivutio vingi kwa nini tunashindwa kusaidia vituo hivi? Mathalan pale wanahitaji Daktari Bingwa kwa ajili ya kuwahudumia wale watoto lakini matokeo yake *operation* zinaahirishwa mpaka Wataliano watakapopata likizo kule Italy ndiyo wanakuja kufanya *operation*. Mgonjwa niliyekuwa nimempeleka pale niliambiwa kwamba haitawezekana kusaidiwa mpaka mwezi wa nne watakapokuwa wamechukua likizo Madaktari bingwa wa kule Italy ndiyo watakuja kufanya kazi za kujitolea. Nadhani ipo haja sasa kwa Serikali kuangalia namna gani inasaidia hivi vituo.

Aidha, kituo kama hiki kilikuwepo kule Mpanda katika makazi ya Wakimbizi ya Katumba, nataka nipate maelezo ni kwa nini Serikali ilishindwa kusaidia kile kituo kuendelea kuwepo. Naiomba Serikali kutenga fedha katika bajeti zake kwa ajili ya kuwasaidia hawa wenye ulemavu katika hatua za awali kupata tiba ambazo zinaweza kuwasaidia baadaye wasiwe wategemezi wa vifaa vingine hasa wale wanaozaliwa na hitilafu katika miguu na kadhalika ambao wanaweza kuhudumiwa hospitalini na hatimaye wasiweze kutumia magongo na ikawa ni mzigo kwao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kituo kile ipo haja na tuwaombe pia watu wa habari hasa vituo vya *television* waende wakatembelee kile kituo badala ya kutuonyesha shule za *international* wanavyokula keki na kadhalika, wakaangalie madhila na malezi wanayopata wale watoto pale Mlali.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina maelezo ya kueleza hisia zangu ni namna gani watu wale wanavyofanya kazi katika mazingira magumu sana, watoto wenye ulemavu wana *multiple complications,* anaweza kuwa ni taahira yaani ni vigumu sana, lakini inapendeza tu kwamba kituo kile kikapata matangazo ya kutosha na msaada wa

Serikali. Wana vifaa vingi lakini wana upungufu mkubwa wa Wataalam, hilo la Wataalam naamini kabisa Serikali yetu ni sikivu itasikia kilio hicho na kusaidia na kuangalia sasa kwamba vituo kama hicho cha Mlali kinajengwa katika kila Mkoa ili kurahisisha kutoa huduma kwa watoto ambao watazaliwa na upungufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Amour Arfi kwa mchango wako.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Afya na Naibu wake. Pia nawapongeza wale wote ambao wamekuwa chachu ya kuwezesha Muswada huu uweze kufika hapa leo hii.

Je, ni kipengele kipi kinatoa Sheria ya Adhabu kwa wale ambao wanawaficha walemavu kwani kuwafungia ndani ya nyumba wasionekane huo pia ni ubaguzi? Ahsante.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja zifuatazo na zizingatiwe katika kuuboresha Muswada huu kama ifuatavyo:-

Je, Muswada huu utazingatia na kuwasaidia walemavu wanaopewa mimba na wanaume baadaye kutokuwatunza na kuwatelekeza kipindi chote wakiwa na mimba; hali kadhalika, baada ya kujifungua na kupata mtoto, hawawajali watoto waliozaliwa hata kama anathibitisha kuwa aliyezaliwa ni mtoto wake? Matokeo yake, baada ya uzazi, mama anakuwa na hali ngumu ya maisha kuhusu kuwezesha hali yake ili awe na afya. Licha ya yeye kuwa na hali duni ya maisha, mtoto aliyezaliwa ndiyo anapata tabu zaidi ya kukosa lishe, matunzo ya kawaida, nguo, malazi na namna ya ulezi. Nitashukuru kama sheria hii itazingatia hali hii na walemavu wazazi waweze kufikiriwa na huyo aliyempa mimba, kihiari au kilazima kwa kutumia sheria.

Jambo la pili, suala la ajira ya walemavu serikalini au kwenye mashirika au kampuni binafsi ni gumu sana hasa kwa walemavu wanawake. Serikali iweke mkazo na msisitizo wa kuwapa ajira kwani wapo wengi waliopata elimu nzuri na ujuzi wa kazi mbalimbali. Nitashukuru suala la ajira likiwekewa kipaumbele kwa hawa walemavu ili waendelee kujitegemea zaidi badala ya kungoja msaada kwa wanandugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Ulemavu ni jambo analopata mtu kwa kuzaliwa ama kuumia baadae. Pendekezo langu ni kuomba, jamii ama serikali kubadili fikra kwa kuzingatia watu wanaoishi na ulemavu wapewe mahitaji ya lazima, mfano, elimu, matibabu, nguo na maji bila ya kusumbuliwa.

Makambi yaliyopo hayatoshi kumudu kuwapa hifadhi watu wenye ulemavu kwa kutosheleza na hata katika makambi hayo bado kuna upungufu mkubwa wa kutosheleza mahitaji yao ya lazima. Idadi ya vituo iongezwe angalau kila Tarafa au Wilaya ipate kituo.

Zipo shule za watu wenye ulemavu mfano Shule ya Viziwi Tabora, Shule ya Wasioona Tabora, Shule ya Uhuru na Bwigiri, naomba zitiliwe mkazo hasa katika maeneo mengine ili kutosheleza upatikanaji wa elimu ambayo ni ukombozi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kuishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kuwafikiria wenzetu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengi ambayo Sheria hii imeyazingatia, bado ningeomba serikali ifikirie kutenga eneo maalum la kuwatunza watu wenye ulemavu ili kuwaweka katika mazingira mazuri, kwani walemavu wengi wanakuwa na ujuzi wa kuweza kufanya kazi mbalimbali lakini huko nyuma walionekana ni watu tofauti na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitolea mfano wa wenzetu wa Mombasa Kenya, wametenga eneo maalum kwa ajili ya walemavu, wamejenga nyumba za kuishi kwa ajili yao na wamefungua miradi kwa ajili yao, hivyo wanafanya kazi mbalimbali za ufundi na wanapata mishahara mizuri na wana uwezo wa kujikimu kimaisha. Inapendeza kwamba, humwoni mlemavu hata mmoja kuzurura barabarani na kuombaomba, wanafanya kazi wenyewe na wanaishi bila matatizo. Kwa nini na sisi hatuwakusanyi tukawatafutia miradi ili waweze kujitegemea?

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii hii inaweza kufanya kazi kubwa za uzalishaji na wanaweza hata kusafirisha nje bidhaa zao na serikali ikapata tija ndani yake, hivyo tuwatengenezee mazingira ya kujitegemea.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji, Wadau na Kamati, kwa kuandaa, kuupitia na kuuwasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo na maoni yangu katika Muswada huu yapo kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inieleze ni kwa nini walimu wanaofundisha watu wenye ulemavu stahiki zao ni ndogo?

Niliwahi kuitembelea Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko Dar es Salaam, wana kazi kubwa tena ngumu, cha ajabu mishahara yao haina tofauti na walimu wengine. Nashauri Serikali iwaongezee maslahi walimu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha (v) cha Muswada unaposema *Medical Care* maana yake nini? Lazima suala la huduma za afya kwa walemavu lifafanuliwe vizuri kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zipewe ulazima wa kutenga bajeti kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. Miradi mingi kwenye Halmashauri wananyanyasika sana kupata huduma za miradi au mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke ulazima wa kuwa na ajira kila Halmashauri wenye sifa. Tunaona wenye ulemavu kupata ajira ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Taasisi zinazojishughulisha na masuala ya walemavu ziangaliwe kwenye Kanuni kwani Taasisi hizi ni msaada mkubwa mno kwa walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu wake kwa kuleta Muswada muhimu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu wengi huwa hawana uwezo wa kufanya kazi na kupata mahitaji yao ya lazima ya kila siku; hivyo, tunaomba Serikali yetu iwatambue walemavu na kuwapatia mahitaji yao ya lazima bure. Tunaomba walemavu wapatiwe elimu bure toka shule za awali hadi vyuo vikuu. Vilevile wapatiwe Bima ya Afya bure na itakuwa vizuri endapo watapewa fedha *(Social Security)* kila mwezi kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanawanyanyasa walemavu, watu hawa wachukuliwe hatua za kisheria bila huruma.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuzipongeza juhudi za Serikali za kuboresha maisha ya walemavu kwa kuuleta Muswada huu kama mwendelezo wa sheria nyingine zilizopo za matunzo na ajira zote za mwaka 1982.

Nilikuwa nadhani kwamba, ipo haja ya lazima kuangalia sheria zilizopo zimewafurahisha kwa kiasi gani walemavu kwa maana wanapata matunzo stahiki, mathalani walemavu wa magonjwa ya akili wameachwa wanatembea ovyo barabarani

bila matunzo, aidha, walemavu wangapi wamepata ajira katika soko la ushindani. Hivyo basi ni vyema sasa tukatengeneza utaratibu muafaka wa kusimamia hizi sheria ili manufaa yake yaonekane kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaangalia mchango wa serikali katika Vituo vya Walemavu, mfano, Kituo cha Mlale hapa Kongwa kinaendeshwa kwa msaada wa Wataliano na wanafanya kazi nzuri sana, lakini tumewasaidia kwa kiwango gani? Ninapenda kuiomba serikali ione namna itakavyoweza kuwasaidia kwa kuwapatia daktari bingwa wa matatizo ya watoto wenye ulemavu; ninaamini serikali inaweza kusaidia hilo. Naomba sana kituo hiki kitembelewe na kuangalia namna serikali itakavyoweza kusaidia hata ikiwezekana kusaidia namna ya kukiendesha na kuwa vituo kama hicho ambacho nimebahatika kukitembelea vijengwe angalau viwili kwa kila mkoa, hatua ya kuwasaidia walemavu iwe ni kipaumbele chetu.

Mwisho kabisa, naomba pia walemavu wapewe msamaha wa matibabu kama ilvyo kwa wazee na watoto. Nashukuru sana.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Wizara kwa kuuleta Muswada huu haraka.

Tabora kuna shule ya watu wenye ulemavu (viziwi na wasioona), ambayo ilikuwa chini ya Madhehebu ya Pentekoste, ambayo serikali imesahau kuisaidia kwa muda mrefu; hivyo basi, naomba Wizara ya Afya isaidie kufuatilia Wizara ya Elimu kuona jinsi ya kuwasaidia walemavu hao kwa kutoa huduma muhimu kama vile vifaa vya kufundishia, chakula na matibabu, ambavyo vitakavyowasaidia kupata elimu bora kama wanafunzi wengine. Pia ningeshauri serikali itoe motisha kwa walimu wanaofundisha watoto wenye ulemavu kwani mazingira yao ni magumu.

Naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kukikarabati Chuo cha Wasioona cha Lwanzari Tabora ili kiweze kutumika kutoa mafunzo mbalimbali. Naiomba Wizara itenge fedha za kumalizia mwaka huu ili kiwe Chuo cha Kitaifa kwa Walemavu Wasioona na ikiwezekana hata walemavu wengine kwa kupatiwa mafunzo ya kisasa.

Kambi ya Ipuli ina mazingira magumu sana kwani humo kuna walemavu wasioona na wasiokuwa na miguu. Kufanyike marekebisho ya vyoo na ngazi kwenye maeneo muhimu hapa nchini.

Naomba Wizara isaidie kuihamasisha Wizara ya Fedha kuhakikisha Wizara ya Viwanda na Biashara na *NGOs* mbalimbali zinatoa mikopo hasa SIDO, kwani walemavu hao wanajitahidi sana kufanya biashara.

TAMISEMI ishauriwe kuwa karibu na vitengo hivi isiachiwe Wizara pekee kwa kutoa misaada na elimu kwa jamii hasa kusimamia ujenzi wa majengo ya shule, zahanati na vituo ya afya, kwa kuzingatia hali ya walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watumishi wote wa Wizara.

Muswada huu umekuja kwa wakati ama umechelewa kidogo.

Serikali iongeze bajeti ya fedha kwa Wizara hii ili Wizara iweze kutoa huduma za kijamii kama mahitaji ya elimu, afya na huduma ya mafunzo, yaani sehemu ya kuishi, chakula na mengineyo.

Katika Muswada sehemu ya III, kifungu cha 9, naomba shughuli za Baraza la Ushauri la Taifa ziongezwe, yaani Baraza lifanye sensa ya walemavu nchi mzima katika vipindi maalum iwe kila baada ya miaka mitano au miaka kumi ili kujua idadi yao kwa uhakika.

Inafurahisha sana kuona Sheria inalazimisha kuwa kila mwajiri mwenye watumishi zaidi ya 50, asilimia mbili ya watumishi hao wawe watu wenye ulemavu. Naomba serikali ilihakiki jambo hili.

Serikali (Sheria) ipange mipango maalum ya kuwafundisha ujasiriamali, wapewe elimu na nyenzo za kujiendeleza katika kuendesha maisha yao. Mafunzo ya ujasiriamali yaambatane na mikopo yenye masharti nafuu kwa watu wenye ulemavu.

Serikali iongeze kipengele cha kulazimisha kuwa pindi ikitokea mtu mwenye ulemavu na mtu mzima wakatokea kuomba nyumba ya kuishi, mtu mwenye ulemavu apewe kipaumbele na apewe hiyo nyumba. Aidha, kama nyumba hiyo ni ya ghorofa, basi mtu mwenye ulemavu apewe nyumba ya chini, yaani *ground floor* ya nyumba hiyo.

Kwa vile kila mmoja wetu ni mlemavu mtarajiwa, kwa mfano, *Road Traffic Accidents, Falls or Stroke* na kadhalika, naomba serikali ibuni kodi maalum kwa kila mmoja wetu alipe 0.5 - 1% ya kipato chake kipelekwe katika *The Tanzania Disability Fund.* Fedha hizi zinaweza kusaidia kuweka hali sawa katika maendeleo ya watu wenye ulemavu.

Mwisho, naishukuru sana Wizara kwa kuuleta Muswada huu Bungeni. Ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, walemavu wanahitaji vifaa mbalimbali ili viwapunguzie shida wanazozipata, kwa mfano, *wheel chair*, miguu ya bandia na kadhalika. Ninaomba vifaa hivyo vipatikane maeneo yote nchini na vipatikane kwa bei nafuu na ikiwezekana kuwepo na taasisi kubwa ya kiserikali katika kuhakikisha uwepo wa vifaa hivyo na ikiwezekana hapo baadae vifaa hivyo vigawiwe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada huu Halmashauri za Wilaya zimepewa majukumu fulani kwa walemavu, lakini uzoefu wa kiutendaji umeonesha mara

nyingi taasisi hizi huwa zinajitahidi kutekeleza majukumu yao na si majukumu yanayotoka TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwapa majukumu Halmashauri kutokana na Sheria ya Wizara ya Afya ni kuweka mazingira ya kutotekelezwa majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo ninachotengeneza au Baraza linalotengeneza Programu za Walemavu ni vyema wakawa na uwakilishi mkubwa wa walemavu wenyewe kinyume na kifungu cha 19 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwajali wenzetu wenye ulemavu na kwa kuonesha nia thabiti ya serikali katika kuwajali wenzetu, katika bajeti ya 2010/2011 inaonekana wazi kuwa serikali itasaidia upatikanaji wa huduma za walemavu wa aina zote.

**MHE. MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kuwa hai na wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, walemavu ni viumbe alivyoviumba Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na wala hakuna mtu yeyote anayependa kuwa mlemavu bali haya ni matakwa ya Mwenyezi Mungu ambayo hayaepukiki. Hali kadhalika, kila mtu ajihesabu kwamba ni mlemavu mtarajiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu ndiye anayeepusha yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo walemavu wa aina mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. Walemavu hawa wanapata shida sana, wengi wao hawawezi kujihudumia wenyewe. Kwa hiyo, ingekuwa vyema Serikali iwasaidie kwa kuwawezesha ili waweze kujihudumia kwa kupata mahitaji yao. Wengine hawajiwezi kabisa, hawa wasiojiweza kabisa serikali iwachukue na iwaweke pahala pamoja na iwahudumie kwa kila hali ili na wao waweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao walemavu wengi katika mikoa yetu yote na wengi wao sasa hivi wanakuwa waombaji wakubwa; hii ni kwa sababu ya kukosa kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba walemavu wawezeshwe na wahudumiwe vya kutosha. Ahsante sana.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu ni viumbe/binadamu wenye haki kama binadamu wengine, hivyo kuwapatia haki za kimsingi ni wajibu na serikali yenye kujali watu wake na ni lazima itoe uangalizi maalumu kwa kundi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingefaa serikali ifanye yafuatayo katika kuwajengea mazingira ya kuwapa haki na kuwatunza walemavu:-

Kwanza, iwajengee vijiji maalumu vitakavyowekewa huduma mbalimbali na shughuli za kimiradi za kuwaendeleza. Ziwepo shule, viwepo viwanda na shughuli nyingine mbalimbali za kuwaendeleza.

Pili, waajiriwe watu wenye fani mbalimbali wa kuwahudumia na kuwaendeleza walemavu hatimaye waweze kufanya shughuli za kujitegemea kwa wanaojiweza.

Tatu, yaandaliwe mazingira katika taasisi za kiserikali ya kuwawezesha walemavu kupata nafasi za kufanya kazi.

Serikali ibainishe aina za adhabu kwa wale wanaowanyima haki walemavu katika mazingira ya kuwadhalilisha.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Naibu wake na Katibu Mkuu, kwa kuuleta Muswada huu kwa wakati muafaka.

Katika jamii yoyote, suala la kuwajali walemavu wa aina yoyote ni la lazima kwa sababu hao ni binadamu wenzetu na hawakupenda wawe hivyo. Kama nchi, jukumu la kuwahudumia makundi haya ya walemavu ni la Wizara husika hasa Kitengo cha Ustawi wa Jamii.

Ukiangalia katika nchi yetu kadiri miaka inavyokwenda tangu tupate uhuru, huduma kwa jamii hii ya walemavu inazidi kuzorota ingawa idadi ya walemavu inaongezeka. Nitatoa mifano michache:-

Makambi mengi ya walemavu yalijengwa miaka ya sitini, hali ya miundombinu ya makambi hayo leo inasikitisha; nyumba hazijafanyiwa ukarabati wala upanuzi ili kuruhusu walemavu wageni waweze kupata maeneo ya kuishi. Wahudumu wa kuhudumia walemavu hao kwenye makambi mengi hawapo baada ya wale waliokuwepo kustaafu *(Social Workers).*

Naomba baada ya Sheria hii, Serikali iweke mipango thabiti ya ukarabati na upanuzi wa makambi hayo ya walemavu.

Katika Wilaya yangu ya Kilombero kuna kituo cha kutoa elimu maalum kwa watoto wenye ulemavu katika Kata ya Lumemo. Serikali ilitumia fedha nyingi kuwapeleka walimu wa vituo hivi kwenye masomo Nchini Malawi kujifunza jinsi ya kuwahudumia watoto wa aina hiyo. Walimu hao waliporudi walinunuliwa vitendea kazi kama pikipiki na vifaa vyote vya kufundishia na kuanza kufanya kazi hiyo. Leo hii walimu hao wanashindwa kutoa huduma hii *effectively* kwa sababu vitendea kazi vilivyonunuliwa miaka ya themanini havifanyi kazi. Pikipiki zimeharibika na vifaa vya kufundishia vimekwisha.

Kama kituo hiki kilianzishwa kama mradi, ilikuwa ni jukumu la serikali kuendeleza vituo hivi kutokana na umuhimu wake, baada ya kipindi cha mradi kwisha kituo hiki ni kama kile kilichopo Chalinze ambacho kwa kauli ya Waziri hapa Bungeni kimeweza kuimarishwa.

Naomba kwa mchango wangu huu, Wizara ikumbuke kutusaidia Kituo cha Kutoa Elimu kwa Watoto Walemavu cha Lumemo katika Wilaya yangu ya Kilombero.

Walemavu wengi wa viungo wana mahitaji ya baskeli za miguu mitatu. Tunaomba baada ya Sheria hii, serikali itoe punguzo maalum la kodi kwa ajili ya kuingiza baiskeli zilizo na ubora zaidi kutoka nchi za nje.

Kama utafanyika mpango maalum bila shaka bei ya baiskeli hizi itakuwa nafuu kama vile zana za kilimo zinavyoingizwa bila ushuru. Kwa vile madhumuni ya baiskeli hizi ni kutoa huduma, serikali iwahamasishe wenye uwezo wa fedha waagize baiskel hizi kwa wingi bila ushuru.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri wanazofanya ikiwa ni pamoja na kuwaleta wataalamu wa magonjwa ya moyo kutoka India na kwa kuuandaa na kuuwasilisha Bungeni Muswada wa Watu Wenye Ulemavu.

Ninawapongeza pia Wabunge wa Viti Maalumu wanaowakilisha watu wenye ulemavu kwa kuwa wawakilishi wazuri, kwani mara kadhaa wamekuwa wakisisitiza katika michango yao Bungeni kwamba, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu itungwe haraka.

Kimsingi, Sheria hii ni ya muhimu sana kwani ikitekelezwa ipasavyo itawawezesha watu wenye ulemavu kujitegemea, lakini pia itaiwezesha jamii kutambua kwamba, wenye ulemavu hawakuwa hivyo kwa matakwa yao na wale wasio na ulemavu pia si kwa matakwa yao. Hivyo ni vyema jamii ikaelimishwa hivyo wakati wa utekelezaji wa Sheria hii.

Vilevile jamii ieleweshwe kwamba, kila mwanadamu ana nafasi sawa ya kuwa mlemavu wakati wa kuzaliwa au kutokana na ugonjwa au ajali na kwamba kutokuwa na ulemavu ni bahati. Hivyo, jamii inao wajibu wa kuwapenda na kuwathamini walemavu.

Nianze kutoa ushauri wangu kuhusiana na sehemu ya pili ambayo inagusia kuihamasisha jamii kushiriki katika kulinda haki za watu wenye ulemavu mpaka sasa wako wanajamii wengi walio mstari wa mbele katika suala hili. Ninalo pendekezo kwamba, serikali iwatambue wanajamii hawa ikiwezekana wapewe tuzo kama njia mojawapo ya kuongeza hamasa ili wanajamii wengi waweze kujitokeza zaidi katika kulinda haki za wenye ulemavu.

Katika sehemu ya nne, Sheria inatoa wajibu kwa Serikali za Mitaa. Hapa ushauri wangu ni kwamba, Sheria itoe wajibu hata kwa taasisi mbalimbali na Wizara zake, pamoja na Mashirika. Ni vyema bajeti zikatenga fungu la walemavu kama ilivyo kwa UKIMWI. Wizara ya Viwanda na Biashara itenge fungu kwa ajili ya kuwapa wenye ulemavu mafunzo ya ujuzi mbalimbali kupitia SIDO na baadaye kuwapatia mikopo. Wizara ya Afya na Elimu zitenge mafungu kwa ajili ya tiba na nyenzo. Wizara ya Maji itenge fungu kwa ajili ya kuwasaidia kuvuna angalau maji ya mvua. TANESCO iwe na fungu la kusaidia kuweka umeme katika majengo ya walemavu wanayoyajenga kwa ajili ya miradi ya kuwapatia kipato. Wizara ya Kilimo pia kupita ASDP inaweza kufanya

mambo makubwa kwa watu wenye ulemavu. Wizara za Mifugo, Maendeleo ya Jamii na Wizara ya Kazi nazo zijipange vizuri ili kuweza kuwanusuru watu wenye ulemavu ambao huzunguka kutwa nzima barabarani wakiungua na jua wakiwa wanasubiri misaada ya wapita njia.

Sehemu ya tano inatoa wajibu kwa Serikali za Mitaa namna ya kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu, ninashauri elimu nayo itolewe na si wajibu peke yake.

Katika sehemu ya saba Sheria inapowataka waajiri kutowaachisha kazi wenye ulemavu wakati wa zoezi la kupunguza wafanyakazi, ikumbukwe kwamba wapo ambao walipata ulemavu wakiwa wanafanya kazi viwandani na matokeo yake wakapunguzwa kazi. Napendekeza kwamba, katika kanuni hawa walioathirika kwa jinsi hii warudishwe kazini. Hata hivyo, Sheria hii itoe wajibu kwa mwajiri ambaye mwajiriwa atapata ulemavu kazini au kwa sababu ya asili ya kazi yake.

Mwisho, napenda kuishauri Serikali iangalie vikundi vya watu wenye ulemavu wanapoanzisha biashara kwa ajili ya kuwawezesha kujitegemea wasamehewe kodi na wanaponunua vifaa kwa ajili ya mradi pia wasamehewe kodi ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni yangu pamoja na kupata majibu mazuri nijue Muswada huu utawasaidia vipi kuwapatia elimu ya ujasiriamali walemavu wengi walioko vijijini na kuwapunguzia kunyanyasika.

Pili, walemavu wa ngozi (albino), wanapata shida sana; je, Muswada huu utawasaidiaje? Hivi juzi kuna mlemavu amekatwa mkono kikatili, tulitegemea jeshi ndilo liwe mstari wa mbele, lakini nimesikia kwenye vyombo vya habari Mkuu wa Kituo anatamka wale waliomkata mkono mlemavu siyo washirikina bali kuna mgogoro kati ya wafugaji na wakulima. Je, walemavu waliosikia anatamka hivyo wamejisikia vipi? Kwa nini waondoke na mkono huo? Je, kwenye mgogoro huo kuna mlemavu huyo peke yake? Naomba nipewe majibu. Muswada huu unawasaidia vipi au ni vipengele vipi vinawajali walemavu hao?

Wizara ijitahidi kuwapeleka walemavu wengi mashuleni kwani hata Mkoa wa Kagera una shule mbili za viziwi; wengi wao ni yatima ambao hawana msaada wowote na wana uwezo mkubwa, naomba hizo shule zipewe kipaumbele.

Je, Muswada umeangalia jinsi ya kuwapatia matibabu walemavu?

Shule ya Ngeza ina walemavu wa aina zote, wasaidiwe vifaa mbalimbali vitakavyowawezesha kupata elimu bora kama wanavyopata watu wengine.

Ninaiomba serikali iwafikishie walengwa yanayosemwa ndani ya Muswada huu. Vilevile vipengele vinavyosema kwamba, walemavu wanatakiwa wajisajili viboreshwe

kwa sababu kwa walioko vijijini itakuwa ni vigumu kujisajili kwa sababu wana uelewa mdogo sana.

Muswada unasema pawepo na usimamizi mzuri, kama tunavyoona Waathirika wa UKIMWI wanavyonyanyasika, wanawafurahisha watu baki; unakuta pesa za kusomesha watoto yatima viongozi wanazitumia kuwapeleka watoto wao na yatima hawafaidiki nazo. Ninaomba misaada ikitoka iwe na usimamizi mkubwa.

Suala lingine ni kuhusu matibabu, walemavu wapatiwe vituo vyao vya afya waweze kutibiwa. Muswada siyo mbaya ukipata usimamizi wa uhakika.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza serikali kwa kuuleta Muswada huu. Ninampongeza Waziri, Timu yake, Wadau wote na Kamati ya Bunge, kwa hatua hii. Sheria itakuwa na faida kubwa:-

Kwanza ni mkombozi kwa watu wenye ulemavu kwa kuwa hadhi yao itarudishwa na utu wao kuheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina maombi yafuatayo:-

(a) Serikali itekeleze majukumu yake kama yalivyoelezwa katika sheria inayotungwa. Isimamie kwa kutoa elimu kwa umma na kuona kuwa sheria hii inatekelezwa na kila mdau. Vile vile serikali iongeze juhudi katika kuona kuwa mianya inayosababisha ulemavu inapungua sana. Juhudi hizo ni pamoja na kupunguza ajali mbalimbali kwa kuimarisha sheria mbalimbali zilizopo; kuongeza idadi ya wataalamu wa mazoezi ya viungo katika hospital mbalimbali hadi ngazi ya Vituo vya Afya; ninaamini wataalamu hao wakiongezeka, watu wengi walio katika hatari ya kuwa na ulemavu wataokolewa. Uwepo usimamizi wa ujenzi wa majengo mapya ya serikali na ya binafsi ili kuhakikisha kunakuwa na mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu.

(b) Jamii inahitaji elimu kuweza kuondokana na mawazo potofu iliyonayo juu ya jamii ya watu walio na ulemavu. Ili jamii iweze kuwasaidia watu wenye ulemavu mbalimbali ili kwa kadiri ya uwezo wao waweze kujitegemea, naomba isiwalemaze, iwawezeshe waweze kujitegemea. Wasipewe misaada ya kuwafanya waendelee kuwa tegemezi.

(c) Watu wenye ulemavu wazikubali hali zao bila kukata tama. Hali ya ulemavu wao iwe changamoto kwa kusonga mbele, waamini kuwa wanaweza kuomba fursa stahili kwa ajili ya kuendelea zaidi. Wawe wa kwanza kuitetea na kuisimamia sheria hii na uwe ni wajibu wa watu wenye ulemavu kuitangaza na kuielimisha sheria hii. Kwa kufanya hivyo, itakuwa rahisi kutambua upungufu wa sheria hii na mapema serikali iweze kuleta marekebisho.

Naunga mkono hoja hii kwa kuwa sheria ni nzuri na inatupatia mahali pazuri pa kuanzia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Mheshimwa Profesa David Mwakyusa (Waziri), Mhe. Dkt. Aisha Kigoda (Naibu Waziri), Mama Blandina Nyoni (Katibu MKuu), Wataalamu wote na Wadau mbalimbali walioshiriki kuuandaa Muswada huu mzuri, uliozingatia mambo mbalimbali yenye kuwawezesha watu wenye ulemavu kuendesha maisha yao kama binadamu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuuleta Muswada huu ni hatua moja na matumaini yangu ni kuwa, Waheshimwa Wabunge wenzangu wataupitisha bila wasiwasi. Jambo kubwa ambalo Serikali inapaswa kulizingatia ni kuhakikisha kila Mtanzania anatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu wa viungo wanayo haki ya kwenda kokote, tunaomba wote wenye majengo ya kutolea huduma, waweke barabara za kupitia watu wenye ulemavu. Hii itawasaidia sana kwenda kupata huduma mahali popote, mfano, ofisi za serikali, hospitali, vyoo, mashule na bila kusahau nyumba za kulala wageni. Vilevile hii itawasaidia sana watu wenye ulemavu kwenda popote kupata huduma kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza serikali kwa kuleta vifaa vya aina mbalimbali kwa ajili ya watu wenye ulemavu, bali vifaa hivyo ni vichache, havipatikani kwa urahisi na bei zake ni kubwa ukizingatia walemavu tuliokuwa nao nchini ni wengi. Hivyo, ninaomba serikali ihakikishe vifaa mbalimbali vinapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu; mfano, mashine za kuandikia na maandishi yao yapatikane, baiskeli *(Wheel Chair)*, magongo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafurahisha sana kuona watu wenye ulemavu wanajitahidi sana kujitafutia riziki zao kwa kufanya shughuli mbalimbali ingawa wengi wao hawana vitendea kazi na mitaji ili wawe na uwezo mkubwa wa kuhudumia familia zao, mahali popote wanapojitokeza walemavu wanaojitahihidi basi serikali iwape kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma ya matibabu, serikali iainishe aina ya walemavu na kwa wale ambao hawana uwezo wala ndugu wa kuwahudumia serikali itoe huduma bure na wale wenye uwezo mdogo wachangie nusu ya gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba serikali isomeshe wataalam ili tuwe na wataalam wa kuwasaidia mahali popote wapate huduma; hii ni kwa sababu wengi wao hukosa huduma kwa kushindwa kuongea (mabubu) na (viziwi). Nininaomba serikali isomeshe wataalam ili wawepo maeneo muhimu mfano kwenye hospitali kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Muswada huu utoe sheria ya magari ya abiria yote kuwa na vivuko vya watu wenye ulemavu kwani na wao wanayo hako ya kusafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa watu wenye ulemavu wanahitaji kupatiwa elimu bali wengi wao hawana uwezo wa fedha, ninaiomba serikali ione umuhimu wa kutoa elimu bure ili waweze kujikomboa kwa kujitegemea pale wanapopata taaluma na fani zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba serikali iwasaidie au itoe kipaumbele cha ajira kwa watu wenye ulemavu wapate kazi kwa wale wenye sifa za kupata kazi.

Mwisho, ninapenda kumalizia kwa kuipongeza serikali kwa kutekeleza maombi yangu kwa niaba ya Wanasingida na kukikarabati Chuo cha Wanawake Wasioona kilichopo Singida Mjini pamoja na nyumba za watu wenye ulemavu zilizopo Sukamahela Wilaya ya Manyoni. Ninaomba moyo huu wa Serikali wa kutekeleza ahadi uendelee.

Napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyenzi Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote, kwa jinsi mnavyoweza kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa *speed* na *standard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu wake, pamoja na Wataalam wote, kwa kuandaa Muswada na kuusimamia na leo hii umeletwa Bungeni; nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zetu wengi wenye ulemavu wananyanyasika sana kiasi kwamba, naona kama hawamo kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sheria hii na wao watajua kama Serikali imewajali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Sheria nzuri iliyoletwa, naomba Serikali isimamie vizuri utekelezaji wake, kwani Sheria ni jambo moja makini, utekelezaji wake ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali ina kazi kubwa sana kwani mambo mengi ambayo yanatakiwa kuwasaidia walemavu kufika katika majengo mbalimbali ni kitendawili. Vilevile ukiangalia vyombo vya usafiri hakuna vipaumbele katika kuingia kwenye usafiri huo kama mabasi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza lina watu wawili tu ambao ndiyo wahusika wakubwa, ninaomba serikali walione hilo kwani jamii hii ina walemavu wa aina mbalimbali basi angalau wawe wanne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali itoe elimu ya kutosha kwa jamii ili kuwaelimisha hata mtu akiwa mzima, yeye ni mlemavu mtarajiwa, hivyo basi, wasiwe wanawanyanyapaa ndugu zetu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante nashukuru.

**MHE. YONO STANLEY KEVELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie yafuatayo:-

Kwanza, kutoa msamaha wa kodi na ushuru wa vifaa vya walemavu hasa walemavu wasioona, vifaa vya walemavu wa ngozi (*Albino*), zile dawa za ngozi; walemavu wa viungo vya mikono na miguu kama vile baiskeli za walemavu na walemavu wengine.

Pili, majengo au miundombinu ifanyiwe marekebisho au kujenga miundo mbinu ambayo inakidhi haja ya walemavu wote hasa wasioona na wasiotembea kwa miguu yaani viwete.

Tatu, walemavu wawezeshwe kiuchumi kwa kuwapa fursa sawa katika kupata mikopo ya biashara na kupata ajira. Wasitengwe katika kupata ajira. Waajiri wengi huhitaji uzoefu hata mlemavu anapokuwa na elimu ya kutosha. Pia wapewe elimu ya kutosha ya biashara na mikopo.

Nne, Baraza la Walemavu wahusika wapewe kipaumbele zaidi. Baraza lao lihusishe walemavu wa aina zote na *definite* uwezo na umahiri wa utetezi wa wale ambao wanawawakilisha walemavu.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, Sheria hii ni muhimu sana katika jamii ya Watanzania ambapo itasaidia kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki zao za msingi. Kikamilifu na sio kama msaada bali lazima kwani ni haki ya kila mtu kulingana na mahitaji yake kupata huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya walemavu. Kama tunavyofahamu, watu wenye ulemavu wanahitaji lao maalum tofauti na watu wasio na ulemavu. Wapo walemavu wanaohitaji miguu ya bandia, mikono, fimbo nyeupe, vifaa vya kusaidia kusikia, vifaa vya kuandikia kwa wasioona na mafuta maalum kwa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itoe vifaa vyote hivyo bure kwa wale wasio na uwezo na wale wenye uwezo wanunue kwa gharama nafuu na sheria iweke wazi kuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana bure kwa bei pungufu, robo ya gharama halisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za afya. Nashauri serikali ihakikishe watu wenye ulemavu wanapata huduma za matibabu bure kwa wale wasio na uwezo kabisa na

wenye uwezo wapatiwe matibabu kwa gharama nafuu pia. Kwani walemavu wanahitaji mengi zaidi ya yale ya mtu asiye na ulemavu kwa kuwa ana matumizi mengi ya ziada, hivyo anahitaji huduma zenye unafuu. Hilo nashauri liwekwe wazi katika sheria inayotungwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira. Pamoja na kwamba sheria imeweka wazi masuala mbalimbali likiwemo hili la upatikanaji wa ajira, nashauri sheria iwekwe wazi au kwenye kanuni kuwa mlemavu mwenye elimu au utaalam apatiwe ajira, asibaguliwe na kiwekwe kifungu kinachotoa asilimia kadhaa angalau tano wawe ni watu wenye ulemavu. Na Serikali ianze kama mfano wa utekelezaji wa sheria hiyo mara baada ya kuwekwa sahihi na Rais na baada ya kupitishwa kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, kanuni zisichelewe ili Rais atakapotia sahihi utekelezaji wake uanze mara moja kwani sheria hii ni muhimu sana kwa jamii nzima ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinachohusu uundaji wa Baraza la Mashauriano juu ya masuala yanayohusu walemavu angalau nusu ya Baraza zima liwe na uwakilishi na watu wenye aina mbalimbali ya ulemavu na wengine wawe wataalam wa Wizara na Vyama vya Haki za Binadamu na Vyama vya Kuwahudumia Watu Wenye Ulemavu. Washirikishwe kikamilifu isitokee kikawa kama kitengo au idara ya Serikali. Kipengele cha adhabu itolewayo mahakamani isiwe ni faini ya fedha peke yake bali na kifungo ili kiwe na uzito katika utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kuwa na *registration* sio vibaya ila jambo hili lifanyike kwa makini sana na kila Halmashauri ihakikishe imepata *statistic* kamili ya idadi na aina za walemavu waliopo katika Halmashauri husika katika nchi nzima. Utekelezaji uwe wa haraka ili waweze kutambulika kwa ajili ya upatikanaji huduma muhimu ikiwemo elimu, afya haki za kisheria na upatikanaji wa vifaa muhimu kwa watakaohitaji kulingana na aina ya ulemavu.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, walemavu ni watu kama wasio na ulemavu. Wanachohitaji ni haki yao itakayowawezesha kuishi kama wasio walemavu kwa kupewa mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea watu wenye ulemavu tunajua wako wa aina nyingi lakini pia walemavu vijijini wafikiwe.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilitoa baiskeli 20 (ishirini)za walemavu, kwa walemavu wa Mpanda kwa kukabidhi Chama cha Walemavu kwa kuamini kuwa kwa kupitia chama hicho kinachowakilisha walemavu wa Wilaya nzima baiskeli zingewafikia walengwa (wahitaji) lakini nilisikitika kuona baiskeli zile zinagawiwa kwa walemavu wa Mpanda (Rukwa) Mjini na wengine hata hawakuwa walemavu wanaohitaji baiskeli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu. Walemavu wengi walioko vijijini hata kupata elimu ni shida, maana vituo vingi vya watu wenye ulemavu vipo mijini na

kuwabeba walemavu kuwaleta mjini ni zoezi gumu. Kwa maana hiyo shule zetu vijijini ziboreshwe ili walemavu nao waweze kusoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri. Kama kuna adha ambayo inawakumba walemavu ni ile ya usafiri. Walemavu wetu watengenezewe mazingira mazuri ya usafiri nchi nzima na katika aina mbalimbali za usafiri ikiwemo treni, meli, ndege, mabasi na hata ikiwezekana kwa wenye uwezo Serikali ichangie kuwanunulia magari yaliyotengenezwa kwa matumizi ya walemavu kujiendesha wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala la afya kwa walemavu bado ni tatizo kubwa. Wengi wenye ulemavu hawapati elimu kuhusu elimu za UKIMWI, uzazi wa mpango na hata elimu ya Mfuko wa Afya. Hivyo kutibiwa kwao ni vigumu na maambukizi ya magonjwa na hasa UKIMWI ni rahisi mno kwa watu hao wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuwasilisha Muswada kwa umakini mkubwa. Aidha, napenda kuwapongeza watendaji wote wa Wizara kwa kufanya kazi nzuri ya kuutengeneza Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri yafuatayo kwa nia ya kuboresha:-

(i) Wizara iangalie mfumo mzima wa kutoa huduma za afya kwa walemavu hususan watoto wenye ulemavu bado wanafichwa ndani hivyo hawapati chanjo hata matibabu. Napenda kushauri kwamba watumishi wa afya hususan afya ya msingi wafuatilie kwa karibu watoto wanaozaliwa na ulemavu. Ufuatiliaji huu ni muhimu sana katika maeneo ya vijijini. Aidha, watoto wenye ulemavu wa ngozi yaani *albino* hawapati huduma ya mafuta (*cream*) ya kutunza ngozi zao ili wasipate matatizo ya ngozi yatokanayo na mionzi ya jua. Naomba suala hili liangaliwe kwa karibu.

(ii) Vituo au makazi ya wasiojiweza wakiwepo watu wenye ulemavu. Napenda kusema kwamba haya makazi yana matatizo makubwa sana kwa mfano kituo cha Fungafunga kilichopo Mjini Morogoro. Kituo hiki kimeshindwa kuwahudumia walemavu wanaoishi katika kituo hiki, wengi wao wamekuwa ombaomba mitaani. Hali hii haitoi picha nzuri kwa Serikali, naomba Wizara iangalie upya mfumo mzima wa kutoa huduma kwa walemavu wanaoishi kwenye makazi ya wasiojiweza kwani bado wanateseka.

(iii) Uwezekano wa kuwapatia huduma za Bima za Afya ya Jamii ili waweze kupata tiba bila kupitia mlolongo wa ustawi wa jamii kama ilivyo. Wanahangaika sana wanapokwenda hospitali wanatakiwa kuomba msamaha kwa Ofisa Ustawi wa Hospitali husika katika Hospitali za Wilaya na Mikoa. Lakini katika maeneo ya vijijini Maafisa Ustawi hawapo hivyo msamaha na kuchangia huduma za afya haupatikani. Hali hii inawanyima haki ya kutibiwa hivyo ni vema Wizara ikaangalia uwezekano wa kuwasaidia kuchangia Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii katika maeneo ya vijijini na miji midogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ushauri naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza Serikali kuleta Muswada huu. Bila kusita napenda kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujitahidi kujali watu wenye ulemavu bado kundi hili bado wana matatizo mengi. Vyama vyao vinajitahidi kutetea na kuomba Serikali kuona matatizo yao na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, wapo walemavu wengi baadhi yao wapo nje wamejitokeza kwenda shule na hata kufanya kazi lakini bado wapo wengine wamejificha, hebu tuone Halmashauri zetu wafanye sensa ya mara kwa mara wakisaidiana na watendaji wa vijiji. Lingine ambalo ningeomba sana hebu na sisi wazazi tulio na watoto walemavu na uwezo wetu mdogo tuonekane kama ni kundi ambalo maalum la kuangaliwa kwa jicho la huruma. Maana yake viundwe vikundi ambavyo vitatambulishwa na kupewa misaada na mikopo ili iwawezeshe kupata uwezo wa kulea watoto hawa. Ulezi wao ni mzito mno.

Mwisho nasema naona umuhimu wa sheria hii, kanuni zitoke haraka ili mambo yaende kama tunavyodhamiria. Walemavu wana haki, ni watu wenye kuhitaji maisha bora kama Mtanzania yeyote.

Mheshimiwa Spika, Waalimu wao waonekane kuwa ni watu wenye kazi nzito. Tuwape moyo na kuwathamini sana tena sana. Mungu awabariki sana

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na wengine, nami naomba niishie hapo kwa kuunga mkono na hayo waliyoongea Waheshimiwa wengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Narudia kusema naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimwa Waziri na watendaji wake wote kwa kuandaa Muswada huu muhimu sana na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kuona sasa kundi hili la watu wenye ulemavu hapa nchini limeanza kuangaliwa kwa umuhimu wao ili waweze kujiona kama sehemu ya jamii ya Watanzania wengine jambo ambalo kwa muda mrefu lilisahaulika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Muswada huu pia naishauri Serikali kuweka mpango maalum wa kuwalinda, kuwawezesha na kuwasaidia kwa njia mbalimbali ili waweze kujiwezesha kujiimarisha wao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, wapo walemavu ambao hawana uwezo wa kupata hata nyenzo ya kusogea kutoka eneo moja kwenda lingine. Wapo wanaotambaa barabarani wakiwa wanaomba wapita njia miaka yote. Watu hawa wanaweza wakawa ni walemavu wa baadhi ya viungo tu lakini viungo vingine vinafanya kazi kama kawaida. Kama kalemaa miguu utakuta akili zao zinafanya kazi vizuri sana na tena wengine ni wabunifu wa hali ya juu. Tatizo ni kuwezeshwa, hawawezi kuendelea kuteseka na hali yao hii, lazima Serikali iweke mfumo na utaratibu wa kuwezesha kundi hili.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa kwa walemavu hawa ni kwenye vyombo vya usafiri, kwa kweli haya ni mateso makubwa. Kwenye maeneo yenye msongamano wa wasafiri kundi hili linabaki kwenye vituo vya mabasi hadi wenye nguvu na uwezo wasafiri wote. Hawa wanakuwa wa mwisho na hakuna anayewajali. Ni muhimu sasa Serikali ikatoa agizo kwa vyombo vya usafiri , wamiliki wote wa vyombo hivyo na waongozaji vyombo hivyo wanapoona mlemavu wamsaidie kwanza kwa kuwapa kipaumbele vinginevyo wenzetu hawa wataendelea kuonekana vituoni usiku na hivyo kuwa katika hatari ya uhai na usalama wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia haki za walemavu hawa Serikali ifanye marekebisho ya majengo ya huduma mbalimbali, Hospital, Mashuleni, Vyuoni, Makazini na maeneo mengine ili kuweka maeneo maalum kwa ajili ya watu wa kundi hili la walemavu.

Mheshimiwa Spika, walemavu wa ngozi bado wanawindwa sana, matukio ya kukatwa viungo na kuwaua bado yanaendelea kujitokeza. Nazidi kuisihi Serikali na vyombo vyote vya usalama wa raia kuweka ulinzi kamili kwa kundi hili ili nao waweze kuishi kwa amani na furaha. Wapo ambao wanashindwa kutoka kwenda kwenye shughuli za maendeleo na hata watoto wameacha shule kwa hofu ya kuuawa, juhudi bado zinatakiwa kuwalinda na kuwatambua wahalifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba Serikali kuhakikisha Sheria hii inatekelezwa kikamilifu ili kuleta tija kwa kundi hili na siyo kubaki kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nilipata nafasi ya kuchangia hoja husika kwa kuzungumza kuna masuala muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 6, Ibara ya 3, tafsiri ya *disability*" liandikwe neno *intellectual* badala ya *mental*.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya *committee* katika kipengelee (b), je, neno "Mtaa" halina Kiingereza chake? Naomba ufafanuzi.

Katika sehemu ya Pili, Ibara ya 5, sehemu ya (1)(b), *take appropriate steps to ensure all national policies programmes and legislation*. Kwa msingi huo nashauri

kwamba, masuala ya watu wenye ulemavu ni ya mtambulika, hivyo yafaa yawe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo ni rahisi kutekeleza maelekezo yatakayotolewa kwa Wizara mbalimbali ila yafaa pia kila Wizara iwe na kitengo (*desk*) cha masuala ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 24, Ibara 33(3), naomba ufafanuzi wa chombo kitakachothibitisha kuwa mwajiri fulani anawabagua watu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuipitisha sheria hii ambayo inaonyesha ni jinsi gani inawajali wananchi wake wote na hasa hawa wenye ulemavu ambao nao wana haki sawa na sisi.

Mheshimiwa Spika, elimu itolewe kwa wafanyabiashara mbalimbali ili waweze kuweka mazingira mazuri ambayo yatawarahisishia walemavu kupata huduma zao kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, migahawa na mahoteli na maeneo mengine mengi wanakotoa huduma za vyakula wamekuwa na utamaduni wa kuweka eneo la kunawia mikono ambapo huwa kwenye *stand* hivyo kufanya walemavu wa viungo (wanaotambaa au wasioona) kupata adha ya kuweza kufikia eneo hilo. Kwa kuwa usafi wa mikono ni jambo la msingi katika afya ya mwanadam kuwe na maelekezo au elimu ya kuweza kuiboresha huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, shule zetu za msingi na sekondari nazo wasanifu wa majengo ifike wakati waweke japo michoro ya choo cha kuweza kusaidia watoto walemavu ili waweze kuepukana na kushika uchafu na upata maambukizo ya maradhi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara yako kwa kazi nzuri mnayoifanya. Endeleeni na moyo huo maana kazi yenu ni wito maalum. Hapo mnapoona kuna baadhi ya watendaji wenu wanakiuka maadili ya kazi zao wachukuliwe hatua kali hapo hapo wanapofanya makosa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa kuleta Muswada huu wakati huu kwani wenzetu wenye ulemavu wana hali sawa na Watanzania wengine wasio na ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanzia sasa majengo yote yanayojengwa yazingatie hali ya walemavu. Upande wa masomo walemavu wengi wapewe nafasi za masomo na pia wapewe vifaa vitakavyowawezesha wasome kwa urahisi. Panapowezekana endapo walemavu ni wengi zitengwe shule maalum za *Boarding* kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii baada ya kupitishwa kiundwe chombo cha Kiserikali cha kusimamia matatizo ya Walemavu nchi nzima na pia Halmashauri za Wilaya zielekezwe, ziwe zinatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya walemavu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yako na Wizara ya Mambo ya Ndani ziongeze juhudi kwa kupitia Halmashauri za Wilaya, wenzetu wenye ulemavu wa ngozi wafahamike wote na mahali walipo na ulinzi uongezwe kwao.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa wenzetu walemavu ziongezwe kote Serikalini, Halmashauri za Wilaya, Mashirika ya Umma, Mashirika ya Dini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa wale omba omba wa Dar es Salaam wanaojidai walemavu, hatua za haraka zichukuliwe na Serikali waondolewe maana sasa hivi wanaongezeka sana yaani wanazaana sana kitu ambacho kinaanzisha jamii ambayo italeta matatizo hapa Tanzania siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, narudia kukupongeza na pia naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote mia moja.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa shughuli za walemavu kuwekewa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Huduma kwa walemavu kama zilivyowekwa ndani ya Sheria hii kimsingi ni *"Cross Cutting"* yaani zinahusisha masuala yanayosimamiwa na Wizara mbalimbali, mathalan Wizara ya Kazi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Ufundi, Wizara ya Elimu ya Juu, Ofisi ya Waziri Mkuu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, nchi nyingi duniani zinazotambua haki za walemavu, shughuli za walemavu zimewekwa au chini ya Ofisi ya Rais au Waziri Mkuu kufuatana na mfumo wa utawala katika nchi hiyo. Mifano hiyo ni Namibia, Afrika Kusini, Ghana na hata Marekani katika Ofisi ya Rais, kuna Mshauri wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, ili masuala yanayohusu walemavu, naomba kumshawishi Waziri akubali katika sehemu ya *interpretation*, tafsiri ya neno Waziri, ibadilishwe na kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, tofauti na ilivyo sasa yaani Waziri ambaye kwa wakati huo anasimamia masuala ya (Afya) Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuunda Wizara na majukumu ni ya Mheshimiwa Rais, lakini kwa kuwa Rais haji Bungeni kujibu hoja na kwa kuwa Serikali ni moja na kiongozi wa shughuli za Serikali yuko hapa Bungeni, Serikali ikubali shughuli hizo zihamishiwe, angalau katika Bunge lijalo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ni kuwa, licha ya kuwa masuala haya ni *cross cutting*, *line ministries* zinashughulika na masuala nyeti katika Wizara zao na hivyo

masuala ya ulemavu yanakuwa kama *Appendix* tu.  Mathalan, Wizara ya Afya *priorities* zake ni *killer Diseases* kama kipindupindu, kuharisha na magonjwa mengine yanayoua. Ulemavu hauui na hivyo hauwezi kuwa kipaumble.  Vivyo hivyo kwa Wizara nyingine na vipaumbele vyao.  Lakini Ofisi ya Waziri Mkuu hubeba yote na ipo kwenye nafasi nzuri kuona matatizo mahsusi ya walemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri ashawishike na kukubali badiliko hili.

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kuhusu Muswada huu wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wabunge walionitangulia ambao wamezungumza vizuri na kuunga mkono Muswada huu, lakini pia niseme mwanzoni kwamba naunga mkono isipokuwa nimesimama kwa ajili ya kufafanua mambo machache yanayohusu Sheria na mambo ya kikatiba ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameyaibua walipokuwa wanachangia.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Muswada huu ni harakati ya kutekeleza masharti ya Katiba kama yalivyo katika sehemu ya pili ambayo ina malengo muhimu na misingi ya mwelekeo wa shughuli za Serikali hasa katika Ibara ya 9 na 11.

Kama mnavyofahamu Ibara ya 9 inasema kwamba; “Pamoja na mambo mengine lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au wa chochote kati ya vyombo vyake na udugu na amani kutokana na kufuata Siasa ya Ujamaa na kujitegemea ambayo inasisitiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa kwa kuzingatia mazingira yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, Mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza Sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha kati ya mambo mengi kwamba utu na haki nyinginezo zote za binadam zinaheshimiwa na kuthaminiwa.”

Pia katika Ibara ya 11 (1) inasema kwamba’ “Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi na bila kuathiri haki hizo Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba Bunge lako Tukufu mwaka jana hapa Bungeni tuliridhia mkataba unaoitwa *Convention on the Rights of Persons With Disabilities* ambao ni wa Kimataifa. Mkataba huo unaweka misingi ya viwango vya kuwahudumia watu wenye ulemavu na kama nilivyosikia wengi wamesema jana kwamba kila mtu hapa ni mlemavu mtarajiwa aidha kwa sababu ya uzee au kwa sababu ya ajali. Kwa hiyo basi, Muswada huu unatekeleza hayo na vilevile mtakumbuka kwamba kwenye Ibara ya 13 ambayo wengi mmeizungumzia jana inazungumzia mambo ya ubaguzi.

Sasa kuna hoja nafikiri ya Mheshimiwa Kaka yangu Abubakar Khamis Bakary Mwanasheria Mkuu wa zamani wa Serikali ya Zanzibar na mstaafu, anasema kwamba Sheria inadurufu haki zilizomo kwenye Katiba, ni kweli kwamba Sheria hii haianzishi haki mpya isipokuwa baadhi ya vifungu vinadurufu haki zile za zamani, katika uandishi wa kawaida isingekuwa hivyo, lakini utaratibu huu wa uandishi unarahisisha usomaji wa Sheria hasa kwa wale ambao wanaposoma Sheria hii wanakuwa hawana Katiba. Kwa hiyo, tumetambua hilo na halileti tabu katika uandishi kama unavyofahamu na ninafikiri ulisema kwamba, unataka ufafanuzi siyo kwamba unapinga, ni staili ya uandishi inayotambua kwamba siyo watu wengi wenye weledi wala ufahamu wa haki za kikatiba. Kwa hiyo, tunapoweka kwenye Sheria hiyo nafikiri itatusaidia.

Hoja ya pili ilikuwa ni kuhusu kifungu cha nne ambacho kinataja misingi ya Sheria hii, kwa kweli kwa wale ambao mlisoma ule mkataba wa Kimataifa, kifungu cha nne kinadurufu kwa kiwango fulani Ibara ya 3 ya mkataba ule na kilivyoandikwa vile sisi hatuoni tabu isipokuwa nimeona kwamba tayari tumefanyia marekebisho kwa kuongeza kasehemu kamoja ka (g) kama Wabunge au wadau walivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwamba je, haki hizi zinazotajwa katika sheria hii zinaweza kuhojiwa Mahakamani? Naomba kufanya kazi niliyokuwa naifanya mwanzoni, haki za kikatiba ambazo zinaweza kuhojiwa Mahakamani ni zile ambazo zimetajwa katika Ibara ya 12 – 29 ya Katiba ambayo kwa msingi wa Ibara ya 30(3) ambayo inasema kwamba: "Mtu yeyote anayedai kuwa sharti lolote katika sehemu hii ya sura hii au katika Sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu kwake linavunjwa au inaelekea litavunjwa na mtu yeyote popote katika Jamhuri ya Muungano anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu. " Nafikiri tumepata jibu hapo.

Mheshimiwa Spika, lakini si haki zote zinapatikana Mahakamani, haki hii ni haki ya utendaji kama vile ilivyo haki ya elimu, kila mtu ana haki ya kupata elimu, lakini Serikali iliyoko madarakani inajua kwamba isipotoa haki hiyo Mahakama itakayoamua ni wakati wa kupiga kura kwamba haikutekeleza mambo ambayo yalitakiwa kutekelezwa na hususan katika Sheria hii ni kile kifungu cha 20 na 26 kinachohusu haki za kupata matibabu na wajibu wa Halmashauri kutoa yale ambayo yametajwa katika kifungu cha 20.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mchangiaji ambaye nimemfuata, utekelezaji wa Sheria hii utategemea sana Mamlaka na Mamlaka hiyo ni ile ya *National Advisory Council for Persons with Disability* ambayo iko kwenye Sheria na tayari tumeshaifanyia marekebisho kama mlivyoona kwenye *schedule* ambayo tumesambaza, tumefanya marekebisho ambako tumesema idadi ya watakaokuwa wanahusika na Sheria hii ni watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, tunategemea kwamba *National Advisory Council,* Waziri anayehusika na *Commissioner* ndiyo wasimamizi wakuu wa Sheria hii na watatekeleza kazi zao na watapimwa kwa kutekeleza Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kwa kumalizia kwamba Sheria hii haileti haki mpya na katika Katiba ilivyo hakuna haki pekee za walemavu isipokuwa kuna haki ziada za walemavu ambazo haziangukii pengine katika Ibara ya 12 – 29.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri atazungumza mengine. Kwa hiyo, napenda kuishia hapa na kutamka kwamba naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi huo, sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ndiye mtoa hoja ili aweze kufanya majumuisho ya hoja mbalimbali zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge kutoka jana. Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana ambayo imetusaidia sana katika kuboresha Muswada wetu. Lakini kabla sijajibu baadhi ya hoja naomba niwatambue wale ambao wamechangia kwa kuzungumza lakini vilevile wale ambao wamechangia kwa kuandika. Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mwenyekiti kwa Kamati ya huduma za jamii; Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Frederick Mwita Werema ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Mwanawetu Said Sarafi, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Bujibu K.P. Sakila, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Wilibrod P. Slaa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Elietta Namdumpe Switi, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Halima Omar Kimbau, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. (*Makofi*)

Kama kutakuwa kuna mtu nimemsahau basi nitaomba jina lake ili niweze kumtambua.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla. Wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia Muswada wa Sheria ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2010 kuna maoni mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa maoni na michango yao na ambayo itasaidia katika utekelezaji wa Sheria hii pindi itakapopitishwa na kuanza kutekelezwa na vilevile katika uandaaji wa Kanuni husika.

Maoni hayo mengine yanahitaji ufafanuzi wa jumla kama ifuatavyo:-

Kwanza, marekebisho mbalimbali katika Muswada. Marekebisho mengi yaliyopendekezwa na Kamati ya Huduma za Jamii, Kambi ya Upinzani Bungeni pamoja na Wabunge waliochangia kwa kuzungumza Bungeni na kwa maandishi mapendekezo mengi yamezingatiwa katika jedwali la mabadiliko. Aidha, baadhi ya maeneo ya ziada yameingizwa katika jedwali la ziada yaani *further schedule of amendment* kama ambavyo imesambazwa leo hii baada ya kufanya mawasiliano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Muundo wa Baraza la Taifa la Ushauri liangaliwe. Waheshimiwa Wabunge karibu wengi wamezungumzia kuhusu umuhimu wa kuangalia muundo wa Baraza la Taifa la Ushauri wa Watu Wenye Ulemavu hasa katika idadi ya wajumbe. Baraza lizingatie umuhimu wa kuongeza watu wenye ulemavu katika baraza hili kuliko ilivyo sasa ambapo hatuna.

Mheshimiwa Spika, Watu Wenye Ulemavu watakuwa wanawakilishwa na Mjumbe mmoja kutoka kwenye *Apex Organisation* ya Watu Wenye Ulemavu. Baada ya kutafakari kwa hoja hiyo na kuzingatia usemi wa "*Nothing about us without us*" kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Zuleikha Yunus Haji, Wizara inaona ibara ya 11.1(a) irekebishwe badala ya kuwa na mwakilishi mmoja kutoka kwenye Chama cha Watu Wenye Ulemavu iwe na wawakilishi watano. Marekebisho haya yamezingatiwa kwenye jedwali la ziada la mabadiliko, kipengele cha 11(g) na kwamba itazungumzia, *other five members to be appointed by the Minister from organisation persons with disabilities.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea pendekezo la umuhimu wa kuimarisha vyuo pamoja na shule mbalimbali ambazo zinatoa mafunzo kwa Watu Wenye Ulemavu. Wizara kama ambavyo imekuwa ikifanya itaendelea kukarabati vyuo na shule zilizo chini yake. Aidha, itawasiliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuona shule zao pia zinafanyiwa ukarabati husika. Daftari la kuorodhesha Watu Wenye Ulemavu halitaleta unyanyapaa? Hili ni suala ambalo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaulizia sana. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walionyesha wasiwasi kuhusu uwepo wa daftari kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 23 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, lengo la daftari hili kama lilivyoainishwa katika Ibara 23(3) ni kwa ajili ya utambuzi wa kundi hili na vile vile kupata takwimu sahihi. Takwimu hizi

zitatumiwa na Serikali pamoja na wadau katika kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya kundi hili. Madaftari kama haya yamekuwa yakitumika kwa ajili ya kujua idadi ya watoto walioko katika mazingira hatarishi, lakini vile vile Wizara ina mpango wa kuwa na daftari maalum kwa ajili ya kubaini wazee waliopo hapa nchini. Hivyo lengo likiwa ni kupata takwimu sahihi kwa ajili ya mipango mbalimbali inayohusu makundi maalum na sio kuwanyanyapaa. Wizara ihakikishe kuwa sheria ikipita inatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sheria hii utategemea sana ushirikiano kati ya Wizara yangu pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara mbalimbali, Halmashauri, Vyama vya Watu Wenye Ulemavu, Watu Wenye Ulemavu wenyewe na wadau mbalimbali na jamii. Ili kuhakikisha kuwa sheria hii inatekelezwa ipasavyo Wizara itaandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sheria hii ambayo itaainisha majukumu ya watekelezaji wa sheria hii na namna ya kusimamia kikamilifu. Utayarishaji na uandaaji wa kanuni utaanza mara moja ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii mara itakapokuwa imesainiwa na Mheshimiwa Rais na kupitishwa. Vile vile kufanya tafsiri ya sheria katika lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo itakayotumika na watekelezaji na walengwa wa sheria hii waweze kuielewa kwa urahisi zaidi.

Kuhusu elimu kwa umma itolewe juu ya sheria hii, Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, kwa kupitia Maadhimisho mbalimbali kuhusu masuala ya Watu Wenye Ulemavu Kitaifa ambayo huwa yanafanywa. Kwa mfano, Siku ya Walemavu wa Ngozi tarehe 4 Mei huwa tunaadhimisha Kitaifa. Siku ya Fimbo Nyeupe tarehe 15 Oktoba, Siku ya Walemavu tarehe 3 Desemba na kadhalika ambazo zimekuwa zikitumika katika kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Watu Wenye Ulemavu. Aidha, Maadhimisho haya ambayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka yamekuwa yanafanyika katika mikoa mbalimbali kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii. Wizara itaendelea kufanya ulaghibishi na uhamasishaji jamii kwa lengo la kuwahamasisha jamii ili kutoa uelewa kwa lengo la kuondoa unyanyapaa dhidi ya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walishauri kuwa Watu Wenye Ulemavu wapate matibabu bila ya malipo, suala la tiba hapa nchini linasimamiwa na Sera ya Afya ya mwaka 2007 na Mwongozo wa Uchangiaji wa Huduma za Afya. Mwongozo umetoa namna ambazo watu ambao hawana uwezo jinsi ya kupata msamaha wa kulipia tiba. Aidha, Mfuko wa Afya ya Jamii umeweka utaratibu ambao watu wasio na uwezo wa kulipia waweze kulipia kadri na Halmashauri zao kwa ajili ya kupata tiba bila malipo. Sheria ya Serikali za Mitaa pia imeweka utaratibu ambao watu wasio na uwezo wanaweza kupata huduma mbalimbali za kijamii bila ya malipo ikiwemo afya, hivyo endapo kutakuwa na mtu mwenye ulemavu ambaye hana uwezo ambao wengi wao hawana taratibu zilizopo ziweze kutumika.

Aidha, kuna Mwongozo umetolewa katika hospitali zote kwa watoa huduma kuwatambua Watu Wenye Ulemavu na watu wenye mahitaji maalum ikiwemo Watu Wenye Ulemavu kupewa kipaumbele katika kuwahudumia. Kwa maana hiyo napenda

kuchukua fursa hii kuwakumbusha tena watoa huduma ili waweze kuwatambua watu hawa na waweze kuhakikisha kwamba wanapata huduma.

Mheshimiwa Spika, suala la Sheria ya Kudhibiti UKIMWI Waheshimiwa Wabunge walilizungumzia hasa hapo walipokuwa wanazungumzia suala la kuandika kanuni, Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI tayari imeshaanza kazi na sasa hivi Wizara iko katika hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba kanuni zinakamilika, kwa hivyo punde tu zitakuwa zipo tayari.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa kwa ujumla wake katika vifaa vya Watu Wenye Ulemavu ni kwamba suala la msamaha liliondolewa katika Muswada huu na kwa sababu zipo sheria ambazo zinasimamia masuala ya kodi chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Hata hivyo, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii atafanya mawasiliano na Waziri wa Fedha na Uchumi kuangalia namna ya kuweka misamaha ya kodi ya vifaa vya Watu Wenye Ulemavu katika jedwali la kisheria husika inayohusiana na masuala ya kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa nitajibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wanachangia kwa mdogo na wengine walipokuwa wanachangia katika maandishi. Mheshimiwa Omar Kwaangw' ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii. Mambo mengi aliyokuwa ameyazungumzia ikiwemo mapendekezo ya marekebisho mbalimbali katika Muswada yalikuwa yamejitokeza katika jedwali la marekebisho, lakini vile vile alivyozungumzia kwamba kifungu cha 3 kufufua neno '*parent'* katika tafsiri ya neno '*relative*'. Suala hili lilikuwa limezingatiwa katika jedwali la mabadiliko kipengele C(g). Aidha, katika jedwali la Mabadiliko ya ziada neno *'relative'* lilitafsiriwa zaidi. Kifungu cha 3, kilikuwa kinazungumzia kwamba, '*Minister*' isomeke *"Minister responsible for the right of persons with disability.*

Mheshimiwa Spika, masuala ya Watu Wenye Ulemavu yanashughulikiwa kitaalam na Maafisa wa Ustawi wa Jamii. Hata hivyo, tulivyokuwa tumewasiliana na Mwanasheria Mkuu tumeona kwamba neno hili libaki *"Minister responsible for social welfare'* na hii itakuwa iko katika Wizara ya Afya au katika Wizara yoyote ile itakayokuwepo basi *'Minister'* ambaye atakuwa '*responsible*' na '*social welfare'* ndiye atakayeshughulikia suala hili hata kama hili suala la Watu Wenye Ulemavu halitakuwa chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, pia alizungumzia kuhusu kuongeza kifungu kipya cha 4(j) ambacho kitasomeka '*Provide adequate standard of living and social protection' na* suala hili tumelizingatia katika jedwali la mabadiliko ya ziada.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 Kamati inaona kuna kujirudia kwa maneno ambayo hayana msingi na kushauri kifungu cha 6(a) maneno '*All persons with disabilities'* yaliyoko katika msitari wa 2 yaondolewe na isomeke *'under this act and that they are full entitled'*. Suala hili limezingatiwa katika jedwali la mabadiliko ya ziada kwa

kukiandika kifungu kipya. Katika sehemu ya 3 kifungu cha 12.1 kiongezwe kifungu kipya cha 12.1 (k) katika ngazi ya Baraza na kusomeka *'To monitor and evaluate the implementation of this act in relation to the convention on the right of the person with disabilities'*. Suala hili limezingatiwa katika jedwali la mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 (d) na (e) neno *the* mwanzoni mwa vifungu liondolewe, hili tulikuwa tume-*overlook* tumelijadili kweli tulipokuwa kwenye Kamati. Kifungu cha 35 neno '*physically environment'* lisomeke '*built environment'* ili kuondoa maneno ya asili ambayo sio rahisi kuyachukua na neno *'buildings'* lisomeke '*infrastructure'* ili kujumuisha maeneo ya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara tumeona kwamba haitakuwa vema kama tutabadilisha haya maneno ya '*buildings*' kuweka *'infrastructure'* na hili tumeliona hivi kwa sababu gani, kwa sababu wakati mwingine inapokuwa walemavu wanakwenda katika maeneo ya kufanyia mikutano si lazima wawe wanaingia katika nyumba au majengo. Wakati mwingine mikutano inaweza ikafanyika nje kwa maana hii tumezingatia kwamba inawezekana mkutano ukafanyika mahali ambapo kuna mlima au kuna kitu ambacho kitamkwaza huyu mlemavu. Kwa hiyo, tumeona kwamba ukiweka neno '*infrastructure'* hili itakuwa ni '*very restrictive'*. Kwa hiyo, tumeona kwamba ibaki hivi hivi ili kuweza kuhakikisha kwamba maeneo haya na *'environment'* inajengwa ili kuweza kuwasaidia Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamesema Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha Idara ya Ustawi wa Jamii, Halmashauri zijengewe uwezo wa kifedha na raslimali watu ili sheria hii iweze kutekelezwa ipasavyo katika kutoa haki za Watu Wenye Ulemavu. Asasi za Kiserikali na taasisi za habari zijumuishwe katika utoaji wa elimu juu ya haki na Watu Wenye Ulemavu ili kuondoa mila na dhana potofu katika jamii ya Watu Wenye Ulemavu.

Aidha, tunaishauri Serikali kuwa masuala ya Watu Wenye Ulemavu sasa yawe masuala ya mtambuka na hivyo yajumuishwe katika kila mpango wa Serikali na hasa katika bajeti ya Wizara zote. Ni kweli hili tumelipokea na kwa sababu suala la Walemavu tulishasema kwamba ni mtambuka, nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa kama kiongozi wa Serikali, yeye atatupa maelekezo ili tuweze kuona ni jinsi gani Wizara husika au Wizara zote zitaliingiza hili katika mipango hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar kutoka Kambi ya Upinzani alizungumzia kwamba, katika kifungu cha 3 tafsiri ya neno '*positive discrimination'* na kifungu 6(c) yametumika na inaonekana maeneo haya kutumika katika Muswada si sawa kwani yanaonyesha kwamba ni ubaguzi wa unyanyapaa. Neno '*positive discrimination'* katika Muswada huu limetumika kwa lengo la kuendelea kutoa haki kwa wenye ulemavu na kuzingatia kwamba kundi la Watu Wenye Ulemavu linahitaji uangalizi wa ziada, hivyo imedhamiria kuweka msisitizo kwamba kundi hili linahitaji uangalizi wa ziada na sio kwamba tunaandika hivi kwa sababu ya kuwanyanyapaa. Nafikiri na Mwanasheria Mkuu pia alilizungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kifungu cha 14, 16 na 17 kinazungumzia '*social support*'. Kambi ya Upinzani inapenda kujua majukumu ya '*social support'* kwa Serikali ni yapi. Wizara inatoa '*social support*' kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu na baadhi ya huduma hizo ni kama vile kutoa vifaa vya kujimudu, mafunzo ya ufundi, stadi za kazi, mitaji kwa ajili ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali, kuchangia gharama za elimu na afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinazungumzia uundwaji yaani *formulations* ya programu ambazo Waziri mwenye dhamana kwa kushauriana na Baraza la Watu Wenye Ulemavu ili kuangalia hizo programu zinaundwa, hili suala tumelishalitolea ufafanuzi. Suala la kuongeza Wajumbe ambalo nimelizungumzia hili pia tumeshalizungumzia wakati nilipokuwa nimezungumzia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna hoja ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi na kwa mdomo kwa mfano Mheshimiwa Mntangi, Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Selelii. Waliouliza masuala haya ni wengi sana siwezi kuwataja hapa ili tusipoteze muda. Kama nilivyosema kuna waliozungumzia kuhusu kutoa mafunzo kwa watu wanaohudumia Watu Wenye Ulemavu. Suala hili limezingatiwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu kwa hiyo litatekelezwa kuongeza idadi ya vituo vya kuhudumia Watu Wenye Ulemavu. Lengo letu ni kutoa huduma hizo kwenye jamii na kwamba kumweka mtu kwenye makazi basi hiyo iwe ni hatua ya mwisho. Lakini pale inapobidi vituo vitaongezeka kulingana na mahitaji.

Kutoa elimu kwa umma ili umma uache kunyanyapaa Watu Wenye Ulemavu, hili nimeshalizungumza kwamba tunafanya maadhimisho. Lakini pia Serikali ilikuwa ikitoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na maadhimisho mbalimbali kama nilivyosema hapo awali. Huduma za bure afya, elimu kuanzia sekondari hadi elimu ya juu kwa Watu Wenye Ulemavu. Huduma ya afya zitatolewa kutokana na taratibu ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 na Sera ya Uchangiaji ya Huduma ya Afya. Wizara ina taratibu maalum kwa ajili ya kuwatambua watoto walio katika mazingira hatarishi na pamoja wanatoka katika familia zisizo na uwezo. Lakini vile vile tutawasiliana na Wizara ya Elimu kupitia TAMISEMI na yenyewe italiangalia hili ili kuweza kuona ni jinsi gani hawa Watu Wenye Ulemavu wanapata elimu kama Waheshimiwa Wabunge walivyozungumza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la gharama kubwa za vifaa na kwamba wale ambao wanahitaji walemavu wapewe bure hasa wale wasiojiweza lakini vile vile vifaa viingizwe katika Mfuko wa Afya ya Jamii. Hili ni kweli, vifaa kama tunavyofahamu wote ni gharama kubwa, kwa hiyo tutaliangalia ili tuweze kuona kama tutaweza kuingiza katika Mfuko lakini pia Mfuko wa Jamii lakini vile vile kuangalia ni jinsi gani tutaongeza bajeti ili kuweza kununua hivi vitu. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo linaweza likazungumzika.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha Mfuko maalum kwa ajili ya kusaidia miradi ya ujasiriamali kwa Watu Wenye Ulemavu. Suala hili tumelizingatia katika Muswada,

kifungu cha 13(2), lakini vile vile katika masuala yote ya ujasiriamali kama tunasema walemavu kama wananchi wengine wowote wale wanayo haki ya kupata misaada na kuwezeshwa katika mifuko mingine yoyote ile ambayo inasaidia watu ambao ni wajasiriamali. Sheria za Usalama Barabarani ziangaliwe upya kwa kuweka alama za Watu Wenye Ulemavu kupita kwa urahisi barabarani. Suala hili limezingatiwa na liko katika jedwali la mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 43(3) ambalo ni jedwali jipya, limezungumzia kwamba Waziri mwenye dhamana pamoja na Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Mambo ya Ndani watakaa pamoja waweze kuona ni jinsi gani hili suala litawekwa vizuri ili Watu Wenye Ulemavu waweze kufaidi matumizi mazuri kwa urahisi wa barabara, lakini vile vile kuwepo na alama. Serikali imeweka mazingira gani ya kuwasaidia Watu Wenye Ulemavu kuweza kufikia huduma muhimu, suala hili liko katika Muswada husika katika sehemu ya 8 kifungu cha 35.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumzia pia kuongeza idadi ya Wajumbe wa Kamati toka Ofisi mbalimbali kama Wizara ya Miundombinu, Sayansi na Teknolojia na Mambo ya Ndani. Hili lilizungumzwa na Waheshimiwa Kahama, Khadija Al-Qassim, Mheshimiwa Mchemba, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Mhonga na wengine. Wajumbe wa kutoka Serikalini watabaki kama walivyo katika Muswada na hawa ambao waliopendekezwa basi wataingia tu kama *co-opted members*. Kwa hiyo, hawawezi wakaingia huku kama Wajumbe wa kudumu. Lakini vile vile nimesema kwamba kuongeza idadi ya Wajumbe walemavu kwa kuzingatia jinsia, ushauri huu umepokelewa na utaongezewa kutoka mtu mmoja ataongezeka kama ambavyo tutakavyoona na kwamba jinsia itazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Watu Wenye Ulemavu walindwe juu ya virusi vya UKIMWI kwa kupatiwa mafunzo ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na vile vile masuala ya uzazi wa mpango. Suala hili limezingatiwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma ya Watu Wenye Ulemavu na vile vile suala hili litazingatiwa katika Sera ya Afya ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika suala la usafiri Watu Wenye Ulemavu walipe nauli nusu ya kiwango kwa ajili ya usafiri wa vyombo vya usafiri kama mabasi, maboti na kadhalika na viwe na alama maalum kwa Watu Wenye Ulemavu na suala hili liwe ni lazima. Wizara imepokea ushauri huu na suala hili kwa ajili ya utekelezaji inahitaji kuwasiliana na Wizara inayohusika na usalama barabarani. Kwa maana hiyo, tutakaa kama Wizara tuweze kuona kwamba ni jinsi gani sheria hizi na wale ambao wanahusika basi watapewa maagizo na Serikali. Watu Wenye Ulemavu wana watoto ambao wanahitaji kutunzwa, hivyo ni vyema Serikali iangalie juu ya matunzo na elimu ya watoto hao.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto limezingatiwa katika Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Novemba mwaka 2009, Muswada ukipita na kuwa sheria Waheshimiwa Wabunge wote karibu wamezungumzia kwamba wahusika wawe makini katika kuutekeleza. Suala hili tumelizingatia na utekelezaji huu utazingatia kushirikiana kwa karibu sana na Ofisi

ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa maana kwenye Halmashauri na wadau na wote wale ambao wanashughulika na masuala ya Watu Wenye Ulemavu. Watu Wenye Ulemavu wenye sifa, wapewe kipaumbele katika kupata ajira, hili suala lilizingatiwa katika suala zima la Muswada. Kwenye Mkutano wa Kimataifa unaohusu Watu Wenye Ulemavu ni vema walemavu wakashirikishwa pamoja na wawakillishi wao Bungeni pia waende.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii Wizara itazingatia ili kuhakikisha kwamba na wenyewe wanashiriki. Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika masuala ya siasa na uchaguzi imesemwa kwenye sheria lakini kuhusu haki wao kuchaguliwa haijaongelewa. Haki ya uchaguzi ni haki ya kikatiba na Watu Wenye Ulemavu wapo na masuala mengine ya uchaguzi yako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini Wabunge vile vile kutolewa kwenye masuala ya Watu Wenye Ulemavu na Kambi ya Upinzani iangaliwe. Sasa hili nadhani sisi Chama cha Mapinduzi tumeshafanya, hii nadhani Mheshimiwa Zitto alipozungumzia hapa yeye kama ni kiongozi sijui ni Naibu, kitu kama hicho, ni kiongozi wa CHADEMA, nadhani atakuwa mstari wa mbele kwenda kuwaambia kwenye chama chake ili walizingatie hili ili nao waweze kuwasilisha watu wao.

Mheshimiwa Margreth Mkanga alizungumzia kwamba kipengele 11.9 alipendekeza Kamishna kushirikiana na Mkurugenzi wa Wakala wa Taifa wa Takwimu katika kupata takwimu za Watu Wenye Ulemavu, vifaa ni ghali, washirikiane katika kupata zile takwimu. Sisi tumepokea ushauri huu, Kamishna atashirikiana na Wakala wa Takwimu wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, alizungumzia pia suala la vifaa vya kujimudu kwamba ni ghali kama nilivyozungumza. Ni kweli tunakubali kwa maana hiyo na lenyewe tunalifanyia kazi. Utekelezaji wa sheria hii unajumuisha Wizara saba ingekuwa vema Muswada huu ukawekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hili limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara hatuna jibu kwa hili, tunachosema ni kwamba, Wizara ambayo inahusika na Ustawi wa Jamii ndiyo itakuwa inazungumzia kwa sasa hivi. Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa kama kiongozi wetu wa Upinzani mimi nadhani sina sababu ya kuzungumzia hapa yeye mwenyewe atakuwa na majibu, sitaki kulisemea hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu kwa madereva kwa alama za barabarani, ni kweli kabisa inatakiwa itolewe. Kwa maana hii, Serikali tunalipokea na kwa sababu ni mtambuka basi tutashirikiana na zile Wizara zote zinazohusika ili tuweze kuona kwamba wahusika wanaelekeza kwa wale madereva ili kuhakikisha usalama wa wale ambao wanatumia barabara unapatikana.

Mheshimiwa Arfi na Mheshimiwa mwingine walizungumzia pia kuhusu ukurasa 23 kwenye yale madhumuni. Hili nafikiri tulikuwa tumeshaliona, hii ni *typing error* tu kile kipengele cha mambo ya posta na kupeleka vifurushi kwa kweli hamna na ndiyo maana unapoangalia hata katika Muswada wetu hili suala la mambo ya posta kweli halipo. Kwa hiyo, ni uchapaji tu nawahakikishia kabisa katika uandikaji wa sheria zitakapotokea hiki kipengele tutakachozungumzia hili pia kutakuwa na suala la simu na

televisheni.  Kwa hiyo hii ilikuwa tu ni *typing error*.  Kwa hiyo, suala hilo tumepokea kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia suala lile la vituo vya Mlali kwamba Serikali itenge fedha, wapatiwe Madaktari Bingwa pamoja na vituo vingine vyote, sisi tumepokea na tutafanya utaratibu kuweza kuona kwamba ni jinsi gani tunaweza tukawapatia Madaktari kwa sababu wanatusaidia kwa kweli na tunawapongeza sana, kazi wanayoifanya ni nzuri na kwa hakika wanahitaji kupata msaada.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanawetu alisema kipengele kipi kitatoa adhabu kwa watu wanaowaficha watoto au Watu Wenye Ulemavu, hili litashughulikiwa chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura 16. Serikali itenge eneo maalum ili kuwatunza Watu Wenye Ulemavu ili wawe katika mazingira mazuri kwa sababu wanakuwa na ujuzi wa aina mbalimbali na ametoa mfano wa Mombasa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kama nilivyosema mwanzo Serikali kwa kweli hatuna mpango mpaka sasa wa kusema tuwatengee mahali pa kuwaweka wenye ulemavu. Lakini ni jambo zuri kama tutakuwa tunafanya jinsi gani ya kuwawezesha ili waweze kuona maeneo ya kufanyia kazi Watu Wenye Ulemavu wayashughulikie.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanazungumzia kwamba wanaona si vema kwamba suala la walemavu na Ustawi wa Jamii likawa chini ya Wizara ya Afya.  Kwa hiyo, nasema kwamba, sisi kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa sasa hivi kwa sababu Ustawi wa Jamii iko chini ya Wizara ya Afya tutaendelea kutekeleza hii sera ama hii sheria ambayo tunaipitisha.  Sasa jambo ambalo tumesema kwamba ihamishwe kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiyo kiongozi wetu wa shughuli za Serikali, nilikosea naomba radhi Mheshimiwa Waziri Mkuu.  Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndio kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali amelisikia na amesikiliza mijadala mizima ya Wabunge na yeye ndio mtu wa karibu zaidi kabisa atakayekuwa anamshauri Mheshimiwa Rais.  Kwa hiyo hili sitaki kulisemea kwa sababu nikijua kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye mwenyewe ndio atajua hili jibu litajibiwa namna gani, naomba nirekebishe, nafuta usemi ule niliosema wakati ule nilikuwa nimekosea.

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyozungumzwa hapa kwa kweli ni mengi, lakini mengi yalikuwa yanajirudirudia, nataka niseme tu tukianza kuyazungumza hapa yatachukua zaidi ya saa moja.  Ninachotaka kusema ni kwamba, sisi kama Wizara tumepokea kwa shukrani kubwa sana yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika kuboresha Muswada huu.  Ninachoweza kuahidi ni kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi wamechangia na vile vile waliochangia kwa kuongea hapa basi tutayaandika vizuri ili kuyaweka na kuyawasilisha majibu katika Ofisi ya Mheshimiwa Spika ili Wabunge waweze kugawiwa ili na wenyewe waweze kufanya rejea.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile hili ni suala endelevu, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wale wote waliochangia napenda pia niwashukuru sana na

wale wenzetu wa vyama vya Watu Wenye Ulemavu lakini niwashukuru na wadau wote ambao wametusaidia sana katika uboreshaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii umejibu vizuri sana. Nadhani Kamati itakapowadia haitachukua muda mrefu sana kwa sababu bado tuna ile Miswada mingine ambayo inahusu sekta ya mifugo.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2010
### (*The Persons with Disabilities Bill,* 2010)

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. DR. WILIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 3, katika mchango wa maandishi nilipendekeza pale kwenye *section* ya *interpretation* inapozungumzia Waziri kuwa Waziri labda ninukuu kwa Kiingereza "*The Minister responsible for social welfare.* Sasa hoja ya msingi hapa ni kwamba *social welfare* ni pana kuliko walemavu. Suala la walemavu sasa hivi liko ndani ya *social welfare.* Hoja yetu ilikuwa ni kwamba tunatunga sheria na kama tunatunga sheria na tunataka walemavu wakae mahali ambapo watakuwa salama na watahudumiwa basi tungewaondoa katika *social welfare* tuwaweke mahali maalum kama nchi nyingi zilivyofanya.

Kuna nchi nyingi zimeweka chini ya Ofisi ya Rais moja kwa moja, nchi nyingine zimeweka kwa Waziri Mkuu, Marekani imeweka katika Ofisi ya Rais Mshauri, sasa tulifikiri kwamba hali hii ya *positive discrimination* ambayo sheria inaizungumzia vizuri ifanye kazi Waziri Mkuu angetupa kauli kwa sababu hapa tunatunga sheria na sheria iweze kumfunga yeyote atakayekuwepo kwamba suala hili liwe la kimtambuka na likae moja kwa moja au Ofisi ya Rais au Ofisi ya Waziri Mkuu. Natambua kabisa kazi ya kuchagua Wizara ni ya Rais, lakini Rais anaongozwa pia na Bunge kwa maana ya mahitaji maalum ya jamii, sasa tungependa Waziri Mkuu atupe ufafanuzi je, Serikali inatoa kauli gani?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua jambo hili limeelekezwa kwa Waziri Mkuu lakini kabla halijafika huko, naomba nilizungumzie kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya neno Waziri inategemeana na shughuli atakayoifanya. Kwa maana ya Muswada wowote au Sheria yoyote ile, Waziri pia anaweza kuwa ni Rais, Waziri pia anaweza kuwa ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, lilivyo hivi hapa hata ikiamuliwa kwamba suala hili sasa liende kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Sheria hii, ndiye atakuwa Waziri mhusika au kama Serikali itaamua kwamba suala hili liende kwa Rais basi Rais ndiye atakuwa Waziri mhusika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa inatosheleza?

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini kama tunafanya *positive discrimination* badala ya *Minister responsible for Social Welfare* basi neno sahihi pale kwa maana anayoisema ni *Minister responsible for disability matters*, hapo ndipo ingekuwa kwamba kuna mtu maalum anayeshughulikia *disabilities*. Hapa anashughulikia *social welfare*, *social welfare* kama nilivyosema ni pana kuliko ulemavu, hata watoto wa mitaani ni *social welfare*, akina mama wajane, ni *social welfare* lakini hapa tunataka walemavu *specifically* wawe *addressed* kama walemavu na ili Rais aweze kuwa-*guided*, Sheria lazima itamke kitu cha aina hiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa na wazo hilo litazingatiwa, itakuwa *Minister responsible for people with disabilities.* *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa *drafting* irekebishe hilo, tusije tukapata matatizo baadaye tena. Maneno hayo yameingia kwenye *Hansard*, kwa hiyo yakae hivyo lakini kisheria itakuwa *persons not people.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5, nafikiri kuwe na marekebisho kidogo, ukianza kusoma *subsection* (1) inasema:-

*"The Minister shall take appropriate steps to ensure and promote the realization of all rights and freedoms of persons…"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu lipo pale kwenye *freedoms of persons,* nafikiri ingeandikwa *rights and freedom of persons* badala ya kusema *freedoms*.

**MWENYEKITI:** Kisheria inakubalika hivyo hivyo unavyoiona hapa na tumeitumia hivyo, ni uandishi tu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 16

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 16, ninaangalia zaidi tatizo la utekelezaji na likiachwa lilivyo, halitaweza kuwasaidia watu wetu wenye ulemavu. Napenda kushauri, kwa sababu unapozungumza tu kwamba, *the relative shall be under collective obligation,* sasa nani anawaleta pamoja? Halafu

inaendelea mpaka Ibara ya 17 ambapo inataka watu hawa waende Mahakamani, tunajua hawa ni watu wenye shida, nchi yetu Mahakama ziko mbali kilomita 100 na zaidi, tukiwaacha itakuwa tatizo, napendekeza katika namna bora ya kuwasaidia, Kifungu kinachomruhusu Waziri kutengeneza Kanuni basi utaratibu mzuri wa kuwasaidia na kutekeleza Kifungu hiki uweze kuandaliwa. Hilo ni ombi tu kwa Serikali.

**MWENYEKITI:** Nadhani ombi hilo ni jema.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 26

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 26(4), ukiisoma haisomeki vizuri, inasema:-

*"The Minister shall, after consultation with the Council, ensure that-*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *kwenye sub-section (b*), kuna kujirudia kwa maneno '*ensure that'*. Kwa hiyo, napendekeza yale maneno '*ensure that'* kwenye *sub-section (b)* yaondolewe lakini pia maneno yale unapoanza na *The Minister shall, after consultation with the Council, ensure that,* yale yatoke halafu kwenye *sub-section (a)* neno *ensure that* ndiyo lianze ukienda kwa mpangilio huo na yale mengine mpaka *section (d)* zitakuwa zinakubali vizuri.

**MWENYEKITI:** Lakini maneno *ensure that* ni kwa hayo yote, kwa hiyo nadhani ilivyowekwa ni sawa, ila uko sahihi kwamba kwenye *sub-section (b)* hakuna haja ya kurudia maneno *ensure that*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mbona hamjibu? Tunapitisha Muswada sasa, najua wengi mawazo yetu yako Majimbo lakini kazi iliyopo mbele yetu lazima tuimalize. *(Kicheko)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 48

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 59

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho yaliyofanywa kwenye *part* nyingine bado ile inasomeka *Part XI* badala ya kusomeka *Part* XII. Mengine yalisahihishwa lakini hapa paliachwa na kwenye masahihisho sijaona.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zambi ameusoma vizuri sana Muswada huu. Ni dhahiri hilo inabidi tubadili hapo ni *Part XII*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 60

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 61
Ibara ya 62

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 63
Ibara ya 64

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2
Jedwali la 3
Jedwali la 4

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 5

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali la tano, sehemu ya kwanza inayosema *compositions, functions, tenure and reporting of Village Committee*. Mimi nafikiri pale *Village* ni Mtaa kwa sababu ukienda kwenye jedwali la nne pale ndipo wanapo-*refer Village* lakini jedwali la tano ina-*refer* Mtaa. *Otherwise* pale inasomeka *Village* na huku kwenye jedwali la tano lina-*refer Village*, mimi nadhani hapa ni Mtaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama hilo linakubalika, ukienda jedwali la tano hilo hilo, *subsection 2*, wanapoanza na *functions of the Mtaa Committee* nadhani

ingesomeka *functions of the Mtaa Committee shall be,* kuwepo na neno '*to'* ambalo naona lina-*miss* pale.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, huu ni mfano mzuri wa kusoma hii Miswada vizuri. Ahsante Mheshimiwa Zambi. *(Makofi)*

Ni kweli *marginal note* iliyoko ukurasa wa 44 imerudiwa ukurasa wa 45 kwa makosa, pale ni Mtaa *Committee* badala ya *Village Committee* kujirudia mara mbili na kweli *functions* haiungani vizuri ukisema *shall be ensure* itakuwa *to ensure*, ahsante sana.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka, 2010 *(The Persons With Disabilities Bill, 2010)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa hoja, kwa taarifa ya kazi ya Kamati.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Persons With Disabilities Act, 2010* pamoja na mabadiliko yake kifungu kwa kifungu na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *The Persons With Disabilities Bill, 2010,* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge sasa hoja iliyo mbele ni ya kupitisha Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka, 2010 *(The Persons With Disabilities Bill, 2010).* Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*

*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umesomwa kwa Mara ya Tatu kwa maana hiyo sasa na kwa mujibu wa Kanuni za Kutunga Sheria, Muswada huu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, leo tarehe 14/4/2010, umepitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaendelea kuipongeza Serikali lakini tunatoa rai kwa Kanuni kutungwa haraka ili Muswada au Sheria mara itakapopata kibali iweze kufanya kazi muhimu sana, hii ya kuwapunguzia adha ndugu zetu wenye ulemavu.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kwa sababu muda upo kwa kusoma hotuba inayofuata ya ile Miswada miwili ya mifugo lakini kwa sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Spika aendelee kwa kazi hiyo.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu shughuli inayofuata.

**Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010. *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010)* na Muswada wa Sheria ya Malisho na Vyakula vya Mifugo wa Mwaka 2010 *(The Grazing Land and Animal Feed Resources Bill, 2010)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa Hoja, naamini muda uliopo utatosha na kama hautatosha, nitatumia mamlaka ya kwamba tutamsikiliza mpaka atakapomaliza kuwasilisha.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kutoa hoja, naomba nichukue nafasi hii, kuwapa pole wananchi wa Jimbo langu la Chato ambapo zaidi ya nyumba 450 ziliharibiwa na mafuriko ya mvua. Lakini pia nichukue nafasi hii, kuishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Afya, kwa hatua mbalimbali ambazo wamekuwa wakizichukua ambapo hadi sasa zaidi ya madawa ya thamani ya shilingi milioni 15 yameshapelekwa, mahema 30, magodoro 130 na mablanketi zaidi 323 na hatua zingine zinaendela kuchukuliwa katika kukabiliana na matatizo ya wananchi wa Kibumba, Imaramawazo na Kata yote ya Kibumba katika Wilaya ya Chato.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Act, 2010)* pomoja na Jedwali la Marekebisho sasa Usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kushukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Gideon Cheyo,

Mbunge wa Ileje, kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Muswada huu kwenye Kamati Tarehe 30 – 31 Machi, 2010 Jijini Dar es Salaam. Pia napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa michango yao tarehe 31/3/2010 mbele ya Kamati hiyo. Michango na maoni ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau wote tumeyazingatia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010),* inayopendekezwa kutungwa, ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo lakini pia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na Mpango Mkakati wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, Ibara ya 3(10) kuhusu mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo, inatamka kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itahamasisha, itaimarisha utoaji wa huduma na kuratibu utekelezaji wa msingi wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo nchini kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

Hali ilivyo nchini kwa sasa ni kuwa, hakuna mfumo huu. Wafugaji wa asili na wakibiashara, hutambua mifugo yao kwa chapa au hereni za masikioni pasipo kusajiliwa na hivyo kuwa vigumu kufuatiliwa. Matokeo ya kutokuwepo kwa mfumo huu, ni kwamba imekuwa vigumu kudhibiti ueneaji wa magonjwa ya mifugo na wizi wa mifugo kwa kuwa inakuwa ni vigumu kutambua mifugo kwa alama za asili na mfumo usiosajiliwa. Pia wafugaji na mifugo yao wamekuwa wakihama pasipo kutambuliwa kwa urahisi kuwa wapo machungani au wanahama na hivyo kuleta uvunjaji wa amani kwa baadhi ya maeneo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini nyingi duniani na Barani Afrika, zimeanzisha na kuendesha mfumo huu zikiwa na Sheria pamoja na Kanuni zake za kusimamia utekelezaji. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika yaani *SADC*, zipo katika hatua tofauti za kuwa na mfumo huu zikiongozwa na Botswana, Namibia, Zimbabwe  Afrika Kusini, Kenya, Madagascar, Misri na Swaziland.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa Sheria hii, kunatarajiwa kuleta matokeo yafuatayo:-

Kwanza, kuzuia na kudhibiti wizi na unyang’anyi wa mifugo kwa kupunguza ushawishi wa kuiba ikiwa mifugo itakayoibiwa itaweza kutambuliwa kwa uhakika na mapema. Wizi wa mifugo umeongezeka na kukithiri katika maeneo ya mipakani hususani Mkoa wa Mara na kuhatarisha usalama wa wananchi unaoambatana na matumizi ya silaha nyepesi na upotevu wa maisha ya watu na kuathiri hali ya uchumi na uhusiano wa kijamii katika maeneo hayo. Kwa hiyo, Muswada huu utasaidia kupunguza matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, utapunguza na kudhibitiwa kwa usafirishaji na uhamishaji holela wa mifugo hususan katika maeneo ya mipaka na nchi jirani na ndani

ya nchi, kutoka kijiji na Wilaya moja kwenda nyingine na hivyo utadhibiti ueneaji magonjwa ya mifugo na kupunguza migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa rasilimali ardhi na maji.

Tatu, Tanzania itaongeza mauzo na mapato ya fedha za kigeni kwa kushiriki katika biashara ya kimataifa ya mifugo na bidhaa zinatokana na wanyama baada ya kuwa na mfumo huu ambao nchi nyingi zinazonunua mifugo na mazao yake kama nchi za Jumuiya ya Ulaya, Japan na Korea ya Kusini zinataka nchi zinazowauzia mazao kuwa na mfumo huu.

Nne, kutaongeza uzalishaji wa mifugo wenye tija kwa kuwezesha udhibiti wa magonjwa ya mifugo na taratibu za kuboresha kosafu za mifugo.

Tano, kutapunguza uharibifu wa mazingira kutokana na kudhibiti uhamaji holela wa mifugo.

Sita, mfumo huu utawezesha mafanikio kwa wawekezaji watarajiwa na waliopo katika ujenzi wa viwanda vya nyama na machinjio ya kisasa vyenye kulenga soko la nje kwa sababu soko la nje linahamasisha kwamba watu watakaouziwa nyama ni lazima wawe wana sheria zinazoendana na mfumo huu.

Saba, kutakuwepo na chombo kinachotambuliwa kisheria kuendesha mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo ambacho kitakuwa na majukumu yatakayobainishwa.

Nane, kuongeza uzalishaji wa mifugo kutokana na mahitaji ya soko, yaani *demanded driven*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuanzishwa kwa mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo utakaoweka utambuzi, usajili wa mifugo na wafugaji pamoja na uwekaji wa kumbukukumbu kuwa suala la kisheria.

Pili, kubainisha taratibu za kutambua na kusajili mifugo na mashamba ya mifugo na kuweka wazi mifugo itakayohusika pamoja na ubebabaji wa gharama za uendeshaji kati ya Serikali na wafugaji.

Tatu, kutofautisha na kueleza namna ya kutumia mifumo ya asili ya utambuzi inayotumiwa na wagufaji sanjari na mfumo wa kitaifa wa utambuzi na ufuatiliaji mifugo.

Nne, kuweka wazi kazi, mamlaka na majukumu ya wadau mbalimbali katika kutekeleza na kusimamia sheria hii kwa kuzingatia mgawanyo na majukumu baina ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na ushirikishaji wa sekta binafsi.

Tano, kutoa fursa kwa asasi binafsi au Serikali kukasimu kwa vyombo vilivyoko kisheria kama Bodi za Nyama kuendesha mfumo huu.

Sita, kutoa maelekezo ya usimikaji, msimamo wa ufuatiliaji katika machinjio ya mifugo hususani kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi na pia maelekezo ya uwekaji alama bidhaa za mifugo, kuwezesha ufuatiliaji bidhaa hiyo kutoka shambani hadi mezani *(farm to folk).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu tano zifuatazo:-

Sehemu ya Kwanza ambayo ni kifungu cha 1-3 inaweka masharti ya utangulizi yanayohusiana na jina la Sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi yake na tafsiri ya baadhi ya maneno yatakayotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili ambayo inahusisha vifungu namba 4 -13 inahusu uanzishwaji wa mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo, masharti ya kutangaza maeneo ambayo utaratibu wa utambuzi na usajili wa mifugo utakuwa ni lazima. Pia sehemu hii inampa uwezo Waziri kutangaza teknolojia ya kitaifa ambayo itakuwa ni lazima itumike katika maeneo ambayo yatatangazwa kuwa utambuzi wake utakuwa wa lazima. Lakini sehemu hii pia inahusiana na uteuzi wa Mkurugenzi, kazi za Mkurugenzi, madaraka yake, Wakala wa Utambuzi wa Mifugo, ufuatiliaji na kukasimu madaraka. Aidha, sehemu hii inaweka masharti ya matumizi ya vifaa vya utambulisho, umri wa mifugo mbalimbali itakayohusika kutambuliwa, utaratibu wa kutumia vifaa vya utambulisho, uhalali na viwango vya vifaa vya utambulisho, umiliki na utumiaji wa vifaa vya utambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya tatu ambayo inahusisha vifungu vya 14 – 18, inaweka masharti ya kuweka kumbukumbu za usajili wa mifugo. Aidha, sehemu hii inaweka masharti ya kutunza kumbukumbu za mifugo, uanzishwaji wa masijala za Taifa, ufuatiliaji wa kumbukumbu za mifugo na utunzaji wa siri wa kumbukumbu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya nne ambayo inahusisha vifungu namba 19 - 23, inahusu ufuatiliaji wa mifugo. Sehemu hii pia inaweka masharti ya utekelezaji, ufuatiliaji wa mifugo inayochinjwa, inayouzwa, inayoingia na kutoka Tanzania Bara na uendeshwaji wa gwaride la utambuzi wa mifugo. Aidha, sehemu hii inaweka masharti ya kuondoa au kuharibu vifaa vinavyowezesha kutambua mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya tano na ya mwisho, inahusiana na vifungu namba 24 -26, inaweka masuala ya kijumla ikiwa ni pamoja na gharama za uendeshaji mfumo, makosa na adhabu pamoja na mamlaka ya kutunga Kanuni chini ya Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mapendekezo ya Muswada huu ili ujadiliwe na Bunge lako Tukufu na hatimaye kuupitisha kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada mwingine ambao nao nauwasilisha, ninaomba kuwasilisha hoja ya kwamba Muswada wa Kutungwa kwa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula na Mifugo (*The Grazing Land and Animal Feed Resources Bill, 2010),* sasa usomwe kwenye Bunge lako Tukufu pamoja na jedwali la marekebisho *(schedule of amendments)* na marekebisho yote haya yamezingatia maoni ya wadau pamoja na Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoshukuru katika Muswada wa kwanza, naishukuru pia Kamati ya Bunge pamoja na wadau mbalimbali ambao walihusika katika kuboresha Muswada huu. Muswada huu umezingatia pia Sera ya Mifugo pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Lakini hali ya ufugaji wa asili na rasilimali za vyakula vya mifugo hapa kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu wa kutunga Sheria mpya itakayosimamia Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo yenye kukidhi mahitaji ya wakati huu. Hii inatokana na ukweli kwamba Sheria ya Nyanda za Malisho, Na.569 ya Mwaka 1964 ilifutwa na Sheria ya Ardhi, Na.4 bila kuzingatia mahitaji halisi ya ufugaji. Hii inazingatia kuwa mifugo inaongezeka mwaka hadi mwaka, mahitaji ya mifugo na mazao yake nayo yanaongezeka kadri uchumi wa Taifa unavyokua. Kulingana na takwimu zilizopo, nchi yetu ina zaidi ya ng’ombe milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.6, kuku zaidi ya milioni 57. Aidha, nchi yetu ina jumla ya hekta milioni 50 zinazofaa kwa ajili ya ufugaji ambazo zinaweza kutosheleza *unit* milioni 20 za mifugo. Hadi sasa, takriban hekta 1,3391,109 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa Sheria inayosimamia Maendeleo na Utunzaji wa Maeneo ya Malisho, kumesababisha wafugaji kuhama kutoka eneo moja hadi lingine kutafuta malisho na maji na kusababisha migogoro kati yao na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, utengenezaji na matumizi ya vyakula vya mifugo, umekuwa ukifanyika bila utaratibu wa kutosha kwa Wizara, hivyo kupunguza tija katika sekta ya ufugaji kwa sababu kuna baadhi ya vyakula vingine vinatengenezwa kwa ajili ya mifugo ambavyo havifai kwa malisho ya mifugo, lakini pia baadaye vinaleta madhara kwa wananchi. Lakini pia katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji ni machache ukilinganisha na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wakulima na hata maeneo ya wafugaji mengine yamekuwa yakichukuliwa kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo, Sheria hii itasaidia kuondoa migogoro hiyo na kuwapa haki wafugaji ili waweze kufuga kwa lengo la kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa Sheria hii, kunatarajia kuleta matokeo yafuatayo:-

(i) Kuweka utaratibu wa kuendeleza na kulinda maeneo ya malisho ili kuleta tija kwa ufugaji na wafugaji kwa ujumla;

(ii) Kudhibiti ubora wa rasilimali za vyakula vya mifugo;

(iii) Kuhimiza uzalishaji wa mazao kwa ajili ya malighafi za kutengeneza vyakula vya mifugo;

(iv) Kusimamia matumizi ya maeneo ya malisho kwa uwiano wa mifugo, maji, malisho ili kulinda mazingira; na

(v) Kudhibiti vifungashio, ufugaji na uwekaji maelezo ya vyakula vya mifugo *(container packaging and labeling of animal feed resources).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama yafuatayo:-

(i) Kuwepo utaratibu wa kusimamia, kuendeleza matumizi endelevu ya maeneo ya ufugaji na kuelimisha wananchi juu ya misingi ya matumizi endelevu ya maeneo ya malisho na ufugaji bora;

(ii) Kuongeza uzalishaji wenye tija katika maeneo ya malisho kwa kufuga mifugo kulingana na eneo hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira;

(iii) Kuboresha usimamizi na uzalishaji wa rasilimali za vyakula vya mifugo hasa vinavyotengnezwa na viwanda vya hapa nchini na hivyo kuiwezesha Tanzania kushiriki katika Biashara ya Kimataifa ya Mifugo na Bidhaa zinazotokana na Wanyama, kwa sababu kwa sasa hivi Tanzania haifanyi biashara sana ya mazao ya mifugo na hasa baada ya *Tanganyika Packers* kuondoka, pamoja na kwamba tuna mifugo mingi ukilinganisha na nchi zenye mifugo michache kama Botswana ambayo ina ng’ombe milioni 1.8 tu lakini inafanya biashara ya mifugo kuliko Tanzania;

(iv) Kuondoa migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na watumiaji wengine na kudhibiti uhamiaji holela wa mifugo;

(v) Kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mifugo (mashamba na viwanda); na

(vi) Kuweka mgawanyo wa majukumu ya wadau mbalimbali katika kutekeleza Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza, yenye Ibara ya 1 – 3, imeweka masharti ya utangulizi yanayohusiana na jina la sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, matumizi yake na tafsiri ya baadhi ya maneno yatakayotumika katika sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili, Ibara ya 4 – 15, inapendekeza kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Ushauri la Maeneo ya Mifugo na Vyakula vya Mifugo na idadi ya wajumbe. Sehumu hii pia inaweka masharti yanayohusiana na uteuzi wa wajumbe wa Baraza, kazi na uwezo wa Baraza. Aidha, inatoa uwezo wa Serikali za Mitaa kuteua Wakaguzi kwa madhumuni ya kufanya baadhi ya kazi ambazo zimewekwa na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ambayo ni Ibara ya 16 – 20, inahusu uendelezaji, ukuzaji na usimamizi wa maeneo ya malisho ya mifugo, pia inaweka masharti yanayohusiana na mambo muhimu katika uendelezaji wa malisho ya mifugo. Aidha, sehemu hii inaweka zaidi masharti ambayo yanawezesha Baraza la Kijiji kusimamia maeneo ya malisho yanayomilikiwa na kutumiwa na jamii yote katika sehemu husika. Sehemu hii pia inaweka masharti ambayo yanampa uwezo Mkaguzi kuchukua hatua pale inapotokea kuwa mifugo imezidi kiwango katika sehemu inayoruhusiwa kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ambayo ni Ibara ya 21 - 33, inapendekeza kuleta masharti kwa ajili ya kudhibiti uagizaji na uchongaji wa vyakula vya mifugo na uagizaji wa vyakula vya mifugo toka nje ya nchi. Sehemu hii pia inapendekeza kuweka masharti ambayo yanataka maeneo yanayotumika kutengeneza vyakula vya mifugo yasajiliwe. Aidha, inaweka masharti ambayo watengenezaji wa vyakula vya mifugo wanapaswa kuyafuata wanapotengeneza vyakula hivyo, si kuchukua tu mkaa halafu unausaga halafu unasema ni chakula cha mifugo. Lakini pia, sehemu hii inaweka vifungu vinavyokataza kuuza au kusambaza vyakula vya mifugo ambavyo vinasadikiwa kuwa ni hatari kwa mifugo na hivyo kuwa hatari kwa binadamu na hatari pia kwa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sehemu ya Tano ambayo inahusisha Ibara ya 34 – 36, inahusu masuala ya vifungashio na uwekaji wa vibandiko kwenye mifuko ya vyakula vya mifugo. Sehemu hii pia inapendekeza kutungwa kwa vifungu vya sheria vinavyokataza mtu yeyote anayefanya biashara ya vyakula vya mifugo kuuza au kusambaza chakula cha mifugo ambacho kimehifadhiwa ndani ya kifungashio kisichostahili au kifungashio kisicho na vibandiko vyenye majina vinavyoeleweka. Hii itasaidia kupunguza watu kutengeneza vyakula ambavyo ni *fake* ambavyo vinaweza kuleta madhara kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ambayo ni Ibara ya 37 – 43, inaweka masuala ya jumla kuhusu uhifadhi wa maeneo ya malisho, makosa na adhabu zake, mamlaka ya kukamata mtu anayedhaniwa kutenda kosa, mamlaka ya Mahakama kuamuru sampuli za kielelezo kuwasilishwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali au Mkemia

mwingine aliyewahi kuchunguza sampuli husika. Pia inaweka masharti yanayompatia mamlaka Waziri kwa ajili ya kutunga Kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha Miswada hii miwili, sasa kwa heshima, naomba Miswada hii ijadiliwe na baadaye ikiwezekana ipitishwe kwa haraka sana. Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu. Kwa upande wa Kamati, sijaambiwa kama kutakuwa na wawasilishaji wawili, lakini upande wa Kambi ya Upinzani, wawasilishaji watakuwa wawili. Mwenyekiti anayehusika, Mheshimiwa Keenja, ni dakika 15, 15.

**Maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka 2010 *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010)***

**MHE. CHARLES N. KEENJA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji juu ya Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa Mwaka wa 2010 *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010)*. Maoni haya yanawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa mifugo. Inakisiwa kwamba Tanzania ina ng'ombe milioni 19.1 na ni ya tatu katika Bara la Afrika kwa kuwa na ng'ombe wengi na ina mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.6 na kuku milioni 56, pamoja na wingi wake, mchango wa mifugo hii kwa pato la Taifa ni asilimia 4.6. Aidha, wachungaji wameendelea kuishi maisha ya kimaskini na ya tabu na wizi na unyang'anyi wa mifugo, hususan kwenye Mikoa ya mpakani yenye mifugo mingi, umeendelea kushamiri na kusababisha vifo na maisha ya wasiwasi kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni na umuhimu wa Muswada. Muswada huu unakusudia kutunga Sheria mpya ambayo itaweka mfumo madhubuti wa kudhibiti umiliki, uhamishaji wa mifugo na mazao yake kutoka eneo moja kwenda eneo lingine na kwa kufanya hivyo kudhibiti wizi wa mifugo, kuenea kwa magonjwa ya mifugo, uharibifu wa mazingira na migogoro kati ya wafugaji na wakulima. Muswada unakusudia kufanikisha malengo hayo kwa kuweka utaratibu wa kutambua, kusajili na kufuatilia uhamishaji wa mifugo na mazao yake kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Muswada huu, mtu yeyote anayemiliki mifugo, anapaswa kuisajili kwa utaratibu utakaowekwa, isipokuwa kama anakusudia kuichinja katika kipindi kisichozidi wiki moja tangu alipoipata. Mtu anayetaka kuhamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine, atapaswa kutoa taarifa na kupata kibali cha kufanya hivyo kutoka kwa mamlaka inayohusika na atapaswa kufanya hivyo huko anakoihamishia. Mifugo yote itakuwa na alama na vifaa maalum vya kuitambulisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana kwa wafugaji na Taifa kwa jumla. Utaratibu utakaowekwa, utawezesha kujulikana mifugo ilipo wakati wote kutokana na mifugo hiyo kusajiliwa na utaratibu wa kuiwekea alama na vifaa vya utambuzi utawezesha kufuatilia mifugo hiyo ilipo na kwa hiyo kuielekeza ipasavyo. Utaratibu huu utadhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo, tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita ambapo magonjwa, kwa mfano ugonjwa wa mapafu wa ng’ombe, uliweza kuenea nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kupunguza tatizo la uharibifu wa mazingira kwa kudhibiti uhamishaji wa mifugo kiholela hata kati ya vijiji vinavyopakana na mwisho, unakusudia kudhibiti wizi na unyang’anyi wa mifugo jambo ambalo litaongeza usalama wa wafugaji na mifugo yao kwa kufanya hivyo, kulinda rasilimali hii ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulichambuliwa kwa siku tatu katika vikao vilivyofanyika kwenye Ofisi ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam, tarehe 30 na 31 Machi na tarehe 6 Aprili, 2010; kama ifuatavyo:-

· Tarehe 30 Machi, 2010, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliwasilisha Muswada kwa Kamati kwa kutoa maudhui ya Muswada na kuuchambua kifungu kwa kifungu kubainisha maudhui hayo yalivyoshughulikiwa. Wajumbe walipata fursa ya kuhoji vipengele mbalimbali na kupewa ufafanuzi waliohitaji;

· Tarehe 31 Machi, 2010 kilifanyika kikao cha Kamati, Wizara na Wadau wa Sekta ya Mifugo. Mahudhurio ya kikao hicho yalikuwa mazuri sana na wadau walipata nafasi ya kutoa maoni yao juu ya Muswada na walipendekeza mambo ambayo waliona ni vizuri yazingatiwe. Wadau walioshiriki ni wafugaji, wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake, Bodi na Viwanda vya Nyama, Kituo cha Msaada wa Sheria, Kituo cha Kusimamia Haki za Binadamu na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa jumla maoni yaliyotolewa yalikuwa mazuri sana na kwa kiasi kikubwa yaliunga mkono Muswada na kupendekeza maeneo ya kuboreshwa.

Kamati inawashukuru wadau wote walioshiriki kwa maoni yao ambayo yamezingatiwa katika mabadiliko ya Muswada na mengine yatazingatiwa katika Kanuni zitakazotayarishwa chini ya Sheria; na

- Tarehe 6 Aprili, 2010 kilifanyika kikao kati ya Kamati na Wizara. Kikao hicho kilipitia maoni ya wadau na maelezo ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi aliyotoa katika vikao vya terehe 30 na 31 Machi, 2010 na kuupitia Muswada kwa umakini kifungu kwa kifungu. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kiwango kikubwa, maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa katika mabadiliko ya Muswada yaliyowasilishwa hapa Bungeni na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaridhika kwamba Muswada huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta ya mifugo na Taifa kwa jumla. Ni maoni ya Kamati kwamba, Muswada huu umechelewa sana kufikishwa Bungeni na kwamba kama ungekuwa umewasilishwa mapema zaidi, matatizo mengi yaliyoikumba sekta hii yangeepukwa na athari zake zingepungua sana. Hata hivyo, Waswahili wanasema “chelewa ufike”. Tunaipongeza Wizara na Serikali kwa jumla kwa kuandaa na kuwasilisha Muswada huu Bungeni. Maoni na mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

- Muswada huu unawahusu wafugaji/wachungaji na mifugo yao. Ni muhimu sana kwa Wizara kuweka utaratibu ambao utawezesha yaliyomo kwenye Muswada huu kuwafikia walengwa. Kamati inasisitiza kwamba ni muhimu kwa wafugaji kuwezeshwa kuunda Vyama vyao ambavyo vitawaunganisha, kuwapa misaada mbalimbali, kuwashirikisha na kuwapa sauti katika mambo yanayohusu sekta yao. Waziri aliahidi kuzingatia pendekezo hili katika Kanuni zikazotungwa chini ya sheria itakayotokana na Muswada huu;

- Kamati inapendekeza kwamba, sheria hizi ambazo zinahusu maisha na shughuli za kila siku za wananchi, zitafsiriwe katika Kiswahili mapema iwezekanavyo na ihakikishwe kwamba wananchi wanazipata kwa urahisi;

- Muswada unatoa majukumu muhimu ya utekelezaji kwa Halmashauri za Wilaya na Miji. Ni muhimu sana Wizara ichukue hatua za kukutana na Mamlaka zinazohusika kufafanua majukumu hayo na utaratibu utakaotumika kuyagharamia;

- Jeshi la Polisi ni mdau muhimu sana katika Muswada huu hususan kuhusiana na utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo mipakani na hata ndani ya nchi, uwekwe utaratibu wa kuwashirikisha;

- Muswada huu unatamka kwamba majukumu ya kuanzisha na kuweka utaratibu wa kutambua, kusajili na kufuatilia mifugo utagharamiwa na Serikali. Kamati inapongeza uamuzi huu na inatahadharisha Wizara iepuke kuwatwisha wananchi mzigo wa gharama ambazo sio muhimu kwao. Kwa mfano, wafugaji wanaweza kuona umuhimu wa kugharamia uwekaji wa alama na vifaa vya utambuzi kwa mifugo yao lakini wasione umuhimu huo kwa huduma nyingine; na

· Mwisho baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa sheria, Wizara ichukue hatua za haraka kuandaa watendaji watakaosimamia utekelezaji wake, vifaa vitakavyohitajika na mazingira mengine yote yatakayowezesha utekelezaji kuanza mapema. Aidha, kanuni zinazokusudiwa kuandaliwa, ziandaliwe mapema kwa Kiswahili na kusambazwa kwa wadau wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaridhika kwamba Muswada huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya mifugo katika nchi yetu. Maoni na ushauri wa Kamati na Wadau wa Sekta ya Mifugo, yamezingatiwa katika mabadiliko yaliyowasilishwa na Muswada huu hapa Bungeni leo. Kamati yangu, kwa hiyo, inaunga mkono Muswada huu na inalishauri Bunge lako Tukufu lijadili na kuupitisha ili Taifa na wananchi wapate manufaa yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuchambua Muswada huu na kwa ushirikiano wao katika kuandaa Taarifa hii. Napenda kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti na Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Charles N. Keenja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. James Wanyancha, Katibu Mkuu, Dkt. Charles Nyamrunda, pamoja na watendaji wengine wa Wizara, kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri kwa Kamati. Kamati inawashukuru Maofisa kutoka kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa msaada wao wa kisheria walioutoa katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Aidha, Kamati inawashukuru wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu kwani yamesaidia katika kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi, kwa kuihudumia Kamati kwa ufanisi wakati wote na kuandaa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, lijadili na likubali kuupitisha Muswada huu ili baadaye tupate Sheria ya kusimamia masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa kuwa sikupewa majina, naona anayekuja labda huyo huyo, Mheshimiwa Hilda Ngoye, kwa niaba ya Mwenyekiti. *(Kicheko)*

**Maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo wa Mwaka wa 2010**
***(The Grazing Land and Animal Feeds Resources Bill, 2010)***

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo *(The Grazing Land and Animal Feeds Resources Bill, 2010).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka na kusababisha kuongezeka kwa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, kumekuwepo na taarifa kwamba baadhi ya vyakula vya mifugo vimekuwa vikichanganywa na madawa mbalimbali yenye athari kwa mifugo pamoja na watumiaji wa bidhaa za mifugo. Baadhi ya madawa hayo yamekuwa yakitumika kwa lengo la kukuza mifugo hiyo kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaridhika kwamba Muswada huu ni muhimu sana kwa ustawi wa mifugo, matumizi bora ya ardhi na usalama wa watumiaji wa mazao yanayotokana na mifugo hivyo umeletwa kwa wakati muafaka kwani utawezesha usimamizi bora wa malisho na vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada, Muswada huu wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo wa Mwaka wa 2010, unakusudia kuweka mfumo wa kisheria wa kusimamia na kudhibiti maeneo ya malisho ya mifugo na biashara ya vyakula vya mifugo kwa lengo la kulinda usalama wa mifugo na afya ya mifugo na binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika,kutungwa kwa sheria hii kutaweka utaratibu wa kuendeleza na kulinda maeneo ya malisho, kudhibiti ubora wa rasilimali za vyakula vya mifugo, kuhimiza uzalishaji wa mazao kwa ajili ya malighafi za kutengeneza vyakula vya mifugo, kusimamia matumizi ya maeneo ya malisho ili kulinda mazingira na kudhibiti vifungashio na maelezo ya vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Muswada, Kamati ilipata nafasi ya kujadili Muswada huu katika vikao vitatu vilivyofanyika kwenye Ofisi ndogo ya Bunge ya Dar es salaam. Kikao cha kwanza kilifanyika tarehe 30 Machi, 2010, ambapo Waziri

wa Maendeleo ya Mifugo alitoa maelezo ya jumla juu ya madhumuni ya Muswada na yaliyomo kwenye vipengele vyake. Kikao cha pili kilifanyika tarehe 31 Machi, 2010 na kiliwashirikisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo. Baadhi ya Wadau walioshiriki ni Wafugaji, Wachinjaji, Bodi na Viwanda vya Nyama, Kituo cha Msaada wa Sheria, Kituo cha Kusimamia Haki za Binadamu na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kamati inawashukuru wadau wote walioshiriki kwani wametoa maoni ya msingi na muhimu ambayo yamezingatiwa katika mabadiliko ya Muswada na mengine yatazingatiwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii. Kikao cha tatu ambacho kilifanyika tarehe 6 Aprili, 2010, Kamati ilizingatia michango ya wadau pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Waziri na kupitia rasimu ya Mabadiliko ya Muswada yaliyoandaliwa na Wanasheria pamoja na wataalam wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Tunaipongeza na kuishukuru Wizara kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na Wadau na kuzingatia katika mabadiliko yaliyokwishawasilishwa na Mheshimiwa Waziri ili kuboresha utekelezaji wake. Aidha, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(a) Baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa Sheria, Serikali ihakikishe inatengeneza Kanuni mapema iwezekanavyo ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa Sheria kwa mamlaka zote zinazohusika;

(b) Serikali ianzishe mtandao unaowakilisha maslahi ya wafugaji katika utekelezaji wa Sheria hii kwa kuwa na Mabaraza Rasmi ya Wafugaji ambayo yatakuwa yakipokea maoni na ushauri wa wafugaji kuhusu utekelezaji bora wa Sheria hii na kuyawasilisha maoni na ushauri huu kwa Serikali;

(c) Utekelezaji wa Sheria hii uzingatie mabadiliko ya hali ya hewa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi (*climatic change*) ambayo imesababisha ukame wa mara kwa mara na hivyo kulazimisha wafugaji kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kwa ajili ya kutafuta malisho;

(d) Serikali ifanye maandalizi ya kutambua maafa mapema (*early warning*) ikiwemo ukame na magonjwa ya mifugo na kufanya maandalizi mapema kabla hayajaleta athari kwa mifugo na wafugaji kwani kwa kufanya hivyo Serikali inaweza kuratibu uhamishaji wa mifugo kwa ajili ya kufuata maeneo yenye malisho badala ya mifugo kuhamishwa kwa dharura kama inavyofanyika sasa;

(e) Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na wadau wengine ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na *NEMC* ili kuzuia utengenezaji na uagizaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kwani mifuko hii ina athari kubwa kwa mifugo kwa kuwa wanyama wakila mifuko ya aina hii wanakufa;

(f) Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ya mara kwa mara ambayo ni pamoja na ukame, ni vema wakulima wahamasishwe kutumia vyakula vingine vya

mifugo ikiwemo vyakula vinavyotengenezwa viwandani badala ya kutegemea malisho peke yake. Aidha, wafugaji waelimishwe umuhimu wa kukata nyasi wakati wa masika na kuzihifadhi kwa ajili ya kulishia mifugo wakati wa kiangazi. Vyakula vya ziada pia vitapunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji kwani mifugo inaweza kulishwa ikiwa sehemu moja bila kulazimika kuhamia maeneo mengine;

(g) Ili Sheria hii iweze kutekelezeka, ni muhimu kutoa elimu kwa wafugaji na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuwawezesha kuielewa na kuitekeleza. Aidha, mamlaka zote zinazohusika na sheria hizo ziwe na mfumo wa kushirikiana katika utekelezaji;

(h) Kwa kuwa kuna Sheria nyingi zinazotekelezwa pamoja na Sheria hii ni vema Sheria hizo zikaandaliwa na kusambazwa kwa wadau pamoja na Sheria hii;

(i) Serikali ifanye maandalizi yote muhimu ikiwemo kutenga fedha za kutosha kusimamia utekelezaji wa Sheria hii;

(j) Kwa kuwa utekelezaji wa Sheria hii utahusisha pia Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni vema uanzishwe mfumo rasmi kwenye mamlaka hizo utakaosimamia utekelezaji wa Sheria hii;

(k) Ili kusimamia ubora wa malisho, Serikali ihakikishe kuwa inaajiri wataalam wa kutosha na wenye sifa zinazohitajika ambao pia watatoa elimu kwa wafugaji kwa masuala yote yanayohusu malisho bora. Aidha, wataalam hawa wafuatilie na kufanyia utafiti, ujuzi na uzoefu walionao wafugaji kwa masuala yanayohusu malisho na vyakula vya mifugo; na

(l) Utaratibu ufanywe ili kuhakikisha kuwa Sheria hii inatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili wafugaji waweze kuielewa na kuitumia badala ya kuendelea kuwa katika lugha ya Kiingereza ambayo haifahamiki na wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano wakati wa kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Napenda kuwatambua kwa kuwataja majina wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Kheri K. Ameir, MheshimiwaTeddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omar, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Benson M. Mpesya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati na kushiriki kikamilifu katika kuwasilisha maoni na mapendekezo yao ambayo yamesaidia sana katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Mawndeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mb, Naibu Waziri, Dkt. James Mnanka Wanyancha, Mb, Katibu Mkuu, Dkt. Charles Nyamrunda, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashilillah, kwa kuiongoza Ofisi ya Bunge na kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha taarifa hii kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Pamela E. Pallangyo na Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi, kwa kuihudumia Kamati vizuri wakati wote na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika,naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba nikushukuru kwa namna ya pekee kwa sababu hukunilazimisha kuongeza muda. Kwa hiyo, tumemaliza kama tulivyopanga.

Waheshimiwa Wabunge, upande wa Maoni ya Kambi ya Upinzanim watakuja baadaye saa 11.00 jioni. Naelewa ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Waziri Kivuli wa Wizara hiyo na Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Halafu wachangiaji wengine, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa George Simbachawene wajiandae na wengine watafuata. *(Makofi)*

Kwa kuwa saa ya kuahirisha Kikao kwa mchana huu imefika, napenda kusitisha shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana tulikuwa tumewasikiliza watoa hoja halafu tukasikiliza Kamati iliyoshughulikia Miswaada hii na sasa tunaingia Kambi ya Upinzani, nao pia wako wawili. Kila mtu

atatumia dakika 15, ataanza Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha ambaye ni Waziri Kivuli wa Wizara hii. Karibu Mheshimiwa Jecha.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa Afya njema na kuniwezesha pamoja na mambo mengine kutekeleza majukumu yangu ya hapa Bungeni. Aidha, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa mwaka 2010 kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui na dhana nzima ya Muswada huu ni kujaribu kudhibiti matatizo makubwa ambayo yamekuwa yakizikabili jamii za wafugaji hapa nchini. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Dr. John P. Magufuli, Naibu Waziri - Mheshimiwa James Wanyancha, pamoja na timu nzima ya watendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa mfumo mzima wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo una faida nyingi kwa nchi pamoja na kwa wafugaji wenyewe. Miongoni mwa faida hizo ni pale unapoibuka ugonjwa wa mifugo inakuwa ni rahisi sana kukabiliana nao kwa kuwa itakuwa rahisi kujulikana umetokea wapi. Pili, urahisi wa kufuatilia mfugo toka anapozaliwa hadi anapochinjwa au kufa na hii inatoa urahisi katika suala zima la tafiti zitakazoweza kufanyika kuhusiana na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo unakwenda sambamba na tasnia ya uzalishaji wa nyama ambayo hivi sasa imekuwa na masharti mengi sana ili kuweza kupata soko la uhakika toka nchi zilizoendelea. Hivyo basi, zoezi zima la hitaji ya Muswada huu wa Sheria inatakiwa elimu ya kutosha itolewe kwa wafugaji wa asili ili kuweza kubaini faida za wazi watakazozipata wafugaji hao. Aidha, katika utekelezaji wa zoezi hili, ni lazima busara zitumike kuliko kutumia nguvu kama vile *operation* hamisha wafugaji ilivyofanyika.

Kadhalika, tunashauri kwamba usajili unapofanyika, basi zitumike *"codes"* maalum ambazo zitaonyesha nchi, mnyama alipo, Mkoa, Wilaya na namba halisi ya mnyama wenyewe. Tukifanya hivi utambuzi wa wanyama utakuwa rahisi kudhibiti nyendo na wizi wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, Kambi ya Upinzani haina tatizo na dhana inayobebwa na Sheria hii. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inatoa tahadhari kubwa kuwa kuna vipengele ambavyo visipoangaliwa upya na kuwekwa vizuri vitakuwa msingi wa kero kubwa sana kwa wengi wa wafugaji na hasa wachungaji kutokana na kutokuangalia uhalisia wa hali ya ufugaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuangalia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinaweza kuleta ugumu kiutekelezaji, naomba tujikumbushe ile tafsiri aliyoitoa

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete inayotofautisha kati ya wafugaji na wachungaji. Dhana iliyopelekea Mheshimiwa Rais kutoa tafsiri hiyo ni dhana hiyo hiyo ambayo imetushawishi sisi kuona kuwa utambuzi na usajili wa mifugo unaweza kuleta matatizo makubwa kuliko hata ambayo yanaendelea hivi sasa katika jamii za wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, walengwa wakubwa wa Muswada huu ni wachungaji na sio wafugaji. Katika hali halisi ni kwamba hao ni watu ambao wanahamahama na mifugo yao kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa lengo la kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Pili, wengi wa wachungaji ni watu ambao hawana nyumba maalum za kulaza mifugo yao kama inavyotakiwa na kifungu cha 6(i) kinachotaka wafugaji wasajili pia makazi yao. Hivyo basi, Sheria hii ikipita, tusipokuwa makini itawaweka wachungaji wengi sana Magerezani hatimaye ni kuzidisha umasikini katika familia husika iwapo itatumika vibaya. Kambi ya Upinzani inadhani, ni muhimu sana sheria/kanuni zinapotungwa, mazingira na hali halisi ya Watanzania yawe yamezingatiwa. Sheria inayogeuka kuwa kero inapoteza hadhi na inakuwa Sheria mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inachelea kusema kuwa upembuzi yakinifu *(feasibility study)* haukufanyika kwa kina sana kabla ya uandaaji wa Muswada huu, kwani kulingana na hali halisi ya wachungaji wa Tanzania ambao siku zote wanachunga kutegemea ni wapi wanapata malisho na maji na hivyo kusafiri mwezi mzima au zaidi kutoka Wilaya moja hadi nyingine au Mkoa na Mkoa, vipengele hivi vya Sheria hii vinaweza kutekelezeka lakini kwa maumivu makubwa sana kwa wafugaji/wachungaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalan, Kifungu cha 6(4) kinamtaka mtu akipata mfugo ndani ya siku saba asajili mfugo wake huo. Jukumu hili linaweza kuwa vigumu kutekelezeka kwa wachungaji hasa wa maeneo kama ya Kiteto, Simanjiro na sehemu nyingine za Wilaya za Monduli, Wilaya za Ngorongoro na Wilaya ya Hanang, ambako hata umbali kutoka kijiji kwenda kijiji ni zaidi ya kilomita 100 katika maeneo mengi. Hivyo basi, inawia vigumu kumtaka mchungaji huyo asafiri kwenda kwenye eneo la usajili kwa sababu tu ya kujisajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani kuna haja ya kutengeneza Sheria bora, lakini pia yenye kujali mazingira maalum wanakoishi wananchi wetu. Aidha, sheria itakayotungwa itatekelezeka kama kila mfugaji wa asili atatengewa na kumilikishwa eneo lake na kuliboresha kwa kuweka huduma za maji na malisho bila kuwepo na mwingiliano baina ya mfugaji na mfugaji. Kinyume na hapo, Sheria hizi zitashindwa kutekelezeka. Serikali ikitimiza wajibu wake wa kutoa huduma muhimu, hata wachungaji wataacha kuhamahama. Wanahamahama kwa sababu ya shida, tukiwaondolea shida, nao pia watapenda kukaa eneo moja.

Katika kifungu cha tano cha Muswada kinachosema kuwa Mheshimiwa Waziri atatoa tamko la utambuzi na usajili wa lazima kwa mifugo katika maeneo tajwa; kwa kuwa wafugaji wa nchi hii wengi ni wale wa kuhamahama pindi itakapotokea kuwa

tamko limetolewa na wao hawapo katika eneo lao la asili: Je, watakuwa wamevunja Sheria? Suala hili ni la kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Botswana ambayo ndiyo mfano wa kuigwa kuhusiana na Sekta ya Mifugo, hutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa. Wao mpango kama huu ambao tunaoutungia Sheria leo hii, ulianza kama mradi tu *(pilot project)* mwaka 1999 na mwaka 2001 ukawa kwa nchi nzima, lakini ulifanyika kwa ngombe tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hao wenzetu hawajaufanya mpango huu kuwa wa kitaifa, ulifanyika upembuzi yakinifu wa kina na kwa kuwashirikisha wadau na washauri mbalimbali kuhusu njia muafaka ya kuweza kuwa na utaratibu mzuri wa utambuzi wa mifugo ambao hautaingiliana na taratibu za nchi nyingine na hivyo kuwa wa kipekee kwa nchi hiyo. Sio vibaya kwa nchi yetu kuchota uzoefu kutoka Botswana ambao wamepiga hatua nzuri katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5(2) kinachosema kuwa, nanukuu *"the livestock identification or registration of premises and livestock establishments in which livestock are kept shall be mandatory within the areas declared by the Minister",* Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa wale ambao tunawaita wafugaji katika nchi hii, ambao kwa sehemu kubwa mifugo yao haiwekwi kwenye jengo maalum, bali inakusanywa sehemu moja ili usiku upite na kesho inakusanywa sehemu nyingine kwa kutegemea na usiku umeingia wakiwa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo hali halisi ya wafugaji wenye mifugo mingi. Hivyo basi, ulazima wa kusajili majengo au nyumba za kulaza mifugo utabaki kuwa wa wafugaji wenye maeneo ya kudumu yaliyoimarishwa kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara. Tuna wasiwasi kuna hatari kwa wafugaji wa kuhamahama wakaachwa nje ya mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri ipo haja kwa Bunge kuitanabaisha Serikali katika utungaji wa Kanuni zitakazosimamia utekelezaji wa Sheria hii. Suala hili limewekewa mfumo madhubuti utaowashirikisha wafugaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 24(2) cha Muswada kinachosema kuwa gharama za uendeshaji wa mfumo huo zinaweza kubebwa, *may be borne by,* na Serikali, wadau na wale watakaonufaika na mfumo huo moja kwa moja au sio moja kwa moja kwa kugawana gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Kambi ya Upinzani inaona kuwa hili litaleta matatizo kwani wafugaji wa asili haitakuwa rahisi kuchangia kutokana na wao kuwa tayari na utambuzi wao wa kiasili ambao unaendana na mila na tamaduni zao. Aidha, kwa kuwa mfumo huu ni matakwa ya Serikali na ili kujenga imani kwa wafugaji, haina budi Serikali kubeba mzigo wa gharama zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama tulivyosema hapo awali, Kambi ya Upinzani haina pingamizi juu ya upitishwaji wa Muswada wa Sheria hii kutokana na faida kubwa zitakazopatikana kuanzia kwa wafugaji wenyewe, wadau wengine na nchi kwa ujumla. Ingawa tunaweka angalizo juu ya njia bora na busara katika mchakato mzima katika utekelezaji wa Sheria hii, angalizo hili ni pamoja na kuchukua tahadhari kubwa ili Sheria hii isiwe ni chanzo cha kero kwa wananchi wetu badala ya kuwaletea manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Ali khamis Seif kwa niaba ya Waziri Kivuli awasilishe sehemu nyingine.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF - (K.N.Y MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudia tena kutoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Dr. John P. Magufuli, Naibu Waziri - Dr. James Wanyancha pamoja na timu nzima ya Watendaji wa Wizara yake kwa hatua wanazozifanya katika kuhakikisha kuwa tasnia nzima ya mifugo inaleta manufaa kwa wafugaji wenyewe na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama sitatambua mchango na msaada mkubwa wa Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa katika matayarisho ya hotuba zote za Kambi kuwa katika viwango. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano walionipatia katika mchakato mzima wa maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulio mbele yetu ni mzuri kwa maendeleo ya tasnia nzima ya mifugo, japokuwa kuna mambo kadhaa ambayo Kambi ya Upinzani inaona ni ya msingi, lakini yamesahaulika au sheria haikuyapa kipaumbele japokuwa ni ya muhimu kwa maendeleo ya sekta nzima ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa, kadri siku zinavyokwenda mbele ndivyo idadi ya watu inavyoongezeka na ndivyo maeneo ya malisho ya mifugo *(grazing-land)* yanavyozidi kupungua kutokana na shughuli za kibinadamu. Aidha, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya mifugo, uharibifu wa mazingira unaosababishwa na mlundikano wa mifugo katika eneo dogo, nao umekuwa ukiongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuinua kiwango cha malisho ya mifugo kwa wafugaji wa asili na wale wafugaji wa kibiashara, uanzishwaji wa mashamba ya malisho *(pasture farms)* ni muhimu sana. Mashamba haya yanaweza kuanzishwa na wafugaji wenyewe au mtu yeyote kwa lengo la kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tafsiri ya maneno hauonyeshi maneno '*pastures*' au '*pasture farms*' pia '*pastoralists'*, lakini katika uanzishwaji wa Baraza la Taifa la maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo inaonesha kuwa mjumbe mmoja atatoka katika jumuiya ya wafugaji na wakulima wafugaji *(one member from national pastoral and agro-pastoral organization).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria, hatujaona kifungu kinachozungumzia jinsi ya kudhibiti ubora wa malisho ya majani makavu *(hay)* yanayouzwa maeneo mengi ya mijini. Hili ni suala muhimu sana kutokana na hali halisi ya ufugaji wa mijini na sio mijini tu, bali kutokana na mabadiliko ya majira ya mwaka ambayo kipindi cha ukame kinakuwa kirefu zaidi na hivyo kusababisha mifugo kukosa majani mabichi *(green pastures).*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Muswada hauongelei lolote kuhusiana na chakula cha mifugo (mashudu) kinachotoka katika viwanda vinavyotengeneza bidhaa tofauti, kama mafuta ya kupikia kutokana na alizeti, pia na bidhaa zitokanazo na mazao jamii ya kunde kwa ujumla wake *(Agro-industry by products).* Sio hilo tu, mtu anayesaga unga, pumba ambayo ni *"by- product"* katika mchakato wa ukoboaji wa mahindi: Je, wahusika wa viwanda hivyo pale watakapouza *"by- products"* hizo kwa wafugaji Sheria inasemaje kwa wanaouza na kununua kwa ajili ya mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 kinacholitaka baraza la kijiji kutenga sehemu ya ardhi ya kijiji kuwa eneo mkakati kwa ajili ya malisho. Kifungu hiki kinawezekana kabisa kama wafugaji wanaozungumziwa ni wale wa kibiashara na sio wafugaji wa asili. Sheria inalitaka Baraza la Kijiji kutenga ardhi, lakini: Je, Wizara imefanya utafiti na kufahamu kama Vijiji bado vina ardhi kiasi gani kinachoweza kutengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rahisi kumtengenezea mtu sheria, lakini utekelezaji usiwepo kwa kuwa vijiji vingi tayari vina migogoro ya ardhi kutokana na upungufu wa ardhi. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inadhani kutoa maagizo tu kwa njia ya Sheria sio suluhisho wala mkakati mzuri wa kuepusha migogoro kabla utafiti wa kina haujafanyika.

Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha, alieleze Bunge lako Tukufu, Vijiji vyetu vina jumla ya ekari ngapi ambazo zinaweza kutengwa kwa mujibu wa Sheria hii ili kuondoa utata huko tuendako? Iwapo Utafiti huu haujafanyika: Je, Serikali haioni kuwa hii ni njia moja ya kuhamisha tu lawama kutoka Serikali Kuu kwenda kwa Mabaraza ya Vijiji, jambo ambalo hatimaye litazua mgogoro mkubwa kwa kuwa Sheria hii inawezekana kabisa katika baadhi ya vijiji isiweze kutekelezwa kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali yenyewe kupitia kwa Ofisi ya Kamishna wa ardhi inayo ekari ngapi ambayo ipo chini ya mamlaka ya Serikali Kuu? Inaweza kutengwa na Serikali Kuu yenyewe kuepuka migogoro? Je, ni kwa kiwango gani Sheria hii imehuishwa na matakwa ya Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 ya Ardhi ya mwaka 1999? Waziri alihakikishie Bunge hili kuwa halitungi sheria ambayo inagongana na Sheria nyingine zilizotungwa na Bunge hili Tukufu. Wafugaji wa asili ambao ndio asilimia

kubwa ya wafugaji tulionao kwani katika idadi ya ng'ombe takribani million 19.1 asilimia zaidi ya 85% inamilikiwa na wafugaji hao, ufugaji wao unaendana zaidi na majira ya mwaka, hivyo kutenga eneo moja kwa ajili yao bila ya kuweka miundombinu ya kutosheleza mifugo yao, ni jambo lisilowezekana kabisa katika hali halisi.

Kifungu cha 18 kinazungumzia uendelezaji wa maeneo ya malisho. Ni jambo zuri la kuendeleza maeneo ya malisho ili kuwa endelevu. Jambo hili lingewezekana ikiwa kila mfugaji awe wa asili au wa kibiashara anamilikishwa eneo lake na analiwekea miundombinu yote inayohitajika kwa maendeleo ya mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji kuelewa ni nani atahusika na gharama za uendelezaji wa eneo hilo la malisho? Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha alifafanulie Bunge hili jukumu hili muhimu kwani sifa ya Sheria nzuri ni uwezo wake wa kutekelezeka, na nani hasa anayewajibika kutekeleza majukumu yanayowekwa na sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20(1) na (2) kinachosema kuwa kama mkaguzi atajiridhisha kuwa kuna mifugo imezidi katika eneo la malisho anaweza kuamuru idadi ya mifugo inayozidi kuondolewa katika eneo husika. Aidha, Mkaguzi anaweza kuomba Mahakama kutoa amri kwa yeyote atakayeshindwa kutekeleza amri yake kwa njia ya kuuza mifugo husika, na gharama za kutekeleza zoezi hilo kwa amri ya Mahakama zitakuwa ni za mfugaji baada ya kuuza mifugo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani kuwa kifungu hiki ni msingi wa matatizo makubwa siku zijazo. Kwanza kabisa, kipengele hiki kinakwenda kinyume kabisa na dhana ya Sera inayotekelezwa katika nchi yetu, yaani dhana ya biashara huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni kwanini mfugaji peke yake alazimishwe, tena kupitia Mahakama kuuza mifugo yake? Je, iwapo mfugaji atalazimishwa kwa amri ya Mahakama kuuza mifugo yake wakati bei ya mifugo ipo chini Kama inavyotokea mara nyingi, Serikali haioni kuwa huu ni ubaguzi, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano? Kwani ni wafugaji tu ndio wanalazimishwa kuuza mali yao wakati wengine wote, mathalan wakulima wako huru kuuza mazao yao wakati wowote anapoamua na kwa mtu yeyote wanayemtaka. Kwanini kwa mfugaji tunaweka kifungu hiki wakati wote tunajua kabisa kuwa kifungu hiki pia kinaweza kutumika vibaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alihakikishie Bunge hili wakati wa kuhitimisha kwamba Serikali inaeleza nini kuhusu ubaguzi huu wa mfugaji? Tukumbuke kuwa hata sasa wafugaji walikwishajeruhiwa na matukio mbalimbali ya kuondolewa kwa nguvu katika maeneo yao na Serikali ndani ya Bunge hili ilitoa tamko zito la kuchukua hatua ya kulinda haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo hakuna hatua yoyote inayojulikana kuchukuliwa labda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni hatua zipi zimechukuliwa baada ya ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyosomwa ndani ya Bunge hili Tukufu na Watanzania wote wakaisikia. Ni vyema taarifa ya Utekelezaji wa ahadi ile pia ukatolewa

kupitia Bunge hili Watanzania waweze kuelewa ni vipi haki zao zinalindwa na Bunge hili Tukufu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kitaleta mvurugano mkubwa kati ya wafugaji na Serikali na kukumbusha machungu ya zoezi lililopita la kuhamisha wafugaji kutoka katika baadhi ya maeneo kwa nguvu. Hivyo, inaitaka Serikali kuangalia upya kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo tunaona yanatakiwa kuangaliwa kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mawasilisho ya Kamati ya Bunge iliyohusika na maoni ya Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, tunaendelea na Waheshimiwa Wabunge kujadili Muswada huu. Kwa bahati nzuri tutaendelea nayo kesho. Kwanza kabisa nitamwita Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Mbene na Mheshimiwa Estherina Kilasi, ajiandae.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na kama mlivyoshauri, nitasema mambo kiasi kuhusu ule Muswada wa *Identification* na baadaye Muswada wa Malisho. Kabla sijasema hayo, nilikuwa nataka niseme mambo ya jumla. La kwanza, naipongeza Serikali na hususan Waziri mwenyewe, ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Magufuli, Naibu Waziri na wataalamu wote kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Mimi sisemi umechelewa, umekuja wakati wenyewe kwa sababu kila kitu na wakati wake. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa uamuzi wa kuleta Muswada huu. Nina hakika kama ukitumika vizuri na kama baadhi ya maeneo fulani yakirekebishwa Muswada huu unaweza kuleta mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la jumla ninashauri Serikali tufanye kazi ya ziada ya kutoa elimu kwa wafugaji kwa sababu huu Muswada ni Muswada unaohusu watu wengi katika nchi yetu. Tusipowaelimisha, watagandamizwa. Kule vijijini wako Miiungu watu kule kwenye Serikali za Vijiji wataumiza sana wafugaji. Kwa hiyo, lazima elimu ifanyike ya ziada kuelimisha waelewe sheria hii. La tatu, ninapendekeza kuwa Serikali yenyewe iweze kutambua maeneo yatakayokuwa ya kitaifa ambayo yanaweza kutumika kwa ajili ya ufugaji na maeneo kwa ajili ya kilimo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo kusema maeneo ya ufugaji lazima yatengenezewe miundombinu ili iwe rahisi kwa wafugaji kuingia. Isitokee tena baada ya Sheria hii wafugaji kuswagwa na kusema nendeni mtoke katika eneo. Ukiwatoa, waende wapi? Kwa hiyo, lazima kuwe na mipangilio mizuri ya mahali watakapokwenda. Vile vile, kuna watu wanapenda kuwekeza katika ufugaji na kilimo. Kwa sasa hivi mtu anayekuja kuwekeza Tanzania hawezi kufaulu kwa sababu wakija watakwenda vijijini na wakienda vijijini au Mikoani hakuna ardhi ya wawekezaji wakubwa. Kwa hiyo, kama tunataka wawekezaji wakubwa waje nchini, lazima kuwe na maeneo ambayo Mikoa na Serikali Kuu tumekubaliana kuwa wakija hawa hawatawabugudhi wanakijiji, watakwenda kwenye maeneo ambayo yametambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda niende moja kwa moja kwenye Muswada. Nitaanza na Muswada ule uliotangulia.

**NAIBU SPIKA:** Utaje kwa jina Bwana.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada uliotangulia ambao ni *Livestock Identification, Registration and Treceability Act*, 2010. Kifungu cha tisa kinazungumzia habari ya Serikali au mamlaka ya Serikali kuwashirikisha pamoja na *Private Sector.* Sasa kwa kuwa katika utangulizi wa Muswada haikuelezwa *Private Sector* ni ipi inayozungumziwa, ningependa Waziri atueleze hapa *Private Sector* inayosemwa ni ipi? Maana *Private Sector* ni *too General*, inaweza kuwa ya Kilimo, inaweza kuwa ya ufugaji, inaweza kuwa ya viwanda; sasa tuelewe *private sector* inayosemwa hapa ni ipi ili ikifika wakati huo, wale waohusika kuwashirikisha *Private Sector* wasibabaike?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tisa, ukurasa wa tisa unazungumzia habari ya *Traceability Officer.* Sasa mimi naona pia hapa imewekwa siyo sawa kwasababu lazima kuwe na mtu ambaye anasemwa hapa. Hatuwezi kusema tu *Traceability Officer!* Mimi napendekeza kwamba mtu huyu awe ni yule ambaye amesajiliwa na *Director,* anajulikana kabisa ili ikitokea matatizo, anajulikana ni nani. Hapa imekuwa ni jumla mno.

Kifungu cha tisa hicho hicho, Na. 2 inasema hivi: "*The livestock* owner *shall with assistance of the livestock Identification and Treacesibility Agent and under the supervision of so and so* mimi nafikiri lile neno *Agent and* lifutwe badala yake yabakie maneno: "*Identification and Traceability under the supervision of so and so*." Lile neno *Agent* lifutwe kwa sababu ni *Agent* gani huyu? Maana jambo hili linahusiana na kazi ambayo ni *professional,* sasa *Agent* huyu ni *Agent* gani? Maana kule kwenye tafsiri ya Muswada hatujaona kifungu kinachotafsiri *Agent* atakuwa ni nani. Kwa hiyo, naomba Waziri akubali kufanya marekebisho hapa. Kama wenyewe wataona haitafaa, mimi nitaleta marekebisho wakati wa kuwasilisha Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kifungu cha 10 sehemu ile baada ya 'J' na 'H' mimi nilikuwa napendekeza vile vile kwamba kuwepo na kifungu ambacho Mkurugenzi au *Director* atakaimu madaraka yake kwa mtaalamu wa *Veterinary Officer* ambaye atakuwa ametambuliwa katika Wilaya husika ili kurahisisha utendaji. Halafu kifungu cha 12 kinazungumzia vilevile habari ya *Traceability Officer.* Mimi naona hapa pia ni tatizo kwa sababu tunataka tujue sifa, itajwe sifa ya mtu huyu kwamba atakuwa na sifa gani, tuwe na uhakika kuwa kazi itafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo Kwa kifungu cha tatu pale chini, pia naomba *Officer* huyu atajwe na sifa zake kwa sababu jambo hili tunalolizungumzia ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 12(4) inazungumzia habari ya uwezo, kinasema: "*A Local Government authority shall within its area of the duration appoint from among its employees a private livestock extension officer and livestock identification registration and identification officer.*" Hapa mimi nina wasiwasi,

ninapendekeza kwamba *Director* anayetajwa katika sheria hii kwa kushirikiana na Halmashauri, wateue huyo Afisa, tusiiache wazi hii ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake mnaposema *local authority* wateue, wanamteua mwenye sifa gani? Maana hatuoni sifa hapa isipokuwa tu kama tutathibitishiwa na Waziri kwamba wao kwenye *regulations* wataeleza aina ya sifa ya mtu atakayechaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13, hapa inazungumzia habari ya Waziri kukasimu Madaraka yake. Mimi napendekeza pia katika maeneo haya, Mkurugenzi mhusika pia akasimu madaraka yake kwa wale watakaotekeleza maagizo haya. Kifungu cha 16 - uwekaji wa rekodi, hapa labda mimi nizungumzie uzoefu na labda niseme naomba ku-*declare interest* kwa sababu naweza kusema halafu mtu akasema ni kwa sababu mimi nina kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Botswana kwao imekuwa ni nzuri sana kwa sababu wafugaji wanaouza ng'ombe kwenye viwanda vya kuchinja na kusindika nyama wanajulikana kwa sababu wana maeneo ambayo yapo *registered* na ng'ombe wanajulikana. Ng'ombe akitoka kwa mfugaji anakwenda moja kwa moja kwenye kiwanda kuchinjwa na anapimwa pale kwa mfugaji kwa uzito, lakini sisi kwa mfano kiwandani kwangu tunanunua ng'ombe mnadani. Sasa ng'ombe wa mnadani wana *identification* gani? Hamna!

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba Serikali kwa kushirikiana na Mikoa na Serikali za Mitaa tujitahidi kuhakikisha kwamba wafugaji wetu wana maeneo yanayoeleweka na ng'ombe wao wanatambuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu ule Muswada wa "*The Grazing Land and Animal Feed Resources Act* wa 2010." Naomba pia tuondoe utata. Katika kifungu cha 14 katika marekebisho ya Muswada yaliyoletwa hapa, badala ya kusema *Say Leader* inasema *Village Leader or Street*, bado hili ni tatizo kwa sababu ukisema *village leader* kuna ngazi mbili, kuna Mwenyekiti wa Kitongoji na Mwenyekiti wa Kijiji. Sasa anayezungumzwa hapa ni nani? Ni lazima tuelewe kwa sababu hii italeta matatizo kwenye utendaji. Tunaomba watufafanulie wenyewe, wakishindwa mimi nitaleta *amendment* tunapopitisha Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kutolea maelezo ni kifungu Na. 20 wanazungumzia habari ya *Inspector*. Katika Muswada huu, sehemu ya *interpretation* hakuna *inspector*. Kwa hiyo, kumweka *inspector* hapa sio sawa kwa sababu haijatajwa kwenye *interpretation* ya Muswada. Kwa hiyo, tunaomba tupate ufafanuzi juu ya hilo pia. Kifungu cha 17 - *Village Council.* Mimi napendekeza kifungu cha 17(1) iwe *village Assembly* kwa sababu *Village Council* hizi zinahongwa, wanaweza kupewa hela wakauza ardhi ya wanakijiji na mimi ni Mbunge wa miaka mingi na nimeona ugomvi wetu vijijini ni *Village Council* kutoa maeneo kwa watu bila wanakijiji kutoa kubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kifungu cha 38. Mimi napendekeza kwamba utaratibu wa kuweka kumbukumbu kitaifa uende mpaka Mkoani, isiwe Taifa peke yake. Nchi hii ni kubwa inawezekanaje kitaifa peke yake ndiyo mkaona kumbukumbu za mambo haya? Tunataka kumbukumbu hizi ziwekwe kwenye ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya ili tunapotaka taarifa kwenye Wilaya zetu tuzipate, siyo tungoje mpaka zitoke Wizarani. Hii ni kukumbatia mamlaka juu zaidi! Kwa hiyo, tunaomba mpango na utaratibu utengenezwe utakaoteremsha madaraka mpaka Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Miswada yote miwili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Janeth Mbene. Nafikiri ndiyo *Speech* yako ya kwanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Simbachawene wajiandaye, pia na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kufika katika Bunge hili Tukufu. Napenda nikushukuru pia wewe kwa kuniruhusu kuzungumza na kuchangia katika Miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Rais kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge hili Tukufu, naamini amekuwa na imani ya utendaji wangu na mimi napenda kumuahidi kuwa nitaitumia imani hiyo vizuri kwa kutimiza wajibu wangu vizuri katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kutoa shukrani za dhati kwa familia yangu, hasa watoto wangu ambao wamenivumilia na wamekuwa wakishirikiana nami kwa kiasi kikubwa sana katika shughuli zangu mbalimbali; napenda vile vile kuishukuru Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao wamenipokea vizuri sana kiasi cha kunifanya nihisi kama nimekuwa na Kamati hii kwa muda mrefu. Napenda niwashukuru sana Mheshimiwa Gideon Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa Salehe Naibu wake na Wajumbe wengine wote wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kwa fursa niliyonayo hapa kuwashukuru viongozi wenzangu, wanachama wa CCM wa ngazi zote; vile vile viongozi na wanachama wa UWT, Wafanyakazi wenzangu pamoja na Asasi mbalimbali ambazo nimekuwa nikizitumikia. Mwisho, lakini siyo kwa uchache wa umuhimu ni wakazi wenzangu na wapigakura wangu wa Mtaa wa Masaki ambao mimi ni Mwenyekiti wao hadi hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo ningependa tu kuchangia na ninaomba kwa idhini yako nichangie Miswada yote miwili kwa sababu ninaamini kwanza ina uhusiano mkubwa sana na kwa hiyo, inakuwa vizuri zaidi nikiichangia yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na ule wa *Livestock Identification, Registration and Treceability Act,* 2010 ambayo mimi naamini lengo lake kuu ni kukidhi

masuala na masharti ya soko la bidhaa za mifugo kimataifa ili kuhakikishia wadau wa soko la mifugo na bidhaa hizo juu ya njia za uzalishaji ambazo tunazitumia, kuhakiki jinsi gani tunavyotunza na ku-*handle* hizi bidhaa za mifugo ili kujenga imani kwa soko letu kwa wanunuzi wa bidhaa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Muswada huu unasaidia kudhibiti masuala ya maradhi, kufuatilia historia ya uzao wa mifugo yetu na kwa hali hii kusimamia vizuri zaidi utunzwaji na suala zima la *breeding* ama uzalishwaji wa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa tunafahamu kuwa mfugo wa aina fulani unafaa zaidi, inakuwa rahisi zaidi hata kwa wataalamu kuendelea kufanya kazi ya uboreshaji wa mifugo hiyo. Kutokana na hilo, mimi naona kuna haja kubwa ya kubuni au kutumia mifumo rahisi sana katika kuhakikisha shughuli hii inakubalika hasa kwa walengwa wenyewe, wafugaji na wadau wengine wa sekta hii na hii itawaondolea adha ya kufikiria kuwa Muswada huu umekuja kuwaongezea bugudha na badala yake kumbe umekuja kwa ajili ya kuwanufaisha wao wenyewe na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kuhaikisha kuwa njia tutakozotumia kuwaelewesha wafugaji na wadau wengine ni njia ambazo zinaeleweka, tukizingatia utamaduni, lugha na maeneo wafugaji wengi wanakotoka na hii nazungumzia zaidi wafugaji wa asili. Kuna mifano ya nchi ambazo zimefanikiwa na ndiyo maana naona Muswada huu hautakuwa vigumu sana kuutekeleza tukiwa makini. Sina wasiwasi na hilo! Ninachofikiria sasa hivi, kitu muhimu ambacho Serikali inapaswa kuzingatia ni elimu kwa wafugaji na wadau wengine wa sekta hii, lakini vile vile elimu kwa Maafisa wetu wa Ugani. Nafikiri hata kwao hili pia ni jambo jipya, kwa hiyo, kwa vyovyote vile itahitajika elimu ya juu kwa ajili ya wao wenyewe pia waelewe hili jambo kabla hawajalipeleka kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jambo hili pia watahitaji kuwa makini na wabunifu katika kutafuta njia za kufuatilia utendaji wa Muswada huu. Kama ilivyoainishwa, wafugaji wetu wengi bado ni wale ambao wanatangatanga na mifugo. Najua hii itafikia ukomo wakati fulani, lakini kwa sasa hivi kwa kuwa hali ndiyo ilivyo, itabidi ufuatiliaji vilevile uzingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala vile vile la matumizi mazuri au bora ya wagani wetu. Nchi imesomesha wagani wengi sana, naamini na wengine wameishia kwenye sekta ambazo hazihusiani na taaluma zao. Sasa huu ndiyo wakati mzuri wa kufanya tathmini ya pale walipo na kuwarudisha katika fani yao kwa kuwajengea mazingira mazuri bora ya utendaji kazi ambayo yatawavutia kukaa katika fani ambayo Taifa lilitumia pesa nyingi kuwasomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni raslimali yenye thamani, lakini vile vile ni mwanzo wa mtiririko wa chakula kwa wanadamu *(supply food chain)*, kwa hiyo, ubora wake ni muhimu kwa afya ya binadamu na ndiyo maana Muswada huu siyo tu kwa ajili ya kuuza, lakini vile vile hata kwa watumiaji wa bidhaa za mifugo utawasaidia kwa kuwa na uhakika kuwa wanakula chakula ambacho kinatokana na mifugo iliyokuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuangalia umuhimu wa kuungana au kushirikiana na nchi nyingine za jirani hasa nchi za Afrika Mashariki na nje ya Afrika Mashariki kidogo ambao nao pia wana idadi kubwa ya mifugo na wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kama za kwetu, nikizungumzia mifano ya Ethiopia, Kenya, Sudani, Uganda na hata Rwanda. Katika kushughulikia sheria hii, utekelezaji wake uzingatie ni jinsi gani tutakuwa tuna uhusiano na nchi hizi jirani katika kujenga *system* ambazo zinaoana ili kuhakikisha tunapofanya *traceability* kwetu na za kwao ziwe zinashabihiana. Kwa hiyo, naamini kuwa vile vile tunazungumzia kuwa hii itasaidia sana katika kuzuia wizi wa mifugo na hii nafikiri itakuwa ndiyo *motivation* kubwa kwa wafugaji katika kuwaelezea na kuikubali sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa hii inafanya kazi, basi zile alama zitakazotumika kwa *system* yoyote ile ambayo itatumika ni lazima ziwe zile ambazo ziko wazi zinazoonekana ili kuzuia mtu kuiba kwa kuona kuwa kwa kuiba atashikwa kwa urahisi na ufuatiliaji wake pia uwe wa wazi unapoweka kinga ya kuzuia wizi, lakini vile vile uwe na njia ya kuhakikisha kuwa wale wanaotaka kuiba na wewe pia unaweza ukawa-*trace* kwa urahisi. Kama vile kwa binadamu tunapokuwa na Polisi wa wanaozuia uhalifu, basi na hili pia nalo liangaliwe ni jinsi gani litakavyosimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisahau mchango wa taasisi zinazopigania haki za wanyama. Kwetu sisi kiafrika, labda hii inakuwa siyo muhimu, lakini kwa sababu tuna soko tunalolilenga, na nje wao hivi vitu kwao wanaviangalia, kwa hiyo, na sisi tusivipuuzie.

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzaji wa kumbukumbu uwe mzuri na salama. Naamini hivyo ni vitu vitakavyokwenda katika utekelezaji. Ningependa tu kusisitiza kwamba huu Muswada hasa wa *The Livestock Identification, Registration and Traceablity* siyo Muswada rahisi sana kuutekeleza kutokana na taaluma ambayo inahusika na kutokana vile vile na tabia ya ufugaji tunaouendesha katika nchi yetu. Kwa hiyo, umakini utatakiwa katika kubuni mifumo mizuri ambayo kama ilivyozungumzwa haitaleta usumbufu wa kupita kiasi. Lakini vilevile utakubalika kwa urahisi zaidi na wafugaji na ndiyo maana suala la elimu linakuwa bado ni la muhimu sana. Masuala ya jadi na ujuzi wa kiasili *(indigenous knowledge)* isipuuzwe katika suala hili kwa sababu wafugaji wengi wenyewe wana taaluma zao na wanajua ni jinsi gani na mifugo ipi inafaa sehemu zipi. Kwa hiyo, na sisi itakuwa ni vizuri tukijifunza kutoka kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia zoezi zima la ku-*track*, ku-*identify* na ku-*trace* hii mifugo, ningependa sana kusisitiza diplomasia itumike ya hali ya juu tukizingatia mila na desturi za makundi ya wafugaji ambao tunawalenga, tukahitajika sisi kama viongozi kuwa na utashi wa kisiasa na kuwa na umoja, wote tujiunge katika kutetea hii Miswada. Naamini huku ndani tuna Wabunge ambao wanasimamia zaidi kwa wafugaji na wengine wanasimamia zaidi kwa wakulima, lakini kwa Miswada kama hii ingependeza kama sisi sote tungeungana kwa pamoja kwa sababu hili ni jambo jema kwa wote. *(Makofi)*

Ningependa kumalizia kuhusiana na masuala ya *grazing land*, ningependa kusisitiza vile kuwa, Serikali itambue mchango wa wafugaji katika kutunza mazingira ya asili, najua kuna dhana kuwa wafugaji wanavuruga sana mazingira, lakini vile vile huwa wanachangia katika kutunza mazingira, hiyo pia iangaliwe. Kule wanapofanya vizuri tujaribu kuboresha, uwezo wa wafugaji kumudu mazingira yao pia utiliwe maanani katika kutambua sehemu zipi zinafaa kwao kwa malisho na matunzo ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kusisitiza kutambua maeneo ya kuchungia mifugo ambayo yanaendana na maji. Tukumbuke kuwa wafugaji wanatangatanga kwa sababu ya kutafuta malisho na maji. Kwa hiyo, maji iwe ni kiungo muhimu ambacho ni lazima kitatumika katika kuhakikisha kuwa wafugaji wanakaa mahali pamoja. Wakati wa kupunguza mifugo iliyozidi katika eneo nafikiri hapa vilevile busara inatakiwa itumike na uwekwe utaratibu wa kujua hiyo mifugo itakayopunguzwa inafanywaje na inakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini nimefikia mwisho wa kuchangia kwangu. Nashukuru sana kwa nafasi hii na ninaunga mkono Miswada hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, naona leo *speech* yako ya kwanza imetoka vizuri sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Estherina Kilasi atafuatiwa na Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Simbachawene ajiandaye.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza nami kuchangia Miswada hii miwili iliyopo mbele yetu, Muswada wa Utambuzi na Muswada wa Malisho ya mifugo. Labda niseme tu naipongeza Wizara kwa hatua moja angalau imeanza kuona umuhimu wa kudhibiti mifugo na kuwapa haki zao wafugaji kwa hali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia Muswada huu, nimejiuliza maswali mengi sana. Swali la kwanza nilikuwa najiuliza, hii sheria tunaitunga kwa ajili ya matumizi ya nani ? Kwa ajili ya matumizi ya wafugaji wanaofanana, samahani Mheshimiwa Mzindakaya, au ni wale wafugaji walioko kule kijijini ambao wanazunguka kila siku na kutafuta maji na malisho ? Kwa sababu mnapotunga hii sheria na unasema itaanza kutumika mara moja, ninaamini kabisa watakaokuwa wanaingia hatiani na wenye matatizo makubwa ambao wamekuwa wakipata kila siku ni wale wafugaji wa kawaida waliopo kule kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niungane tu kwa mara ya kwanza na Msemaji wa Upinzani aliyesema, sikutegemea kwamba sheria hii ingekuja saa hizi kabla hatujaandaa mazingira mazuri ya wafugaji, kwa sababu ukishaandaa mazingira mazuri, ukawapa elimu, sasa unawatungia sheria wasikiuke vile vitu ambavyo umewawekea.

Sasa unawatungia sheria wakati bado haki zao hazijatekelezwa ipasavyo, halafu unamuweka ndani, itakuwaje? Tuangalie tu *reference* ya kule tulikotoka, nami nasema kwa sababu tunatunga sheria baada ya matukio, linatokea tatizo unafikiria kuna tatizo mahali tutunge sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwenye matukio ambayo yametokea tunaposema kwamba kutambua mifugo, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo, labda wizi; kwa sababu kama lengo ni kuzuia wizi na kuzuia magonjwa mimi nakubaliana na huu Muswada naunga mkono, lakini kama lengo ni zaidi ya hapo ni tatizo sana kwangu. Kwa sababu hapa tungeangalia hata usafirishaji tu wa mifugo, kwamba hii mifugo inaruhusiwa kusafirishwa kwa kuswagwa kwa kilomita ngapi ili kuzia mateso ya mifugo wanayoipata?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mfano uliotokea Kilosa na Mbarali ambao na mimi imenivutia sana nichangie huu Muswada, kwamba tunapopitisha sheria hii unawaachia wale wanaoitumia kule, fikiria tuliposema mifugo ihamishwe bila sheria hii kuwepo, hatukufikiria wanasafiri vipi, hatukufikirii wanakokwenda wataishije, lakini bado umemwambia ni lazima uhame uende Mkoa wa Lindi. Kule Lindi anakokwenda hakuna josho, hakuna maji, hakuna malisho na ni sehemu ya wakulima kule, sasa huyu mfugaji unamwambia nenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwa uzoefu kabisa na kwa uchungu mkubwa, umaskini waliopata wafugaji ni katika zoezi la kuhamisha mifugo na nafikiri ilikuwa ni ajenda muhimu sana ya kujadili kabla hata ya kutunga sheria. Tunawapa fidia gani hawa wafugaji ambao wamekuwa maskini mpaka leo ? Lundo la mifugo iliyokufa njiani huko inasikitisha na inatia uchungu, na waliofika Lindi wana ng’ombe elfu moja wanarudi na ng’ombe mbili na wamerudi tena kule kwenye makao ya zamani wameanza kulima badala ya kufuga, watafikiriwaje hawa watu na hii sheria itawalindaje ili isitokee tena hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu huyu mfugaji ambaye hajui kusoma atasajili, ataweka rekodi, atafanya nini ni vitu ambavyo vinaonekana viko *advanced* sana kuliko mfugaji mwenyewe. Mimi nilikuwa namshauri Waziri kuhusu sheria hii, kwamba iangaliwe katika kanuni anazotunga itaanza lini utekelezaji wake ? Kwanza tunatoa elimu kwa wale wafugaji wenyewe, lakini pili tuangalie hawa wafugaji wengi wanaotoka sehemu moja kwenda nyingine wataangaliwa vipi na hii sheria ili isiwaathiri tena wakarudi nyuma kule ambako matatizo yaliwapata ? Kwa sababu mifugo haina sheria kama wanyamapori, hivi kuna eneo linaweza likatengwa leo kwa ajili ya wafugaji, lakini kesho likatangazwa kwamba hii inakuwa ni hifadhi ya Taifa ya Wanyamapori, inabidi wafugaji tena wahame wapishe wanyamapori! Sasa ndiyo hii imekuwa tatizo. Hakuna sheria ya wakulima, hakuna ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kilimo, kwa ajili ya mifugo na kwa ajili ya shughuli nyingine. Sasa hawa wamekuwa wakihangaishwa kila wakati na hii imeleta mkanganyiko kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba niseme tu kwa uchungu kwamba wafugaji wale ninaowafahamu mimi wa jamii yetu ya klisukuma ambayo namwona kwamba sio rahisi akasema nina ng’ombe 2000 au 3000 kwa mila na desturi zao mimi ninavyofikiri, sasa leo watabanwa sana kwa sababu utamwuliza una ng’ombe wangapi? Hatasema hata siku moja, sana atadanganya ana ng’ombe mia mbili kumbe ana ng’ombe 1000. Leo atabanwa na hii sheria, elimu hiyo Msukuma ataipataje pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ni ngumu. Ungeanza kwanza na elimu na kutengeneza mazingira mazuri ya hawa wafugaji wanaozurura kila siku ili kusudi kuwawezesha sheria inapotungwa iwe rahisi sana kwao kuifuata, vinginevyo hatufiki mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye usafirishaji wa mifugo, hapa sioni kipengele katika sheria hii kinachosema: Je, tutaendelea kuswaga? Umesema tu utambuzi, usajili na kutunza kumbukumbu. Je, usafirishaji wa mifugo utakuwaje? Hivi mfugaji aruhusiwe tu kuswaga kilomita 200, 300? Nafikiri kingewekwa kipengele kwamba angalau utasafirisha mifugo zaidi ya kilomita tano au moja utumie usafiri wa gari, treni au usafiri wa njia nyingine yoyote, lakini siyo kwa kuswaga. Hiyo iongezwe pale kwenye sheria. Najua kwa wafugaji wenye mifugo mingi ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine lililopo ni kwamba tunataka kupunguza mifugo, kwa sababu ya udhibiti ni lazima uwe na mifugo michache, usiwe na mifugo mingi.  Soko la mifugo liko tayari? Tunawawezeshaje hawa wafugaji wapate soko kwa ajili kuuza hii mifugo yao ili wapunguze idadi ya mifugo? Kwa sababu sio rahisi kwa mifugo iliyopo hapa kwa mfano Mbarali, nilikuwa na mifugo zaidi ya 600,000, lakini wengi wamekufa kwa kuhamishwa, hawakufika huko walikotakiwa kufika, tukaambiwa tubaki na mifugo sitini na tano elfu kule ndani kwa ajili ya kufuga. Lakini hilo eneo linatengwa na nani ? Hapa  mnasema Halmashauri waachiwe kazi ya kutenga maeneo na kuangalia malisho ya mifugo, hivi kweli Halmashauri itaweza kufanya hiyo kazi ?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiri tu kama nchi nyingine unapokwenda,  mfano *South Africa* unakuta kabisa ni eneo limetangazwa kwamba hili eneo lote kinchi ni la ufugaji, kwa ajili ya wafugaji wenye mifugo mingi, badala ya kuwaachia Halmashauri huu mzigo. Sasa sijajua Waziri utakuwa umejipanga vipi na sheria hii! Kuwaachia Halmashauri ni kazi na kuwaachia Maafisa Watendaji wa Vijiji wa-*identify* eneo la kufugia ni kuwapa sehemu nyingine ya ulaji na kuwanyanyasa wafugaji kama ilivyokuwa inatokea huko nyuma na kwa sababu wamekuwa wakiuza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa mifugo, tunasema ng’ombe ukimuuza utatoa taarifa na ng’ombe wanaozaliwa tena watatolewa taarifa na yule mfugaji awe na rekodi yake.  Hiki kitu kinawezekana kweli? Basi tutafunga wafugaji wengi sana tulionao hapa Tanzania. Sheria iko *advanced* kuliko hali halisi tuliyonayo sisi.

Mimi nimevutiwa sana kama ni kudhibiti ugonjwa, kama ni kudhibiti kwa ajili ya kuzuia wizi, sina tatizo. Lakini kama ni lengo la kuboresha mifugo na kuwafanya wafugaji wapate kipato, tunahitaji elimu zaidi kwa wafugaji wetu zaidi sana hawa ambao wanatoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Hii nyingine ya kuweka alama ya kwamba watu wanaweka chapa kwenye mifugo, kwa kweli imekuwa ni kero, lakini mfugaji utamwambiaje kwamba ni lazima uweke utambuzi wa jina lako?  Hivi vitu vipo, hizo hereni za kuvisha zipo ama tumejiandaa vipi  zifike kule kabla ya sheria hii kuanza matumizi yake? Kwa hiyo, kuna muda mwingi sana wa sasa tangu tutakapoipitisha sheria mpaka hapo itakapoanza kutumika, hawa wafugaji wawe tayari wameshapewa elimu na

vifaa viwe tayari vimeshaandaliwa kwa ajili wa wafugaji kuweza kupata hivi vifaa kwa ajili ya ku-*identify* mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme ni kuhusu udhibiti wa magonjwa. Kwa kweli Mheshimiwa Mzindakaya amelisema hapa kwamba mifugo inatoka labda Sumbawanga, Iringa au kwingineko inakuja kuuzwa mnadani. Lakini bila kujua magonjwa haya, lakini Serikali imekuwa ikitangaza, madawa ya mapafu na madawa mengine yanatolewa bure, *since then* hatujawahi kuyaona hayo madawa yakitolewa bure. Sana sana ni watu binafsi ndiyo wamekuwa wakiuza hayo madawa. Sasa tuombe tu kwamba kama kuna eneo fulani lina matatizo ya ugonjwa wa mapafu Serikali itoe kipaumbele kupeleka dawa hizo ili kudhibiti ugonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *finally* sheria hii itawagusa wenye maeneo ya ufugaji tu. Mimi nakumbuka wakati tatizo hili linatokea kule Mbarali, nikauliza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kuna sheria gani inamruhusu mtu kufungia mifugo ikakaa wiki nzima bila kupata chakula? Hakuna sheria yoyote inayoweza ikamdhibiti huyu mtu anayefungia mifugo, kwa sababu labda hawajalipa ushuru, wanafungiwa siku tatu hadi nne bila chakula. Ukikuta mfugo umekonda hata huwezi kuamini hata kama huna uchungu kiasi gani unatoa machozi, ni nani apewe adhabu ya namna hiyo na sheria gani itamlinda au italinda hii mifugo kwamba huruhusiwi kushika mifugo ukaifungia mahali kwa siku tatu bila chakula ? Ukifanya hivyo na wewe uchukuliwe hatua basi na sheria nayo iseme kwa upande huo mwingine ili kuweza kutoa haki kwa hawa wafugaji, kwa sababu wafugaji wamekuwa ndiyo watu wa kuonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ni sawa kwamba wakulima wana haki na wafugaji nao wana haki zao, wa-*identify* njia za kupitisha mifugo hasa wanapokwenda kwa ajili ya chanjo na kwa ajili ya kuogeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sheria imezungumzia tu kwamba utatangaza eneo lakini vile vile nafikiri ungeongezea kwenye Halmashauri kwamba wa-*identify* njia muhimu ambazo zitapitishwa kila Wilaya au kila Halmashauri ionyeshe au kila Kijiji kwamba mifugo itapita katika njia fulani kwa ajili ya kwenda kwenye malisho au kwa ajili ya kwenda kwenye majosho au kwa ajili ya kwenda kuogeshwa kwa sababu imekuwa ni matatizo. Huko sisi tunaokaa vijijini mifugo mingi inatembea inakanyaga mazao ya watu, inakuwa ni vita na watu wanauana. Lakini kama kwenye kanuni itaonyeshwa kwamba kila Halmshauri ihakikishe sehemu za mifugo, wanaandaa njia ambayo mifugo itapita kusudi isiathiri mazao ya wakulima. Kwa hiyo, mimi nilikuwa na hilo.

Lakini nimeguswa sana kwamba hii sheria inabane sehemu zote, iwalinde wafugaji lakini iangalie kwamba tuko wafugaji wa hali ya chini sana ambao kielimu hatujui chochote. Kwa hiyo, isije ikatuumiza na itakapokuja kutekelezwa mara nyingi huwa tunaachiana maeneo. Wewe mwenye mifugo ndio utaanza kutetea wafugaji wako, utampigia Mheshimiwa John Magufuli humpati, utampigia Naibu Waziri humpati, wewe unahangaika na wafugaji. Kwa hiyo, naomba tu kwamba sheria izingatie vipengele vyote ambavyo vitalinda haki ya mfugaji, italinda vile vile haki ya mkulima kwamba

huruhusiwi kwenda kwenye mazao na wafugaji. Lakini kwa kuwekea kila njia kwa kuwekea maeneo ya malisho, malisho haya isiachiwe Halmashauri, maana yake mara nyingi nimekuwa nikisema hapa nikiomba majosho, mnasema Halmashauri itafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtusaidie kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, Halmashauri itafanya. Halmashauri siku hizi hazina kipato. Naamini zamani ng'ombe walikuwa na thamani kwa sababu walikuwa wanatozwa ushuru na Halmashauri zilikuwa zinapata ushuru. Kwa hiyo, walikuwa wanaona mifugo ni kitu muhimu sana. Kwa sasa hivi baada ya kufutwa ushuru mifugo imekuwa ni kero kwa kila Halmashauri kwa kila mahali kwa sababu sasa haiongezi kipato chochote ndani ya Halmashauri. Kwa hiyo, tunahitaji sana Serikali Kuu iwe inasaidia. Kama ni ruzuku kwenye maeneo ya ufugaji itolewe mapema. Hata kabla ya kuhamisha mifugo kwenda kwenye maeneo hayo isiwe kama vile tulivyofanya Lindi. Maeneo ambayo tunafikiri tuta-*identify* kwa ajili ya wafugaji, basi yawekewe miundombinu ya kutosha na hatimaye wafugaji nao wapate haki yao kama wananchi wa nchi hii. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Leo umewawakilisha kweli watu wako.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelekea kwenye Kanuni ya 69(1) inasema hivi: "Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, aaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe."

Mheshimiwa Naibu Spika, inaendelea na kifungu kidogo cha (2): "Kama Spika atakuwa na maoni inaendelea pale kwenye fasili ndogo ya (2)."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikidhi matakwa ya kanuni hii ya 69(1) kwa kutoa maelezo ya sababu za kwa nini nataka kuliomba Bunge lako Tukufu liahirishe hoja muhimu sana iliyoko mbele yetu. Hoja tunayoijadili sasa inagusa mstakabali wa maisha mazima ya wafugaji wa Tanzania katika nchi nzima na ambayo kama Miswada hii miwili itapitishwa kwa jinsi ilivyo bila kupata muda wa kufanyiwa marekebisho ya kutosha, athari yake ni kubwa sana kwa maisha ya watu hawa. Nichukue tu mfano wa vifungu ambavyo wenzangu wamejaribu kuelezea kikiwemo kifungu cha 4(3) na kifungu cha 6(4) au kifungu kizima cha sita cha Muswada huu ambao uko mbele yake wa *The Livestock Identification Registration and Traceability Bill, 2010.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hiyo kwamba anayepata mifugo unalazimika kusajili mifugo kama ambavyo unasajili gari, kuandika *chases number* unakwenda baadaye unapewa namba. Unazungumzia kazi hiyo ifanyike ndani ya siku saba, unamtoa mfugaji ambaye kila siku katika maisha yetu ya kawaida unalazimika kumbadilisha dume kwa ndama kadhaa, hawa nao wanatakiwa kusajili leo na wanatakiwa

kusajili ndani ya siku saba. Sheria yenyewe ukiendelea huku mbele ina utaratibu wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine nao umewekwa katika sura ambayo hauna tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka Bunge hili lione kwamba kama wafugaji wasingehama miezi michache iliyopita juzi leo Longido kusingekuwa na ng'ombe hata mmoja. Kama mifugo isingehama katika msimu huu wa kiangazi iliyopita, leo Simanjiro tusingekuwa na ng'ombe hata mmoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, kifungu cha 69 kimoja kiko *very clear* sababu unazotaka tuondoe huo Muswada. Sasa unaingia kwenye mjadala ambao wewe uko katika orodha ya watu watakaojadili. Kwa maana hiyo na mimi natumia kifungu cha 69(1) kwamba tupate maoni ya Wabunge wanavyochangia na mwisho tutafikia maamuzi. Kwa hiyo, nasema tunaendelea na mjadala kusudi Serikali izidi kupata maoni ya Wabunge maana tukiahirisha hatutapata maoni yoyote. Tutaondoka, lakini hakuna maoni yoyote. Sasa tuache Wabunge wajadili tufikie mahali tukubaliane. Kwa hiyo, mujibu wa kanuni ya 69(2) nakataa ombi lako. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru na mimi kupata fursa hii ili niweze kuchangia katika Miswada hii miwili ambayo imewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Sheria ya Malisho ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na viongozi wote wa Wizara hii kwa kuleta Miswada hii ili tuweze kuijadili kwa kina. Kama wenzangu waliotangulia, Miswada hii ni Mizuri lakini inaleta mikanganyiko mingi tu ambayo tutaipata wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukua mfano tu, katika Muswada wa *Livestock Identification, Registration and Traceability Bill, 2010* kifungu cha nne pamoja na kifungu cha tano kinazungumza juu ya *National Livestock Identification* na *National Livestock Registration* na mambo kama hayo. Unaweza kuanzia tu *Registration*, lakini mimi nilikuwa nafikiri ni vizuri Wizara hii kwanza ikaanza kufanya sensa ya mifugo ili tuweze kujua kwa uhakika tuna mifugo kiasi gani katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Lakini ukisema tu uanze kufanya *Registration* kama tunavyosajili pikipiki na magari, wapo ndugu zetu ambao ni wafugaji wamejificha katika misitu na hawataki kutokea katika maeneo yoyote kwa sababu wanaogopa idadi ya mifugo itajulikana. Walikuwa wanaogopa hivyo kwa sababu mifugo hii ilikuwa inatozwa kodi.

Sasa hawa waliojificha wewe ukitaka waandikishe mifugo yao, utakuta mfugaji mmoja ana mifugo zaidi ya 6,000, unamwambia afanye *Registration.* Lakini anaishi katika msitu, mfano wa Uvinza na anatakiwa afanye *Registration.* Ni nani atakayekwenda kule kufanya *Registration*? Kwa sababu utakuta hata katika Halmashauri

wanazoishi hakuna Afisa ambaye anafahamu hawa watu wanachungia mifugo yao wapi! Lakini wapo!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nadhani tungeanza kwanza na sensa ya mifugo ili tuwe na uhakika. Tunapotaja takwimu hizi nyingi ni zile ambazo tumefanya tu kwa kukadiria kwamba tunadhani tuna ng'ombe kiasi kadhaa, mbuzi kiasi kadhaa na nguruwe kiasi kadhaa. Halafu ng'ombe hawa wanazaliana kwa wingi sana kila siku wala idadi ile tunayotaja sio sensa halisi ambayo tunakuwa nayo. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tuanze na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tukienda katika kifungu cha 5(6) na (8) kweli kuna jambo ambalo linatokea kwa wafugaji wetu kujiwekea alama zao za asili. Alama wanazoziweka kwa sababu ni mbinu za jadi wanawaharibu ng'ombe kweli kweli kwa sababu wanaweka alama ambayo hata akiwa mita 20 aweze kumtambua kwamba yule ni ng'ombe yake kwa alama aliyoweka kwenye ngozi. Yaani amemchoma kuweka alama ambayo anaweza kuiona hata kwa mbali. Huu ni ukatili wa wanyama ambao tunawafuga.

Lakini pia wanaharibu ngozi ndiyo maana hata tunapopeleka katika masoko ng'ombe wanaotoka Tanzania wengi unakuta ngozi zao inabidi wakate vile vipande ambavyo vimeharibiwa kwa alama tunazoziweka. Kuweka alama ambazo zitawasaidia ku-*identify* wanyama wetu itasaidia. Lakini pia itasaidia kwa wizi ambao unatokea sehemu za mipakani. Mnaweza mkafuatilia kama tutakuwa na njia mpya ya kuweza kuwatambua hawa wanyama. Tunaweza kweli tukawatambua wakibiwa wakivushwa katika nje ya mipaka yetu. *(Makofi)*

Lakini kwa Mkoa wa Rukwa ng'ombe akibiwa akivushwa akiingia tu katika nchi ya Zambia akionekana tu kitu cha kwanza ni kupigwa risasi majadiliano yatafuata. Halafu mnapojadiliana wameshatengeneza na nyama wanakula, ndio mnajadiliana ng'ombe huyu alikujaje na kitu gani wala hutapata kitu chochote. Sasa *traceability* hiyo wala haitakusaidia kwa sababu ng'ombe akiingia katika nchi ya Zambia ni kupigwa risasi. Wale wanaoibiwa katika mipaka mingine wanaibiwa kwa ajili ya kwenda kufugwa au kwenda kubadilishwa na vitu vingine. Lakini kwetu inakuwa ni vigumu, kumbe hiyo inaweza wala isitusaidie ile ku-*identify* wanyama wanapoibwa upande wa Mkoa wetu wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye malisho kwa sababu katika eneo hili la malisho ndilo hasa mimi naona lina migogoro sana kwa sababu sheria hii ilivyotungwa mimi ninavyoliona kwa bahati nzuri Mheshimiwa John Magufuli alikuwa Waziri wa Ardhi anaifahamu Sheria namba nne na tano ya vijiji ambayo imeeleza wazi kwamba vijiji vitajiwekea matumizi bora ya ardhi watenge maeneo.

Sasa hapa ni kama ame-*superimpose* juu ya sheria namba nne na tano sheria hii ya malisho kwa sababu ipo sheria namba tano ambayo inaeleza vijiji vifanye nini. Vijiji hivi ni vile vya wakulima na wafugaji, wanaishi pamoja na wanafuga ng'ombe wa kiasi ambao mipaka yake unaweza kusema imefika pale na watalisha mifugo huku na huku

wataweka msitu, huku wataweka vitu vingine. Lakini kwa idadi ya mifugo tuliyonayo na wahamiaji wanaokuja mfano katika Mkoa wa Rukwa wameingia kiasi ambacho hata kijiji kikipanga kwamba eneo hili litakuwa la mifugo haiwezi ikatekelezeka kwa sababu idadi ya mifugo ni mingi sana.

Lakini la pili hali ya hewa inavyojitokeza ikifika wakati wa kiangazi malisho yamekwisha mfugaji anataka mifugo yake iendelee kuishi, atapeleka mahali popote hata pale mlipokataza kisheria kwamba msipeleke hapa mfano, misitu wanaingiza ng’ombe kwenda kula mle. Katika vyanzo vya mito, vyanzo vya chemchemi vyote vinaharibiwa kwa sababu ikifika kiangazi ndiyo sehemu zilizobaki na nyasi kidogo au malisho wanapeleka huko hivyo kum-*control how* huyu mtu kumwambia usiende sehemu hiyo inakuwa vigumu kwa sababu na yeye anasema natetea mifugo yangu isije ikafa. Hivyo, Sheria hii sijaona ni namna gani ambavyo itaweza kuepusha migogoro na kuweza kutumia maeneo madogo ya vijiji kwa ajili ya malisho ya mifugo. *(Makofi)*

Mimi nafikiri Serikali ingeangalia jinsi ya kutafuta maeneo makubwa yasiyokaliwa na watu watengeneze miundombinu ya maji, majosho na kupeleka madawa katika maeneo hayo. Wafugaji wale ambao wako tayari kuwa na mifugo idadi inayojulikana wapewe maeneo hayo ili waweze kufuga kisasa ili tuweze kuiga wale wa Botswana wanavyofuga, hapo ndipo mifugo itakapokuwa na manufaa.

Lakini wakati huo huo tuandae mazingira ya kuhakikisha kwamba wafugaji hao watavuna mifugo kwa kupeleka katika viwanda tuweze kupata mazao yale ambayo yatasindikwa na tuweze kuuza nchi za nje. Lakini kama tutaendelea kufuga kiasili na kuacha watu waendelee kuhangaika katika kutafuta malisho, nina uhakika uharibifu wa mazingira utaendelea, vyanzo vya mito vitaharibiwa, migogoro kati ya wakulima na wafugaji itaendelea na hili suala halitasaidia hata kidogo badala yake tutajiona kwamba tunazusha migogoro mingine badala ya kuweza kuwasaidia wafugaji wetu ambao tunataka waweze kufuga katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani sheria hii pia ya malisho ingeweza kusaidia kupiga marufuku ufugaji holela ili watu waanze kutafuta jinsi gani wanavyoweza kupata maeneo makubwa ya kuweza kufuga kwa kufuata maelekezo ya Wizara ili waweze kufuga kisasa na waweze kufuga mifugo ile ambayo inaweza kunenepeshwa na ikaweza kuleta faida kubwa kwa kuuza katika soko. Bila kufanya hivyo, mifugo itaendelea kuzurura sehemu mbalimbali katika nchi hii na tutaendelea kuharibu malisho, tutaendelea kuharibu mazingira yetu na hivyo tutaendelea kuingia katika mazingira magumu ya nchi yetu kugeuka jangwa na kupata ukame ambao utakuwa unaharibu mifugo mingi ambayo tumekuwa tukihangaika nayo kila mwaka.

Kuhusu suala la huyu *inspector* inakuwa vigumu sana kuangalia ni jinsi gani huyu *inspector* anavyopewa madaraka ya ku-*inspect* mifugo, eti akiona mifugo imekuwa mingi anatoa amri tu kwamba mifugo hiyo iuzwe au ihamishwe wakati Serikali hamjapanga maeneo ya kitaifa kwamba wale ambao wana mifugo mingi katika eneo hili watakwenda mahali pengine. Tutaleta mgogoro ule mkubwa kama ule ule tuliokuwa tumeepuka kwa kuwatumbukiza hawa ma-*inspector* waanze tena kugombana na wafugaji kama ilivyotokea katika Mikoa ile ambayo wakulima na wafugaji walianza kugombana.

Kumbe jambo hili nadhani ni busara tu Serikali ikaangalia ni jinsi gani ya kuweza kuepuka jambo hili lisije likatokea kwa sababu likitokea tena itaonekana Serikali haiko makini, ilitunga sheria hii tu kwa haraka kwa ajili ya kutaka tu kupitisha mambo fulani kadhaa machache, lakini haikuweza kutatua matatizo yote ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la kuwashirikisha wadau. Sheria hii kwa kweli wafugaji wameshirikishwa vizuri. Lakini ukienda katika vijiji ambavyo kuna wakulima na wafugaji kwa kweli jambo hili halikutekelezwa vizuri, wafugaji ndiyo tu wameshirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba Serikali ifikirie vizuri jinsi ya kuweza kushirikisha wadau wote. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha hadi leo kuwa niko salama. Lakini pia nawashukuru wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwa namna wanavyonipa ushirikiano na ninaamini wataendelea kunipa ushirikiano hadi muda wote mpaka kipindi cha mwaka huu mwezi kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo kama sita hivi ya kuchangia katika Miswada yote miwili. Kwa kuwa inafanana kwa hakika nitajitahidi kuchangia yote kwa pamoja, mchango wangu wa kwanza unakwenda katika huu Muswada wa *The Grazing Land and Animal Feed Resources Act, 2010* kifungu cha nne.

Nilikuwa najaribu kuangalia ile *composition* ya *council* nikapata shida kidogo na nikadhani pengine hawa waliowekwa hapa wote ni watalaam wa Serikali tu wanaowakilisha taasisi mbalimbali za umma. Lakini pale kwenye kifungu cha 3(c) nimeona pale wamesema *one member from the National Pastoral and agro pastoral organizations*. Sasa mimi nikajaribu kuwauliza wafugaji: Je, mna umoja wa wafugaji na umoja wa wakulima na wafugaji hapa Tanzania ambao ni *National*? Kwa hakika kwa majibu nilioupata kwa utafiti nilioufanya kwa wafugaji waliomo humu ndani ni kwamba hawana umoja huo. Sasa hiyo *National and Agro Pastoral Organization* wanapatikana wapi wawakilishi watakaokuwa kwenye hii *council*?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kifungu hicho chenyewe kinavyosema: *"One member from the National Pastoral and Agro Pastoral organization"*, maana hawa ni watu wawili. Mfugaji na mkulima anaweza akawa na ng'ombe watano, kumi, lakini analima pia. Huwezi kumkuta mfugaji mwenye ng'ombe 10,000 na mkulima pia. Kwa hiyo, mfugaji ni mfugaji na mkulima ni mkulima. Hapa tuwe wazi, kama tunataka kuingiza hawa ambao wanalima na kufuga, basi tuingize mwakilishi mmoja na hawa wanaofuga tu kama wenzetu wa akina Lekule Laizer, basi tuwaweke wao tu na wao wawe na mwakilishi. Kwa hiyo, hapa nadhani tunazungumzia wawakilishi wawili kama nitakuwa sijakosea kwa namna ilivyoandikwa. Lakini kwa kuwa wamekuwa ni *one member,* napenda nipate ufafanuzi maana yake ilikuwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nirudie tena. Nimesahau kuweka wawakilishi wengine ambao wanapaswa kuwepo. Kifungu cha nne, *composition* ya hii *council* kwamba wakati mfugaji hapa amepata matatizo siku za karibuni na kupoteza mifugo yao mingi kujitokeza *NGOs* ambazo zilikuwa zinawatetea na kujaribu kuwasaidia kutafuta haki yao, hivi kwa nini kusiwe kuna mwakilishi katika hii *council* inayotokana na *NGO reputable one* katika taasisi hizi za *NGO* akawawakilisha *NGO* zote zinazoshughulikia kuwatetea wafugaji hawa? Kuna ubaya gani? Katika dunia ya sasa ya *private public partnership* mimi nadhani hili ni jambo la msingi sana na wenyewe waweze kushirikishwa kwa sababu nia yao ni kusaidia ili hiki chombo kiweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika kile kifungu cha 14. Katika kifungu cha 14 ambacho Mheshimiwa Mzindakaya naye alikizungumzia hapa inazungumzwa kwamba mwanzo kabla ya kubadilishwa ilikuwa ni kwamba *inspector* huyu anaweza akaingia kwenye *dwelling house* akiambana na *Tensely Leader*, lakini baadaye wakasema *a Village Leader.*

*A Village* kama tunavyofahamu kwa hakika ni ngazi mbili katika kijiji, kuna Mwenyekiti wa Kitongoji na kwa Mijini kuna wa Mitaa. Sasa katika hali hiyo, mimi ningependekeza iwe kwamba *inspector* huyu anaweza kuingia kwenye nyumba kukagua akiambatana ama na Mwenyekiti wa Kijiji au wa Mtaa au wa Kitongoji.

Yeyote kati ya hawa akiambatana naye inakuwa vizuri. Vinginevyo inaweza hii ikatumika vibaya na tunafahamu mazingira ya taabu matatizo kule vijijini masuala ya utawala bora kidogo yako chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la tatu ni *section* ya 17 (1) ambapo pale anasema *the village council shall set aside part of the communal village land to be a strategic grazing land.* Sasa hapa uzoefu unaonyesha kwamba mara nyingi sana hawa *village council* kwa maana ya Serikali ya Kijiji ni wachache mno na kwa hiyo, wanaweza wakawa *corrupted* na wakamgawia mtu ardhi ya malisho halafu wananchi wengine hawajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano halisi uliotokea kwenye jimbo langu, ningependekeza hapa iwe ni *village assembly* badala ya *village council*. Maana wakiwa wengi wana uwezo wa kupendekeza, kwa hiyo, wengi watakubaliana kwa hiyo, rushwa pale inaweza isiwepo. Nadhani hii inaweza kutusaidia sana. *(Makofi)*

Lakini pia nilikuwa na taabu pia katika suala zima la mtiririko wa hizi *section*. Kwa kuwa *section* ya 19 inasema *the local government authority shall prepare grazing inventory analysis condition and land use planning,* mimi nilidhani hii ndio ingeanza, hii ndio ingekuwa *section* Na. 17 halafu inafuata hii hapa Na. 18 halafu hii ya kijiji inakuwa chini. Maana zinapokosa *sequence* sasa unaisoma sheria kinyume chake kabla huja-*plan* ile *grazing land inventory,* sasa wa kijiji anafanya nini kwa sababu hana ile *plan*. Kwa hiyo, ningependekeza *section* hizi zirekebishwe kwa namna nilivyozisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine unakwenda kwenye ile *section* ya 20 ambapo anazungumziwa huyu *inspector*. Niseme tu kwa kweli tunapotunga sheria hizi tuelewe kwamba kuna siku zinakwenda kwenye utekelezaji na wanaotekeleza ni watu. Kwa hiyo, lazima tujaribu ku-*feel gape* japo ninafahamu kwamba ziko kanuni zitakazokuja kujazia mapungufu yaliyopo katika Muswada huu. Lakini mfumo wetu wa utungaji wa Sheria katika nchi yetu bado sehemu kubwa ya sehemu zinazogusa maisha ya watu wetu, baada ya sheria hizo kupita hapa Bungeni unafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kupendekeza kuwa mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo kwamba Kamati imewia vigumu sana ku-*trace* hizi sheria ndogo kwa sababu hazijulikani. Ni vizuri basi kwa muundo wa sasa na kwa kisasa zaidi Waziri atakapotunga sheria ndogo, basi zipitie hata angalau kwenye Kamati ya Sheria Ndogo ya Bunge ili iweze kujiridhisha kama kweli zinakidhi na zinaishi kwa kutegemea sheria mama na Katiba kama ilivyo kawaida. Lakini kitendo cha Sheria Ndogo kuanza kutumika kabla ya kupitia kwenye ya Bunge, Bunge linakuja kustukia baadaye watu wameshaumia na linaonekana Bunge ndio lilitunga sheria hizo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna kitu kinatisha kidogo kwamba eti *inspector* huyu *where an inspector is certified that there is access livestock unit in a grazing land, he may order the removal of such number of livestock units so kept or grazed*. Lakini ya pili, anasema hiyo *removal* inatafsiriwa huku mbele kwamba ina-*include* pia ku-*sell*, yaani anaweza baada ya kuwa *certified* kwamba mifugo imezidi, akaenda Mahakamani akaomba *order* kwamba mifugo ile imezidi ipendekezwe na ambaye ni *expert* inasikilizwa upande mmoja ana akaenda ku-*implement*, mimi nadhani hii Sheria haijakaa vizuri katika eneo hili. *(Makofi)*

Kule vijijini tunafahamu hivi ni nani mtakatifu tunayemtuma aende akaangalie awe *certified* na aseme kweli hapa imezidi na lugha tunadhani ni hii tunayozungumza hapa? Kule watu watakwenda kunyang'anya tu mifugo ya watu. Lakini unasema pia kwamba itauzwa mifugo ya mtu, hii ni sheria ambayo inalenga utaifishaji na katika hii nchi hatuna sheria za namna hiyo. *(Makofi)*

Mimi nadhani sheria hapa inapaswa kubadilika. Pengine ingekuwa bora kama ingesema *section 2 the inspector may where any person fails to comply with an order made under sub section one apply to the court for an order to enforce the order*. Liishie tu pale, isiseme habari ya kwenda kuuza mali ya mtu. Sasa huko ni kutaifisha. Hii sio sheria ambayo itatusaidia na itatuletea mgongono mkubwa zaidi kuliko hali tuliyokuwa nayo wakati sheria hii inavyojieleza katika madhumuni yake, ni sheria iliyokuja kuwakoa wafugaji. Lakini mimi sidhani kama hapa watakuwa wanaokolewa kweli. *(Makofi)*

Jambo lingine ni la jumla, sheria hii imesemekana kwamba katika utekelezaji wake itazingatia *The Land Use Plan Act*, *The Village Land Act* katika utekelezaji wake. Hapa tunazungumzia habari ya vijiji na Halmashauri kutenga maeneo. Lakini kwa asili kwa kadri ninavyofahamu mimi ni kwamba maeneo ya nchi hii ambayo yanatumika kwa malisho, leo ni maeneo yaliyotokana na wakulima. Ni wakulima ndiyo waliotengeneza maeneo hayo.

Ninayo mifano ya jimboni kwamba ambapo sasa wafugaji wanagombana na wakulima, lakini wakulima wanadai maeneo hayo walifyeka wao zamani na waliyatumia kwa kilimo sasa wanataka kulima tena. Je, hatuoni kwamba kutakuja mgongano hapa? Lakini Wanasheria wenzangu watakubaliana na mimi kwamba bado katika nchi yetu tunatambua sana ile falsafa ya Mwalimu Nyerere *(The Mwalimu Nyerere Doctrine)* inayosema *the one who clears bush is the owner of that land.*

Sasa kama hivyo ndiyo na kama msimamo wa sheria hizi zipo na hii *Mwalimu Nyerere Doctrine* imetumika sana kuamua kesi nyingi katika nchi yetu na imesaidia sana kupunguza migongono ukiondoa zaidi ya pale tunapozungumzia habari ya *an exhausted improvement,* lakini hapa mimi nauona mgongona utakaokuja katika utekelezaji wa sheria hii.

Wakulima nao hawatakubali kuyaachia maeneo, kwa hiyo, vijijini huko tunapeleka vurugu. Tunapeleka vurugu vijijini, ni vizuri hapa tukasimama vizuri na tukaja na kitu ambacho kwa hakika kinakuja na mamlaka ya tofauti pamoja na kwamba kitashirikisha wananchi. Kwanza tutambue ardhi, pia tutambue mifugo kiasi gani tuko nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye tatizo kubwa ninalopata kwenye Muswada wa *The Livestock Identification, Registration and Tracesability Act* wa mwaka 2010. Hapa Muswada huu unakuja na kitu kinachoitwa *system* ya ku-*identify* na ku-*register* na ku-*trace* mifugo, lakini kipengele cha sita kinatisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezekano wa kufanyika vitendo kwa uhalisia wa hali inayozungumziwa hapa katika kifungu cha sita hauwezekani, wapo wafugaji nchi hii wana ng’ombe laki moja, kwa siku wanazaliwa ndama karibu hamsini kwa *rate* ya asilimia kumi ya wale mifugo. Sasa kila siku huyu atakuwa anafanya kazi ya ku-*register* nini, kufanya nini, mimi nadhani pengine jamani tusiwe tuna-*copy* tu sheria zilizotumika kwa wenzetu, tukiamini *situation* za kwao zinalingana na za kwetu. *(Makofi)*

Mimi naamini kabisa ufugaji au kuwa na mifugo sio laana ila ni baraka. Kama tumeshindwa kudhibiti, kama tumeshindwa kutafuta namna bora huko nyuma, tusidhani tutaweza kulimaliza tatizo hili la mifugo kuwa wengi nchini kwa kutunga sheria kali za namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii utekelezaji wake unalenga kuwaumiza zaidi wafugaji na pengine kuwafuta kabisa katika nchi hii, sasa tunajiuliza hivi wamekosa nini? Hivi mbona wenye magari hawaambiwi wa-*register,* Dar es Salaam pale *traffic,* magari yamejazana mtu mmoja ana magari kumi, mtu mmoja ana magari ishirini familia moja, lakini wenzetu Nigeria mtu haruhusiwi kuwa na magari zaidi ya mawili. Tuanze hebu na magari tupunguze foleni ya Dar es Salaam, sasa wafugaji hawa ambao maeneo ya ardhi ya Tanzania ukitoka Morogoro mpaka unafika Gairo pale kuna ardhi chungu nzima ipo ya bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli imefikia hatua kubwa ya kutisha hadi kufikia kuweka hatua ya namna hii? Nimeambiwa ni kengele ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Ya pili.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** nashukuru na naomba kuunga mkono hoja, lakini mambo haya yakizingatiwa nitaunga zaidi mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Simbachawene, anafuata Mheshimiwa Mahenge, Mheshimiwa Laizer jiandae na Mheshimiwa Ole -Nangoro.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii nikushukuru kwa kupewa nafasi ya kuchangia kuhusu Muswada huu muhimu, na nafasi ya kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu na hasa nataka kuchangia kwenye hii *The Grazing-Land and Animal Feed Resources Act, 2010* (Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Maeneo ya Malisho ya Mifugo, Vyakula na Biashara).

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeguswa sana kuchangia sheria hii, kwa sababu ya umaskini wa nchi yetu, kwa sababu ya umaskini wa nchi za Afrika ambao umepelekea nchi nyingi za Afrika au karibu zote kuingia katika karne ya ishirini na moja zikiwa bado maskini na zikiwa bado zinategemea misaada kutoka kwenye nchi zilizoendelea na naomba nirudie haya niliyoyasema kwamba baadhi ya sababu ambazo zimechangia sana nchi za Afrika ziendelee kuwa maskini na hatimaye kuingia karne ya ishirini na moja zikiwa bado maskini nitazitaja baadhi; moja ni masuala ya utawala mbovu *(bad governance);* ya pili ni masuala ya nchi za Afrika kuwa nyuma katika masuala ya sayansi na tekinolojia, na ya tatu nchi nyingi za Afrika ziko nyuma katika suala zima la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya nne mifumo ya fedha ya kidunia imewekwa kiasi kwamba haipendelei nchi za Afrika na haswa nchi zinazoendelea. Lakini ya tano ambayo nataka niizungumzie ni uharibifu wa mazingira na ya sita ni matatizo ya njaa katika nchi za Afrika, kwa sababu huwezi kufikiria suala la kuleta mabadiliko ya maendeleo kama watu wako wana njaa wakati wote. *(Makofi)*

Suala la njaa kimsingi, linasukumwa sana na vyanzo vya uharibifu wa mazingira. Sisi sote ni mashahidi, tunaangalia wazi jinsi mazingira yanavyoharibiwa, tunaona wazi jinsi ufugaji ambao hauzingatii maeneo yaliyotengwa, ufugaji unafanywa hata kwenye miji mikubwa kama ya Dar es Salaam na inapoteza mandhari hata ya mji. Tumeshuhudia usumbufu wa wafugaji ambao wametoka maeneo kama ya Usangu na kutoka maeneo mengine na yale mazingira kuharibika, tumeshuhudia wananchi wakihama kutafuta sehemu nyingine za malisho kwa sababu sehemu walizokuwa wanafugia kumekosekana maji au mifugo inakufa na wao wafugaji wenyewe kufa, lakini tumeshuhudia vile vile duniani maelfu ya watu wanakufa kwa sababu ya uharibifu wa mazingira unaopelekea ukosefu wa maji na ukosefu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tunaendelea kushuhudia kwamba mamilioni ya watu mpaka tunavyoongea sasa hivi wanahangaika, kutafuta maji au kutafuta chakula ambayo imetokana na uharibifu wa mazingira, hii ndio hoja yangu ya msingi, nilidhani ningeiona kwenye sheria hii kwamba imejitokeza, ingawa yote yanayoongelewa kimsingi yanahusu ulinzi wa mazingira, lakini sheria haijaainisha na kuelezea hili, umuhimu wa mifugo katika yale mambo ambayo ni mazuri, *positive effects* kuziendeleza na katika yale mambo ambayo ni *negative* kuziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna mtu mmoja alinitania akaniambia inaonekana kama vile wanadamu wamefukia vichwa kwenye mchanga kwa hiyo, kiwiliwili kiko juu na hawaoni kinachotokea kuhusu mazingira duniani kwa sababu hali ni mbaya sana kwa kweli.

Kwa hiyo, nataka kuongelea kuhusu umuhimu wa sheria hii jinsi inavyoainisha idadi ya mifugo kwenye maeneo husika inapokuwa imezidi, madhara yake ni nini. Tunashuhudia kwamba pale panapokuwa na idadi kubwa ya mifugo kwenye eneo ambalo pengine halistahili kuwa na idadi hiyo, ni wazi tunashuhudia kutakuwa na mmomonyoko wa udongo. Ni wazi tutashuhudia kwamba ile ardhi inaanza kuwa ngumu na vile vile haiwezi kuchukua maji na kuweza kuyahifadhi. Lakini tunashuhudia rutuba ya ile ardhi inapotea kwa sababu ya wanyama wanakuwa wengi kwenye eneo ambalo halikutegemewa kwa hiyo, naomba kwamba sheria hii tungetegemea kwamba iweze kusimamia yale mazuri ya ufugaji, *biodiversity* na yale mabaya ya ufugaji iweze kuyapunguza ili kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea hilo, la pili naungana na wenzangu kabisa kwamba sheria na hasa kwenye vipengele vya *inspector* imempa madaraka makubwa mno ambayo nimekuwa nikijiuliza kwamba ni namna gani huyu mtu anaweza akafanya kazi, akafanya maamuzi yeye pekee yake na kufikia hayo maamuzi kwamba au mifugo ipunguzwe au anaweza akaingia sehemu yoyote na kufanya ukaguzi na kwamba yeyote atakaemuona akikagua akamsumbua basi atakuwa amevunja sheria na anaweza akachukuliwa hatua za kutosha. Kwa hiyo, nadhani hilo ni la msingi kwamba ni lazima sheria hii pengine ingetakiwa ipitiwe kwa undani zaidi ili iweze kubaini vile vifungu ambavyo vinawakinza baadhi ya wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda ukurasa wa tisa kwenye sheria niliyoisema kifungu cha nne kuhusu ile *council composition* yake, ukiangalia kwenye Muswada inaelezea sana kuhusu wataalamu ambao ndio wanatakiwa wawe ndio ma-*inspector* na ambao watakuwa wamesomea fani za mifugo kutoka Vyuo Vikuu kama vya *Sokoine University of Agriculture*, lakini kwenye *composition* hakuna mtu hata mmoja kutoka *higher learning institutions* kwa hiyo, nilikuwa napendekeza ili kuweza kuwa na mtaalamu ambaye anaweza akaangalia hivyo vyeti, hao wataalamu ambao wana *degree* moja au mbili basi ni lazima kuwe na mtu kutoka vyuo vya elimu ya juu kama *Sokoine University of Agriculture* ambao ndio wanaofundisha hao wataalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nilikuwa napendekeza na nimefurahi kuona kwamba kuna mwakilishi kutoka *TBS* ambao ndio wanatengeneza viwango vya

mazao mbalimbali kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwa *TBS* kazi yao kubwa ingekuwa basi kuwawezesha wawe na maabara za kutosha zenye uwezo na vifaa ili kuweza kuweka viwango kwa ajili ya mazao ya mifugo kama maziwa, ngozi, vyakula mbalimbali kama *sausage*, *cheese* zinazokuwa zinatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ukienda ukurasa wa kumi, sehemu ya 6(c) inasema kwamba *functions of the director shall be to liaise with the Tanzania Bureau of Standards in setting standards on animal feed resources.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hapa sio sahihi kwamba huyu Mkurugenzi yeye ndiye ana-*set standards*, *standards* wana-*set TBS*, *Tanzania Bureau of Standards* kwa hiyo apeleke labda *data* kule ili wale waweze kuanda vile viwango na pengine kule *TBS* ndio kunatakiwa kuwe na wataalamu wa haya maeneo ya mifugo ambao ndio watashiriki kwenye kuanda vile viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Uendelezaji, Ukuzaji na Usimamizi wa Malisho. Nilikuwa nadhani hapa suala la msingi pengine baada ya hii sheria kuipitisha basi iandaliwe sera, iandaliwe *policy* ambayo itaeleza vizuri sasa yale mazuri ambayo yanaweza yakahifadhiwa kwenye suala zima la ufugaji na yale mabaya ambayo yanatakiwa yasimamiwe kwenye suala zima ambao ni ufugaji lazima yaende kwa pamoja, huwezi ukaliongelea moja la ufugaji wakati unajua kuna suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na mazao ya mifugo na nafurahi kuona Sheria imeliangalia hilo na kwa sababu sasa hivi tunazo bidhaa nyingi za mifugo ambazo hatujui zinatengenezwa wapi, hatujui zina viwango vya aina gani lakini zimesambaa katika masoko. Kwa hiyo, tunadhani hii Sheria kwa usimamizi huu inaweza ikasaidia. Utakuta kwamba kuna maziwa yanauzwa yako katika kiwanda gani, katika hali gani kile kiwanda, mwenye nacho ameki-*register* au vipi hatuwezi kujua na hii inaweza kuwa hatari katika maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho tunalo shamba la ng'ombe pale Kitulo na shamba hili tulikuwa tunadhani kwamba kwa kuwa lina wananchi wanaozunguka lile shamba, hususan kata za Matamba, kata za Magoma, kata za Mlondwe, kata za Kitulo kwamba basi wangetumia fursa hii kuwawezesha wale wananchi na hasa ukizingatia hali halisi ya mazingira ya Makete kwamba wanaozunguka lile shamba waweze kuwezeshwa kupata wale ng'ombe na kwa kutumia wataalamu waweze kuwafuga ili kuwainulia kipato chao na hii pengine ingewapunguzia kuwa na ng'ombe wengi ambao pengine faida yake inakuwa ni ndogo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu ambao ni muhimu sana na niseme inanigusa mimi, niko miongoni mwa wafugaji ambao Muswada huu unanigusa.

Na niseme tu Muswada huu nilitegemea sana sana ungezingatia utawala bora na haujazingatia.

Muswada huu nilitegemea usiwanyanyase wafugaji na unawanyanyasa sana na Muswada huu nilitegemea wafugaji wangeshirikishwa na haswa wale wachungaji mnaosema wachungaji na hawajashirikishwa, walioshirikishwa ni wafugaji wa *zero grazing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zote hizo tatu au nne nasema siungi mkono Muswada huu na nikiunga kwa kweli itakuwa nimewasaliti wafugaji na sitegemei hata Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi sitegemei nao watakuwa tayari kuwanyanyasa wapiga kura. Wafugaji ninaowasemea hapa ni wapigakura wakubwa wa Chama cha Mapinduzi, hawajawahi kupigia chama kingine chochote. Kwa hiyo, nathubutu kuwatetea hapa kwa sababu ndio wamenileta hapa na nategemea hata Serikali watatusikiliza kwa sababu ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na alama ya mifugo; kwa watu wengine ambao sio wafugaji wanaweza kusema jambo la alama za mifugo ni jambo rahisi, lakini sio rahisi. Ukiwaambia wafugaji waache alama zao za kimila, hawatakubaliana, mimi mwenyewe ninayesimama hapa sitakubali, kwa sababu ni alama za jadi, za ukoo, ukoo wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda Kenya nikiona mifugo ya ukoo wangu natambua hawa ni wa ukoo wangu. Hata kila mahali tunaposafiri na Kamati yangu wanashangaa ninapowaambia hawa mifugo ni wa ukoo wangu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ukija kuwaambia kwamba hizo alama zisitumike haitakubalika moja kwa moja. Jambo lingine ni namna ya kutambua, mmeandika rangi, kwa wataalamu rangi za mifugo wanaweza wakasema ni rangi nne tu nyeupe, nyekundu, nyeusi na yenye mchanganyiko wa rangi. Ni rangi hizo nne tu, lakini kwetu kwa wafugaji tuna zaidi ya rangi sitini na kila moja inatambuliwa kwa jina lake. Sasa kweli katika Muswada huu haupo kwa sababu ule weupe sisi tunachanganua rangi nyeupe zaidi ya nne, nyeupe tu hata nyeusi. Sasa ukituambia kwamba nyie mnatambua kwa rangi sisi tunawashangaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni *property* ya mtu kwamba *property* yake anawekewa *limit*, lakini mfugaji tu katika nchi hii ndio anawekewa *limit* ya *property* yake kwamba wakifika idadi kadhaa lazima wapunguzwe, hivi mkulima amewahi kuwekewa *limit* ekari anazolima? Hana *limit* au kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Simbachawene magari yamejaa mpaka wengine wanatamani kwenda ofisini kwa miguu, hivi nani amepewa *limit* kwamba lazima uwe na magari manne au matatu? Au wakati mwingine hata *limit* ya fedha, kwamba usiwe na fedha kiasi gani, hata *limit* ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wafugaji, nilichogundua hata mlipoweka wakati ule kusema wahamishwe sehemu fulani ilikuwa ni utaratibu wa kumaliza mifugo na mifugo isiwepo tena Tanzania nikaona sasa wameleta Sheria ya kujaribu kupunguza mifugo wala sio upunguzaji, ni unyanganyi. Unasema kwamba baada ya kufika idadi fulani kwa huyo *inspector* eneo la mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu eneo la mifugo kama kule kwangu kuna eneo moja vijiji nane vinatumia eneo moja la malisho, sasa unaposema wakizidi pale huyu *inspector* ataenda kupunguza, kwanza apunguze eneo la kijiji kipi na apunguze eneo la nani? Hivi anaweza tu akaamua akaenda kwenye boma la mtu fulani akasema kwamba mifugo ipunguzwe, kwa hiyo, nasema kwamba ndugu zangu, Wabunge wenzangu hatuko hapa kupitisha Sheria za unyang'anyi na hii ni Sheria ya unyang'anyi haijafuata utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kutafuta kibali unaposafirisha mifugo, niseme wakati mwingine kiangazi kina kuja mpaka unashindwa, huna nafasi ya kukimbia kwenda kutafuta kibali. Halafu unapokwenda kutafuta kibali unanyimwa, ni lazima unyimwe na kijiji unachohamia, hivi utabaki kufa? Na bado Katiba inasema kwamba Mtanzania ana uhuru wa kwenda popote, lakini uhuru wa Katiba, mkulima anaruhusiwa, mchimbaji madini anaruhusiwa, lakini mfugaji tu ndio anawekewa Sheria asitoke na hawa mabosi wakubwa wanaoitwa wawekezaji ndio wanaruhusiwa watengewe sijui ekari milioni arobaini ya wawekezaji na mtambue kwamba kila siku Hifadhi za Taifa zinaongezwa na kumegwa ardhi ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi niulize nyumbu walioko Serengeti na walioko Simanjiro, hivi nani kasema kwamba mmeweka *limit* kwamba nao wapunguzwe? Pundamilia waliojazana kule kwangu katika eneo hilo hilo la wafugaji na kumaliza majani na kuleta magonjwa mmeweka *limit* kwamba wapunguzwe? Kwa nini iwe ng'ombe wa mfugaji tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati mwingine huu usajili wa mifugo unakwenda kusajili mifugo, hivi imekuwa silaha? Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Simbachawene inawezekana nikiwa hapa Bungeni ndama mia moja wamezaliwa na wakafa baadhi na kila siku hasa kipindi hiki mifugo imeisha, kwa hiyo, ndugu zetu wanazunguka kwenda kuomba mifugo. Kwa hiyo, hivi unakimbia kusajili kwanza suala la *clinic* limeshindikana kule kwetu *clinic* tu, mpaka Serikali ikawa inatoa *mobile clinic*; wataalamu ndio wanazunguka kwenda kufuata. Kama hiyo *clinic* ya watoto imeshindikana ndio usajili wa mifugo ukimbie barabarani kila siku unakimbia kwenda kusajili?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiweke Sheria ambazo hazitekelezeki, nitoe tu mfano Sheria tuliyopitisha hapa Bungeni ambayo mpaka sasa haitekelezeki, tulipitisha mwaka 2003 kwamba hairuhusiwi tena mifugo kwenda mnadani kwa kutembea, wabebwe kwa malori, mpaka sasa kwangu mifugo inatembea kwa sababu hakuna magari, wala hakuna barabara.

Sasa hiyo Sheria iliyowekwa ni Sheria ambayo haitekelezeki, tangu tulipoipitisha mpaka leo, mpaka mwaka 2020 haitekelezeki. Kwa hiyo, nasema kwamba baadhi ya Sheria tunazozipitisha hapa ni kwamba hazitekelezeki, moja yao ni hii. Sheria kusema kwamba *inspector* atauza mifugo au ataomba *order* ya Mahakama, hivi *order* unapoenda Mahakamani kupunguza ng'ombe wa mtu ambaye hana hatia, wa kijiji ambacho hakina

hatia sio wizi? *Order?* Hivi kweli sisi bado ni watu watunga Sheria au ni wanyang'anyi, hiyo ni kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo moja naungana na ndugu yangu Mheshimiwa Ole-Sendeka, nasema siungi mkono Muswada huu, Miswada yote miwili na iahirishwe mpaka iboreshwe zaidi. Kwa hiyo, napenda kurudia kwamba siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika mjadala wa Miswada hii miwili iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kwamba nilipokuwa natazama hii Miswada yote miwili nikafikiri kilichofanyika ni *templat*e, imechukuliwa ya mwanafunzi anayeandika *Ph.D Thesis* kwenye Chuo Kikuu kule Texas anayefanya mambo ya *ranching* nadhani ndiyo Sheria hii ikatungwa kwa kutumia *model* ambayo ni ngeni na kutumia mifano na kupendekeza vitu ambavyo kwa kweli ni vigeni sana katika mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama kijuu juu unaweza ukaona ni Sheria kama Sheria nyingine. Lakini kwa kuelewa hali yetu halisi ilivyo hasa vijijini kama wengine walivyosema, maeneo mengi vijijini imeshindikana tu kuwasajili watoto wanaozaliwa na wengi hawana vyeti vya kuzaliwa kwa sababu ya kukosa huduma za msingi na kwa kuwa hakuna *facility* zinazohitajika na huu ni ukweli nadhani hakuna yeyote atakayebisha katika jengo hili na kama watu kwa maana ya watoto tumeshindwa kuwasajili japo ni haki yao. Tunapoongelea sasa kuwasajili ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na katika maeneo yetu mengi kwa kweli hakuna karatasi, hakuna kalamu *illiteracy levels* ni juu.

Kwa hiyo, nadhani turudi kwenye ukweli wa hali halisi na kusema kwamba kwa kweli Miswada hii yote miwili inatetea maslahi ya nani, inazingatia *reality* ya nani? Maana kama ni madai ya soko labda ni soko ambalo tutaliendea kule mbele, lakini si kwa sasa, maana hatujafika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kama lengo ni *commercial ranching* tubainishe, Muswada utungwe kwa ajili ya ranchi zilizoanzishwa kwa sababu ya kuchukua tu mifugo kama zao na kukazania taratibu za kibiashara. Maana ranchi labda itaanzishwa kwa kuzingatia *parameters* ambazo zipo humu. Lakini kwa ufugaji wa kawaida nadhani ni mzigo mkubwa na kama tunavyoelewa kwamba kila Sheria ni lazima itetee na izingatie haki ni lazima pia iwe ni *reasonable* na ni lazima iwezekane kutekeleza mapendekezo yaliyopo huku, ninaogopa kusema kwamba kwa kweli si rahisi yawezekane kutekelezwa katika mazingira yetu.

Kwa hiyo, nikirudi katika Muswada huu, nianze na huu wa malisho, kama eneo la *interpretation* walengwa wa msingi wameachwa kwa sababu wafugaji kwa maana ya *livestock keepers* hawakuguswa katika *interpretations* na hizo *definition* zilizotolewa, *pastoralist* kwa maana tunayoielewa hawa hawakuguswa, *agro-pastoralist* hawapo

kwenye *definitions* na hawapo pia kwenye hizo *interpretations.* Kwa hiyo, hapa pana upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikija katika ibara ya nne kwenye Muswada huo wa malisho tunaongelea *Council* lakini zaidi hii *Council* imekuwa inazingatia ushauri zaidi. Lakini hapo hapo kuanzia Ibara hiyo ya 16 hadi ya 20 tunaongelea maeneo ya malisho yanayohitaji kuwa *managed* kwa maana ya *grazing resources.*

Kwa hiyo, ningedhani kwamba kuna haja ya hiyo *council* pia kupewa *function* nyingine kwenye *function* za *council* ili pia iweze kuwa na hiyo kazi ambayo ni *managerial*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 18(2) tunakuta kwamba Sheria inayopendekezwa inakinzana na Sheria ya sasa ya vijiji ya mwaka 1999. Maana tayari hapo kuna tatizo kwamba haiko *harmonized* na Sheria zingine ambazo zipo kule kijijini na eneo hili linahitaji kutazamwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye sehemu ya 19 inaongelea kufanya *inventory,* kwenye maeneo ambayo tunaongelea sasa kufanya *inventory* ya *grazing resources* lakini hata *inventory* ya mifugo ni ya tangu mwaka 1984 ndiyo nadhani tuna sensa ya mwisho, hesabu ya mifugo ilipofanyika kwa mara ya mwisho. Kwa hiyo, nadhani kwamba kuna maeneo ambayo tunahitaji kuyatazama kwa ukaribu zaidi tukaunganisha na hali halisi ili Sheria hii iweze baadaye kuja kuwa ya manufaa kwa wafugaji, vinginevyo ikibaki hivi itakuwa ya manufaa kwa watu wanaoanzisha ufugaji kwa maana ya *commercial ranching* lakini si kwa wafugaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika Sheria hiyo nyingine ya *livestock identification* nadhani hapa kuna matatizo makubwa. Wenzangu wameshaeleza na kijadi kila jamii inayofuga wanakuwa na namna ya kutambua mifugo yao. Alama zipo na si alama tu, kunakuwepo pia na uelewa wa jamii juu ya alama hizi. Tutakapokuwa tumependekeza sisi alama ni ngeni hizi zitakuwa na ufahamu kwa watu gani. Maana tunaongelea *numbering* labda tunaongelea *codes.* Uwe na *code* moja ya nchi, *code* ya Mkoa au *code* ya Wilaya. *Code* nyingine itakayokuwa sijui ni ya mfugaji na kama mfugaji ana wake kadhaa, utakuwa una-*code* kwa kila kaya na kwa kila ng'ombe labda na ukoo wa huyo ng'ombe maana ng'ombe nao huwa wana koo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani haya hayawezekani na ni busara tu tuanze kufikiri na kuona kwamba *practicality* ya hiki tunachokipendekeza kwa Tanzania ya leo *practicality* yake kwa kweli ikoje? Kwa hiyo, busara nadhani ingetuma kwamba tujaribu moja kushirikisha wadau wengi wafugaji. Lakini kushirikisha kule na siye kama Serikali tukajifunza mengi ambayo bado hatujawahi kuyafahamu.

Mheshimiwa Michael Laizer ameongelea mambo ya rangi, na rangi kwa kweli nilipokuwa najaribu kujifunza jinsi wafugaji wanavyotambua vitu, kwa upande wa rangi tu nikakuta kwa urahisi wanakuwa na njia 44 za kueleza kuwa huyu ng'ombe ana rangi za aina gani. Ukija kwenye sura tu ya pembe zilivyokaa, ama muundo wa mwili wa ng'ombe kunakuwa na njia nyingine nyingi karibu 68 na hii ni taaluma ambayo nadhani

tukiri tu ingewezekana na sisi tukajifunza ili katika kufanya *identification* tu-*harmonize* na tu-*integrity* hiki kilichokuwepo kijadi, kimila na kinachofahamika kwa watu wengi na mengine ambayo tutajaribu kuyapendekeza ili kuboresha mfumo mzima wa *identification.* Lakini *identification* ikitokea kuwa alama zitakazotumika zote ni ngeni, ujuzi utakuwa wa watu wageni, labda kwa manufaa ya watu wageni, mahali fulani tutajikuta kwamba hawa walengwa wa Muswada hawakutendewa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningependekeza kwamba mtoa hoja kwa unyenyekevu nadhani labda angekubali ifanyiwe kazi zaidi ili tuweze kuboresha. Lakini katika kuboresha kule tuanze kufikiria pia na *logic* ili kile kilichoandaliwa hasa Kwa aijli ya *commercial ranching* tuanze kufikiria kwa sasa. Tumekuwa tunatumia mifano mingi ya Botswana. Lakini Botswana wao wamewekeza kabla hawajaja katika *regulations* za kisheria. Sasa sisi tunataka kutangulize *regulations* na Sheria kabla hatujawekeza chochote katika sekta hii ya ufugaji. Nadhani tunapaswa kwenda kwa utaratibu zaidi ili mazingira kama wengine walivyosema yaweze kuandaliwa vizuri kusudi Sheria itakayowekwa iweze kuwa ni *functional identification* zaidi kuliko kubaki na Sheria itakayokuwa kwenye *shelves* lakini kwenye mawazo ya wafugaji na kwenye watumiaji wa Sheria hiyo kitu hakitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, labda hili lingesaidia zaidi kazi ikifanyika zaidi lakini kuweza pia kutunga Sheria kwa sababu *logic* nadhani ya kuwa na Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 kwa upande wa ardhi ilikuwa ni ugumu wa kuwa na Sheria moja inayojumuisha mahitaji ya ardhi katika ngazi ya vijiji na ardhi ya jumla. Isingekuwa vibaya pia nadhani tukijaribu ku-*borrow,* nadhani kuazima pia wazo kutoka kule la kutenga ili tuwe na Sheria ambayo itakuwa ina-*restrict regulations* kwa wale wanaolenga sana ng'ombe kama zao la kibiashara hasa kwa maana ya *commercial ranching* lakini pia tukawa na sheria nyingine ambayo zaidi itawalenga wale watu wafugaji wanaoishi katika mazingira ya vijiji ambako hata ukisema kwamba ni kuhesabu kufanya *registration* hakuna *facilities* na watu wengi hawatakuwa na huo uwezo wa kufanya haya tunayotaka.

La mwisho katika upande huu wa hii *livestock identification* kwenye *article 24* imeongelea suala la gharama na ni vizuri nadhani Serikali isijaribu kuwa na *externalities* katika kitu kama hiki. Shuhuli zote za gharama zibebwe na Serikali huenda wengi kati ya wafugaji hawakuandaliwa kwa kukabiliana na gharama kama hizi kwa wakati huu. Lakini pia *article 25* inahitaji kutazamwa kwa sababu viwango vya faini ambayo vimewekwa mle ni juu mno, nadhani hii pia hailingani na mazingira ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema kwa sura ya Sheria ilivyo, Miswada yote miwili siwezi kuunga mkono yoyote kati ya hii Miswada miwili. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Nangoro. Sasa nimwite Mheshimiwa Kaika Telele.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

**NAIBU SPIKA:** Samahani na Mheshimiwa Selelii ajiandae.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Na mimi niweze kusema kidogo kuhusiana na hii Miswada miwili. Nina ombi kwamba katika Bunge lijalo kama Mwenyezi Mungu atatujalia kurudi, wakati wa kutengeneza Kamati za Kudumu za Bunge hii Kamati ya Mifugo imekuwa na wafugaji wachache sana katika Kamati ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya tuko wawili au watatu na unaweza ukakuta wakati wa Kamati kule Dar es Salaam tusifike wote kwa wakati na hasa hao ambao wanahusika na mifugo moja kwa moja.

Mimi ni mjumbe katika Kamati ile na kwa bahati mbaya sana nilichelewa kufika, nilishiriki siku moja yakatokea matatizo kule Ngorongoro - Loliondo nikakimbia kurudi nikawakuta wenzangu wamekwenda mbali kidogo. Kwa sababu mambo mengine ningeweza kutoa tahadhari kule katika Kamati na pengine mambo yasingekuwa mabaya sana humu ndani. Kwa hiyo, nitakachowaomba ndugu zangu na hasa Mwenyekiti wangu wa Kamati asinione kama namsaliti leo. Kwa sababu kwa kweli nimefika mahali katika kuchambua Muswada huu na mimi sitaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakwenda moja kwa moja kwenye alama na ndugu yangu Mheshimiwa Laizer ameeleza vizuri. Hizi alama za asili za mifugo kwa kweli hakuna namna na sidhani kama Sheria imesema kwamba sasa hii *identification, registration, traceability* itaondoa alama za wafugaji wa asili. Sijaona kama ni kitu cha Kitaifa, hizi alama za kiasili zitakufa kifo cha kawaida. Kwa sababu mimi nakumbuka katika miaka ya 1970 na 1980 wakati ule kulikuwa na wizi mkubwa sana wa mifugo hasa katika Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Mara na katika Jeshi la Poliksi kulikuwa na kitengo kilichojulikana kama *STPU* na kirefu chake ni *Stock Theft Prevention Unit*, ilikuwepo kitengo hicho miaka hiyo. Kwa kweli walifanya kazi nzuri na kubwa kipindi kile na hata kutokana na matatizo ya wizi wa mifugo ng'ombe wa Ngorongoro kwa mfano, walikuwa wanapigwa chapa ya *NGOR* na kwa sababu Ngorongoro ipo Mkoa wa Arusha ikawekwa *AR* halafu inafuata Tanzania *(TZ).*

Sasa ile ilisaidia lakini hiyo haina maana kwamba alama za asili za wafugaji wa asili zilifutwa; zilisaidia sana katika kudhibiti wizi na alama hizi ambazo tunaweka sisi kule nyumbani ya kutambulisha ukoo wa Laizer, ukoo wa Mollel, ukoo wangu mie. Mimi sitawaambia, mtatafuta baadaye, mtamwuliza Laizer. Lakini hizi zilisaidia sana kokote waliko Wamasai hawa, iwe Tanzania, iwe Kenya, iwe mahali popote akienda atajua hawa ng'ombe, huyu ng'ombe ametoka mahali fulani kama ameibiwa atawasiliana na ndugu zake. Huyo ng'ombe atarejeshwa alikotoka. Kwa hiyo, nataka niulize swali kwamba mifumo ya asili inayotumiwa na wafugaji wa asili itaoanishwa vipi na huu mfumo wa utambuzi wa Kitaifa ambao sasa tunaka kuuweka?

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo wanakoishi wafugaji, yamepakana na maeneo mengine mengi tu yanayotawaliwa na Sheria zingine ambazo zimepitishwa na Bunge hili. Kwa mfano, wafugaji wanaopakana na maeneo ya wanyamapori kuna Sheria ya

Wanyamapori ambayo tumepitisha mwaka jana au mwaka juzi 2008 nadhani, lakini kuna Sheria pia ya misitu ya mwaka 1998, kuna Sheria ya Ardhi na Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Tunayo *The National Park Act*, kwa maana ya maeneo ambayo hawa wafugaji wanaishi. Lakini maeneo haya kuna mambo ambayo Sheria zilizotungwa na Bunge hili zinasimamia maeneo yale. Lakini ukiangalia hii Sheria haijasema sasa inapotokea pengine kukinzana na Sheria hii ambayo tunataka kupitisha leo ni Sheria ipi inachukua nafasi ya kwanza? Hilo halijasemwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Ngorongoro, yule mtu tunayemsema *Inspector* anaeonekana kupewa madaraka makubwa katika Sheria hii. Kwa kweli kama hatatumia busara yatatokea matatizo makubwa zaidi na nashukuru kwamba hilo limeonekana na kipengele hicho kitarekebishwa. Ndiyo maana wakati ule tunapakana eneo lile la mifugo kuna mifugo fulani imeondolewa kule, tena kwa hali ambayo siyo sawa sawa ni haya mambo ya kupitiliza ya kukamata sheria kwa mtu mmoja au wawili na kutumiwa tofauti na inavyotakiwa. Ukiangalia maudhui ya Sheria hii ya kwanza kwamba malengo yake ukiangalia kwa makini siyo mabaya. Kwa sababu inajaribu kuainisha mfumo wa Kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo ili kukwepa tatizo la wizi wa mifugo ili pengine kuondoa au kupunguza maradhi au magonjwa ya mifugo.

Lakini watu wamezungumza hapa kwamba tumetunga Sheria ya usafirishaji wa mifugo kama wanakwenda mbali zaidi tutumie magari badala ya kuwaswaga kwa miguu. Lakini hilo halifanyiki na kwa hiyo, Sheria hiyo haifanyi kazi kwa sababu kama walivyosema wengine hakuna barabara wala magari ya kubeba ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inapaswa kuwa shirikishi na kama alivyosema ndugu yangu mmoja kwamba kwa kweli kuwashirikisha wadau ambao siyo wale *pastoralists* kabisa, wenyewe wa vijijini, hawa wengine wanaweza wakatusaidia tu mambo fulani fulani. Lakini wale wenyewe kabisa ambao kazi yao ni hiyo kila siku ukienda kulala ukiamka ni kazi ya mifugo hao nao tungewatafutia nafasi wangekuwa na mchango katika dhana tunayosema tuthamini *local knowledge* katika masuala fulani fulani. Siyo hii tu ya *academic* tunasoma, tunakuwa na ma-*Ph.D* lakini *the local knowledge also has got a role to play.*

Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba Sheria hizi mbili kwa kweli kwa kipindi hiki zingeahirishwa bila kupitishwa ili tuendelee kuangalia kwa makini zaidi kwa sababu tukipitisha haraka haraka hivi kwa kweli watu wengi na hasa wafugaji wale wa *grassroot*, wa *level* ile ya chini kabisa wataumia na hawatakuwa na mahali pa kukimbilia baadaye, wataambiwa tu basi ninyi bahati mbaya hii Sheria imetungwa na Bunge ilipaswa kuonekana na Bunge matatizo ya Sheria hii lakini sisi tumepewa kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona Sheria zote mbili tuendelee kupata nafasi ya kutafakari ili tuweze kupunguza matatizo ambayo kwamba tunafikiri yangeweza kutokea tu kama tukipitisha Sheria haraka haraka. Kulikuwa na matarajio ambayo tungepitisha Sheria hii tarajio la kwanza tungeona kwamba kulinda maeneo ya malisho

ya mifugo, lakini tunakuja kuona Sheria hizi kwa kweli hatutalinda badala yake kwa kweli inaonekana maeneo ya wafugaji tutaendelea kuwapora tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya wafugaji kwa muda mrefu kwa kweli yameendelea kuchukuliwa na Serikali kwa manufaa mengine ya Kitaifa. Lakini watu wanapopita maeneo wakaangalia kuna eneo kubwa tu wanadhani halina mwenyewe lakini kumbe kwa kweli kwa sababu tunakuwa na mifugo mingi tunahitaji eneo kubwa. Na Sheria hii vilevile haikusema kwamba ukikadiria kwamba mifugo kiasi hiki italisha katika eneo hili lakini wakati wa ukame kama mwaka jana kwa mfano, majani yakawa yamekwisha kabisa katika eneo lile. Mifugo italazimika kuondoka tu kwenda mahali pengine kutafuta malisho. Sasa ndipo hapo sasa wataingia migogoro wafugaji na Sheria hii na watekelezaji wa Sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niishie hapo. Sitaunga mkono Sheria hii, naomba irejeshwe katika Kamati husika na tukaangalie huko kwa makini ili tuweze kuwatendea haki wafugaji. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Lucas Selelii halafu na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu atakuwa msemaji wa mwisho.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kusema juu ya jambo kubwa ambalo kwa kweli litaonyesha mustakabali mkubwa sana kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kuwashukuru wenzetu wa Wizara, kuwashukuru wenzetu wa Kamati inayoangalia Wizara hii kwa jinsi ambavyo walivyochambua na kuamua kuja na Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ukiusoma una pande zote mbili. Ukiuangalia una maelezo ambayo yanaweza kutupeleka kuzuri sana lakini vilevile una pande ya pili ambayo inatupeleka ambako si kuzuri. Sasa nisingependa kwenda moja kwa moja katika kuelezea mazuri, wenzangu wameshayasema mengi inatosha na mimi ningeomba tu Waziri John Magufuli pamoja na mwenzake, waone busara ambayo inaonekana kwenye Bunge hili kwamba wao siyo wa kwanza ni vizuri wakarudi kwenye Kamati yale yanayosemwa na Wabunge yakachukuliwa ili kurekebisha matundu mengi ambayo yanaonekana yapo katika Muswada huu, si jambo ambalo ni la ajabu, tumelifanya katika Miswada mingi mbalimbali ya Sheria. Kwa sababu unatunga Sheria ambayo ni ya watu. *(Makofi)*

Sheria hii inawahusu watu wengi, lazima uangalie na wakati wenyewe. Wanasema waswahili, kumchinja kobe inahitaji *timing* lazima umwelekezee kidole, akiking’ata umchinje. Sasa muda wa kuchinja wafugaji sio huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii ni kubwa sana na wafugaji ni wengi sana na mifugo tunayo mingi sana. Kwa bahati mbaya, mifugo hii kwa jumla hatujaichukua tukaiweka kwenye utaratibu rasmi wa kutuletea mapato katika Taifa letu. Haijawa na

manufaa makubwa sana hata kwa wafugaji, haijawa na manufaa makubwa sana hata kwenye Pato la Taifa. Kwa hiyo, naaamini kwa yale mazuri ambayo yamepangwa yakija vizuri zaidi yakapangiliwa basi inawezekana siku zijazo Tanzania itakuwa ni nchi ambayo inatoa pato zuri kwa wafugaji na vile vile inatoa pato zuri kwa Taifa vile vile. Mifugo ni utajiri, kule kwetu mifugo ni kama benki. Wakulima wengi wanapopata mazao yao wanauza yale mazao kwa sababu hawawezi kupeleka benki. Benki yao ni kununua ng'ombe, mbuzi au kondoo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa wakulima wa kwetu ili awe mkulima sahihi kabisa lazima vile vile awe ni mfugaji. Ufugaji ni pesa, ufugaji vile vile ni kinga hata ya njaa. Wanatumia mazao ya mifugo wanapokosa chakula kuuza ili wanunue chakula. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kwa wakulima na wafugaji ni jambo ambalo ni la sifa ya pekee kwamba umekamilika kama binadamu na ina heshima yake kule kwetu wanaitwa basavi. Anaweza kuwa ni mkulima, lakini akaitwa mkulima tu, lakini akiwa na ng'ombe akawa na mbuzi, anaongezeka hadhi anaitwa nsavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nsavi maana yake ni tajiri. Nsavi maana yake ana uwezo, uwezo umetokana na kuwa na mifugo, uwezo umetokana na kuwa na ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kwa hiyo, tunapozungumza suala hili ni jambo ambalo linawagusa watu wengi sana. Sasa mimi ningeenda moja kwa moja kwenye changamoto ambazo nimeziona ambazo ingefaa tukazirekebisha ili hawa wafugaji wetu, basavi wa nchi yetu waweze kunufaika na Muswada huu ambao tunategemea kuutunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ni kubwa mno na mifugo ni wengi sana. Kufanya jambo hili hata kwa mwaka mmoja haiwezekani, sembuse kwa siku saba ambazo tunapewa hapa ni kitu ambacho kwa kweli changamoto hii haiwezekani na ni jambo gumu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona Muswada huu ni mgumu, mimi naona Muswada huu hautekelezeki. Changamoto ya pili, wafugaji walio wengi wa hawa ambao tunawazungumzia basavi, ni wafugaji ambao elimu yao ni ya chini. Kwa hiyo, kuwaelimisha jambo hili hata ungetumia Kiswahili tu inawezekana wasikuelewe, lazima utumie hata lugha zao za kienyeji. Huwezi ukaeleweka kwa wafugaji wa Kimasai kwa kutumia Kiswahili pekee, hauwezi kueleweka kwa wafugaji wa Kisukuma kwa kutumia Kiswahili peke yake. Lazima elimu iende zaidi ya Kiswahili kwa kutumia lugha zao za jadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wingi wao na elimu waliyo nayo ya chini lazima twende zaidi ya hapo, tuwe makini sana. Lingine ni uwezo wa Serikali uliopo katika ngazi ya Halmashauri zetu. Sisi wote ni Madiwani hapa, *mechanisim* ambayo inatakiwa kutumika hapa ni Halmashauri zetu za Wilaya. Je, tunao watumishi wa kutosha kuwafikia wafugaji wote walipo sehemu zote? Je, tunayo magari na nyenzo za kutosha kuwapa wafugaji wote kote kule waliko? Haiwezikani, kama tumeshindwa kusajili watoto, kama tumeshindwa kusajili hata wananchi, sembuse mifugo, ni jambo ambalo haliwezekani. Kwa uwezo wa Serikali iliyopo kwa maana ya Halmashauri zetu ni kitu ambacho hakiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililoliona kuwa ni changamoto ni suala la miundombinu. Tunatarajia twende kuzuri sana kama nilivyokwishatangulia kusema, lakini bado miundombinu iliyoko haitoshi kutufikisha. Katika maeneo ambayo tunaotoka wengi wetu hakuna malambo, hakuna barabara, hakuna majosho. Unapozungumza kwamba unaenda kuanzisha Sheria mpya na mtu akasajili kwa kweli unaweza kumwonea tu kwa sababu bado haujamtendea haki katika kuimarisha ile miundombinu ambayo ni mahitaji yake ya kwanza ya lazima katika kufanikisha ufugaji bora ambao tunaukusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lile la kulazimishwa kuuza. Katika mambo yote mabovu katika Wizara hii ya Mifugo ni uuzaji wa kiholela wa mifugo. Vitu vyote hapa vinauzwa kwa kilo, leo ukimwuliza Mheshimiwa Magufuli pamoja na uwezo wake mkubwa kukariri mambo hajui bei ya ng’ombe, ila anajua bei ya kilo ya nyama ya ng’ombe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo yetu yote nchini inauzwa kwa bei ya kulangua, inauzwa kwa bei ya kuangalia. Anakuwepo dalali pale, anaanza kumkadiria ng’ombe kwa kumwangalia sura, kwa kumwangalia rangi, lakini ukienda kununua kilo ya nyama unanunua kwa kilo. Kwa nini tusiweke miundombinu kuhakikisha kama nyama unanunua kwa kilo kwa nini tusiweke miundombinu kuhakikisha minada nayo imeanza kuwekewa mizani ili mfugaji huyu akauze kwa mizani, hata ukisema kwamba nenda kauze kwa amri ya Mahakama au kwa amri ya yule Msajili atajua nauza ng’ombe kwa bei gani. Lakini sasa nenda kauze yatatokea yale ya Ihefu. Wafugaji wameuza ng’ombe mpaka shilingi 5,000, tunawapeleka wapi Watanzania hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kupanga ni kuchagua. Lakini lazima uangalie dalili, dalili mtu mzima ukiambiwa inatosha elewa. Mimi ningeshauri naomba sana itumike busara, Miswada yote hii miwili irudi kwenye Kamati. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Selelii. Msemaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme kwamba mimi ni mmoja wa wajumbe katika Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo na nimeshiriki kama mjumbe kwenye Kamati. Tumeichambua, tumeshirikiana na wataalamu na wafugaji na wananchi wa kawaida katika *public hearing.*

Vilevile mimi natoka katika sehemu ya wafugaji, najua matatizo ya wezi wa wafugaji na hapa juzi tarehe 10 Aprili, nimepewa cheo cha kuwa Kamanda Mkuu wa Sungusungu katika Jimbo la Bukene. Kazi ya sungusungu ni kuangalia wezi na tunaamkiana kwamba; *“washosha-ng’ombe”* yaani wanaorudisha ng’ombe wanaoibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema hilo ili yanayofuata nitakayozungumza yaeleweke. Vilevile nawashukuru sana sungusungu wa Bukene kwa kunipa cheo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuelewa mambo yanavyokwenda hapa. Kwa sababu tunapozungumzia migogoro ya ardhi, tunapozungumzia sheria ya ardhi vijijini namba 5 ya mwaka 1999 ambayo kila siku tunahangaika kwamba wakulima na wafugaji wanagombana, sasa mambo yameonekana hapa tunaweza kutekeleza sheria ya ardhi ya vijiji ya mwaka 1999, namba 5 na kuhakikisha utekelezaji huu ambao haujatekelezwa miaka 11 tangu tumepitisha sheria hiyo.

Sasa tunataka uitekeleza hii ili ardhi ya wakulima ijulikane iko hapa. Na ardhi ya wafugaji iwe hapa, wengine wanaleta maneno mengine. Mimi nashindwa kuelewa hii sheria tuliyoipitisha mwaka 1999 na wenzao waliotangulia tulikuwa nao wengine humu tukapitisha na bado hatujatekeleza miaka 11; sasa bado tunataka tusiitekeleze sheria ya ardhi zaidi ya miaka 11, hivi kweli tunawatendea haki wananchi wetu wakulima na wafugaji ambao wataendelea kugombana na kuleta migogoro hiyo? *(Makofi)*

Mimi naomba kuunga mkono hoja hizi zote mbili asilimia mia kwa mia. Na sababu ninazosemea kuunga mkono ni kwanza tunatoa migogoro ya ugomvi kati ya mkulima na mfugaji. Hii sheria tukiipitisha hapa watu wa ardhi watagawa ardhi ya wakulima, watagawa ardhi ya wafugaji, na wafugaji hawatazurura tena kama ilivyokuwa zamani. Watatakiwa wakae kwenye ardhi yao wapate hatimiliki yao, wapange mipango kwenye ardhi yao, ugumu unakuja wapi? Mimi ninashindwa kuelewa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikija kwenye kugawa ardhi pale, mfugaji anatakiwa kupanga ardhi yake, ni wapi anaweka mifugo yake, mahali gani atalima kwa ajili ya malisho yake na anaweza kuweka vitalu vyake tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kitalu namba moja anaweza akakilima Januari, kitalu namba B akakilima Februari, kitalu namba C akakilima Machi, na kadhalika na vivyo hivyo atalisha mifugo yake kufuatana na kitalu. Mwezi Januari anaweza kulisha kitalu namba D, mwezi Februari akarudi kitalu namba A, huku akalima tena kitalu namba D. Halafu mwezi Machi akalisha kitalu namba B, Februari halafu akalima kitalu namba A, kwa hiyo anakwenda anabadilisha na pale pale anapata malisho na pale pale hazunguki na wala hamuudhi mkulima ambaye ng’ombe wake wanaweza kwenda kula mazao ambayo ni mahindi na chakula cha binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kui-*support* sana hii sheria kwa sababu ya utekelezaji wa sheria hiyo na vilevile kuondoa migogoro kama nilivyosema na vilevile kuzuia uhamaji hamaji wa wafugaji. Lazima tujifunze kukaa mahali pamoja, lazima tujifunze ufugaji ulio bora, sio wingi wa ng’ombe wengi lakini maziwa yake ni kidogo. Unakuwa na ng’ombe 1,000 lakini unapata lita 10 za maziwa. Unakuwa na ng’ombe mmoja unapata lita 70 za maziwa. Sasa ni lazima twende kwenye maendeleo, ni lazima tuhakikishe tunawatoa wafugaji wetu waende kwenye kupata faida, kwenye uchumi, kwenye kujikwamua kutokana na umaskini na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile kuzungumzia kilichonifurahisha zaidi, alama. Alama hizi zitawekwa kufuatana na kujua kwamba kwa mfano, ng’ombe huyu anatoka kwenye Jimbo la Bukene ambayo ni Wilaya ya Nzega. Kwa hivyo, kutakuwa na

alama inayoonesha kwamba ng'ombe huyu anatoka Nzega, anatoka Mkoa wa Tabora na huyu mwingine anatoka Mkoa wa Mara, hata wakiibiwa wanajulikana kwamba huyu ni wa Tanzania, huyu ni Kenya, huyu ni wa Uganda. Hata yakitokea magonjwa vilevile inakuwa ni rahisi kufuatilia kama nyama ya ng'ombe imeuzwa Dar es Salaam, au imeuzwa Nairobi, lakini hujui ng'ombe yule ametoka wapi.

Kwa hiyo, unaweza ukamfuatilia kwa taratibu kutokana na *data* zilizopatikana, kwa taratibu kujua ng'ombe huyu alifika kuuzwa Nairobi lakini alinunuliwa Dar es Salaam kwa Tanzania na alama hii ni ya Tabora, ukifika Tabora unajua alama hii ni ya Nzega na kadhalika, ili kuzuia magonjwa yasiongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaonunua ng'ombe wetu wasije wakatufungia tu kwamba ng'ombe wote wa Tanzania ni wabovu wana ugonjwa fulani, ambapo si sahihi. Pengine ni ng'ombe wa Mbeya tu peke yake ndio walikuwa na ugonjwa, lakini wa Tabora, wa Dodoma, wa Mara, wote wako *okey*. Kwa hiyo, kama ni karantini inafungwa basi inafungwa katika sehemu husika lakini ng'ombe wengine wanakwenda kuuzwa na hivyo wananchi wanapata mapato ya kutosha na kuondokana na umasikini kutokana na mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo, lakini bado...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:**...alah! Muda umekwisha!

**NAIBU SPIKA:** Bado moja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi niseme haraka haraka. Hizo alama zitatusaidia katika kuzuia magonjwa na mambo mengine. Halafu vilevile tumeambiwa alama hizi ni lazima ziwekwe kwenye masikio ili kuhakikisha kwamba wale wafugaji wanajua kwamba hata ngozi nayo ina pesa, lakini wakati huu sasa hivi tunawekelea tu, mnachoma lichuma hapa, ngozi inaharibika na ngozi na yenyewe ni thamani.

Kwa hiyo, na yenyewe iweze kuuzwa ilete faida kwa Mtanzania ambaye ni mfugaji; kwa hiyo, mambo yote ni alama kwa kweli, alama zinazopangwa kwa kweli ziandikishwe na wale wanaoondoka kama ng'ombe anatolewa kule Bukene, anakuja kupelekwa Dar es Salaam, anaandikishwa kutoka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanasema tumeshindwa kuandikisha watoto wa shule, sijui tumeandikisha wapi? Lakini mimi sikubaliani nao, tunaandikisha magari mengi sana na wala hakuna gari linalotembea bila *plate number*. Kwa hiyo, ni vizuri tukubaliane na kuamini kwamba ng'ombe wote au mifugo yote itaandikwa. Na yule aliyeandikwa vilevile hata kama akiiba, anaogopa kwa sababu kama vile unavyokuwa unaendesha gari ukipata ajali ukitaka kukimbia kidogo unajua kwamba eeh, labda watu wameniona kwa *plate number* yangu. Kwa hiyo, inasaidia kuwaweka watu wajue

kwamba tunakuwa raia wema. Kwa hiyo, naomba niongezee katika malisho na vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wataleta vyakula vya mifugo kutoka ndani na nje ya nchi. Lakini kuna madhara ambayo yanaweza kutokea kwenye chakula hiki kwa wale wengine ambao wanataka utajiri wa haraka. Maana tutakuwa tunawategemea ng'ombe kwa uzito na sio kwa wingi huko tunakokwenda. Ufugaji bora, maana yake ni uzito wa ng'ombe na sio wingi wa ng'ombe.

Kwa hiyo, Watanzania wengine walio wajanja, wanaweza kuwalisha hata dawa za *family planning* au *ARVs* ili wanenepe zaidi na kuhakikisha kwamba wanatuletea madhara zaidi. Kwa mfano nasema, sasa hii katika utaratibu ulivyopngwa tutahakikisha kwamba haya madhara yasije yakawekwa, tusiwekewe dawa nyingine katika viwanda vyetu vya ndani na dawa nyingine zinazotoka nje ya nchi kwa sababu yatatudhuru hapo baadaye. Utaratibu huu utatusaidia kuhakikisha dawa na vyakula vinavyotengenezwa viwandani, vinatengenezwa vizuri kwa ajili ya kutusaidia sisi walaji yaani *consumers* wa hapa ndani kutoka kwenye viwanda vya nje ya nchi na viwanda vyakwetu wenyewe hapa nchini.

Mheshimiwa naibu Spika, nafikiri kwa kifupi nimemaliza. Asante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa nashukuru, unajua kifungu cha 69, alichosema Mheshimiwa Sendeka, ni sahihi katika kufanya kazi zetu. Lakini pia kuna nafasi ya kutumia busara ya Spika, kwa sababu tungesema tuahirishe twende zetu, huu utajiri wa maneno yote tusingeupata. Kwa sababu, muundo wa Kamati zetu sasa hivi ni kwamba Kamati zinazohusika ndio zinajifungia kwenye chumba wanajadili mambo wengine mnakuja kuyasikilizia hapa.

Lakini tukikaa wote hivi, tunashirikishana na kujadili na mimi napenda *freedom* ya *discussions*, kusudi watu waweze kujadili kwa makini na kwa utaalamu unaostahili na baadaye tunafanya maamuzi.

Kwa hiyo, mimi nasema hata kesho tutaendelea, tutaanza na Mheshimiwa Ole-Sendeka, atafuata Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuata Mheshimiwa Tatu Ntimizi, atafuata Mheshimiwa Rosemery Kirigini na wako wengi tu; maana mko 24 lakini kwa nafasi tuliyojipa mnaweza kutosha lakini msilete majina mengine, haya yametosha. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kesho, kwa suala hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mengine; kesho Kamati ya Uongozi ya Bunge, hii ya Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu, tutakutana saa 05.00 asubuhi kwenye Ukumbi wa Spika. Halafu kesho pia kutakuwa na semina ya kuhusu kuangalia shughuli zilizofanywa na MKUKUTA kipindi cha kwanza na kuangalia MKUKUTA namba mbili, itakuwepo semina kwanza kwa Wabunge wote. Hii itafanyika saa 07.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa, kwa sababu ule ni mkubwa.

Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi, yenyewe itakutana kesho usiku saa 02.00 usiku baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge. Kwa hiyo, saa 05.00 asubuhi Kamati ya Uongozi ya Bunge kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu, halafu semina ya MKUKUTA saa 07.00 mchana baada ya kuahirisha kikao hapa na Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi, saa 02.00 usiku. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naomba niwashukuru sana kwa siku ya leo. Nategemea mtakuwa na mapumziko mazuri na mtaendelea kutafakari juu ya Miswada hii na kufanya *lobbing*, ndio utaratibu wa Bunge; kwa hiyo, nawatakia kazi njema usiku huu. *(Makofi)*

Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 15 Aprili, 2010 saa tatu asubuhi)*